

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Nane - Tarehe 12 Desemba, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae, Katibu.

KIAPO CHA UTII

SPIKA: Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro - aingie.

Mjumbe afuataye hapa chini aliapa Kiapo cha Utii na kukaa katika nafasi yake ndani ya Ukumbi wa Bunge

Mhe. Asha-Rose Mtengeti Migiro.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka 2012.

MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka 2012.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge leo ni siku ya Alhamisi, tutakuwa na Maswali kwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani simwoni basi tunaenda na Waheshimiwa Wabunge waliomba. Tunaanza na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katibu Mkuu wa Chama cha CCM, Mheshimiwa Abdulrahman Kinana pamoja na Katibu Mwenzezi wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Nape Nnauye, wakiambatana na Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, ambaye ameapishwa sasa hivi humu Bungeni kuwa Mbunge, walikuwa katika ziara Mkoani Mbeya wakifuatilia Ilani ya Chama cha Mapinduzi alisema kuwa kuna baadhi ya Mawazi ni mzigo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RUKIA KASSIM AHMED]

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe kama mfuatiliaji wa shughuli za kila siku na kiongozi wa Serikali umeichukuliaje kauli hiyo? *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo tu kwa ufupi tu kwa dada yangu Rukia na mimi niliyasikia kwenye vyombo vya habari na kwenye magazeti wameandika. Lakini kiutu uzima huendi na yanayosemwa kwenye magazeti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi tunangoja arudi, tutakaa naye tumsikilize alichokuwa anasema ni nini na naamini atakuwa na Wizara kadhaa kichwani mwake. Halafu tutaona sasa namna ya kwenda mbele pamoja. *(Makofi)*

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hata hivyo juzi tu tulipokuwa tukijadili taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na Serikali za Mitaa. Kuna Mbunge wa CCM ambaye alinukuu kauli hii ya Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM na akasema kuwa kama kuna mzigo basi mzigo nambari moja ni wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa je, kauli kama hii ambayo imetoka ndani ya chama chako unawaambiaje Watanzania kuhusu hili. *(Makofi)*

SPIKA: Haikutoka ndani ya Chama ilitoka ndani ya Bunge. *(Kicheko)*

WAZIRI MKUU: Najaua pengine ulikuwa unalenga huko zaidi pengine vile vile ulikuwa unazunguka tu. Unajua kuna *personal judgments* juu ya mtu, kila mmoja anamhukumu mtu kutegemea na alichonacho kwenye fikra zake. Waziri Mkuu huyu anasimamia Wizara zaidi ya 20, kama utamhukumu kwa sababu ya Wizara moja au mbili humtendei haki vile vile. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Kwa sababu hawezi kuwa nzuri kwa Wizara zote isipokuwa moja na hiyo moja ukasema basi utabeba msalaba huo. Lazima ulitazame jambo kwa mapana upime upana wa kila Wizara inavyofanya kazi kwa sababu mimi kazi yangu ni usimamizi.

Kila Waziri analo eneo lake. Kwa hiyo, inawezekana kabisa pengine Mbunge alikuwa analisema, lakini ningekaa naye mimi kichwani angeniambia wewe upungufu wako sikupendi kwa sababu ya moja, mbili, tatu. Kwa hiyo, mimi nadhani ni kitu kinataka tu watu kukaa pamoja na kujaribu kuona tufanye nini. Lakini kwa upande mwingine dada yangu wala hili lisikusumbue, unajua uzuri wa nafasi hizi huombi. *(Makofi)*

Ni Rais kwa maongezi yake kichwani na anavyojaliwa na Mwenyezi Mungu anaamua kusema ngoja nimpe dada Rukia kuwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, isipompendeza ni kazi rahisi sana kwake. Ni kuamua tu kusema Pinda nimeona nikupe jukumu *you are not performing*. Unatoka wala hunung'uniki, sana sana utacheka na kusema ahsante sana. *(Makofi)*

Lakini upande wa pili, Bunge mnaweza vile vile kumwondoa Waziri Mkuu kwa uwezo mlio nao. Kwa hiyo, dada Rukia kama umefika mahali unaona na wewe unaliafiki na unafikiri Wabunge wote hawa wanaliona hivyo, mimi nitakuwa tayari mkiniweka kiti moto, tena utashangaa, nitafurahi kweli kweli kwamba la angalau nimepumua kidogo. Kwa sababu kazi hii ni mzito sana, tunaibeba kama msalaba, tunajitahidi sana. Lakini naelewa wakati mwingine hatuwezi kuwa *perfect* kwa kila kitu kama ilivyo kwa binadamu wote.

Kwa hiyo, tunaendelea kujitahidi kadiri ya uwezo wetu wote, Mawaziri wangu na mimi mwenyewe, kufanya kazi kuwa nzuri zaidi. *(Makofi)*

MHE. ENG. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali, sasa kuna mambo yanatokea inaonekana dhahiri Serikali yako inadharau muhimbili wa pili wa Bunge ambao ni Bunge. Nikisema hivi itakuwa hujafahamu vizuri. Lakini bora nifafanue. Ilikuwa kauli ya Mawaziri hapa Bungeni, nakala ninayo kuhusu chenji ya rada, au chenji ile ya rada *by system problem, pound* za Kiingereza milioni 30. Ukazuka mjadala kwa nini fedha ile itumike kwa shule za Tanzania Bara tu na sisi baadhi yetu tukasimama hapa kuomba miongozo mbalimbali na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Nyongeza ya kwanza kile kifungu cha (2) kuhusu mambo ya nje, kifungu cha 11 kuhusu anga, posta na simu. Kifungu cha 12 kuhusu fedha na sarafu, vyote vinathibitisha kwamba jambo lile ni jambo la Muungano.

Baada ya mzozo ule Kiti, (Mheshimiwa Spika), akatoa mwongozo. Akasema pande zinazohusika zikakae. Huo ulikuwa ni mwezi Mei, 2013. Pande zinazohusika zikakae zitafute ufumbuzi wa suala hili. Kuanzia tarehe hiyo mpaka leo hatujaona chenji ya rada kwenda Zanzibar, hatujaona mrejesho wa mwongozo wa Kiti mpaka leo kimya.

Je, kwa nini tuiseme Serikali inadharau muhimili huu wa Bunge?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mnyaa yaani na wewe umekaa muda wote huo mpaka leo ndiyo unakuja kujaribu kulizungumza hili kwa nguvu zote hizo? Kwa nini hapo katikati tusingekutana basi tukajaribu kuona kumetokea nini na pengine tukalimaliza *okay*.

Sasa nakumbuka yaliyojiri wakati ule na mimi najua jambo hili tulilizungumza. Sasa labda anipe tu nafasi. Mimi kazi yangu ni ku-*cross check* tu. Nione katika yale tuliyokuwa tumekubaliana kwa nini hili unalolisema halijatekelezwa, na ungekuwa umeni-*tip* mapema pengine ningekuwa nimeshapata na jibu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Lakini kwa sasa sina jibu la uhakika kwamba ni kitu gani kimejiri. Lakini jambo hili tulilizungumza ndani ya Serikali tukakubaliana na likaisha. Ndiyo maana nikasema bahati mbaya tu siku zote Mheshimiwa Spika, huwa naomba sana kama unaona ni kitu unataka upate jibu la uhakika zuri, wewe ni-*tip* tu kidogo tu. Bwana fedha ya rada ile Zanzibar hatujapata pesa, *full stop, I will look for it*. Unajua kichwa kimoja hiki kina vitu vingi na kusema utakumbuka kila kitu wakati mwingine *it is not easy*.

MHE. ENG. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:

Nashukuru kwa jibu zuri sana la Mheshimiwa Waziri Mkuu na mtasubiri baada ya yeye ku-*cross check* hatua zilizofikia. Lakini Mheshimiwa Spika naomba baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ku-*cross check* hatua zilizochukuliwa, naomba pia Bunge hili tupate mrejesho zile nyumba 1,196 zilizokusudiwa kujengwa za shule za msingi za walimu na vile vitabu. Je, fedha ile ni kweli imetumika kwa zile shughuli za msingi zilizokusudiwa kwa upande huu wa Tanzania Bara? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, Nyumba za nini?

MHE. ENG. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:

Nyumba za walimu, zilipangiwa mpangilio au kama nikupe ninao hapa. Zilipangiwa nyumba 1,196 za walimu wa shule za msingi vijijini. Zilipangiwa kununua madawati laki mbili (200,000/=). Zilipangiwa kununua vitabu laki moja na tisi na mbili. Kununua vitabu milioni 4.4. Kwa hivyo zilipangiwa kwa huo huo mpango kwa upande wa Tanzania Bara. Utekelezaji wake pia tungependa kuona, kwa huu upande wa Tanzania Bara. Pia umetekelezwa kwa kiasi gani? Ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Tutajitahidi tutajaribu kutoa maelezo.

Kwa sababu unajua ni jambo la Kisekta. Kwa hiyo, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, najua yuko hapa. Kwa hiyo tutamtaka tu aandae maelezo mazuri tuone jambo hili limefikia wapi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge ni kosa kubwa kwa Mbunge na au Serikali wakati mwingine kuweza kutoa ahadi za uongo Bungeni. Kwa miaka takribani zisizopungua mitatu mfululizo kwa maana ya miaka ya fedha ya Serikali, Serikali yako ambayo kwamba pengine unaiongoza imekuwa ikiahidi kuweza kutekeleza majukumu yake katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali iliahidi kuweza kujenga barabara ya Kigahwe-Nyakanazi, ambapo fedha kiasi kisichopungua bilioni 6 zilitengwa.

Mwaka uliofuata zilitengwa si chini ya bilioni 2, mwaka uliofuata tena ambao uliishia Juni mwaka, 2013 zilitengwa bilioni 3.5. Lakini hadi leo hakuna hata senti moja, hakuna kazi yoyote ambayo imefanyika. Swali langu, ni lini Serikali itaepuka tabia hii ya kuwa wakati mwingine inawahadaa wananchi na sisi Wabunge hapa Bungeni? *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba tu nimjibu Mheshimiwa Kafulila kama ifuatavyo. *Sorry1*

SPIKA: Ni hao hao tu. *(Kicheko)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Machali. Swali lake ni zuri tu na nafikiri kila sababu ya kuomba maelezo. Kitu kimoja ambacho sikukifurahia sana maana na mimi ni binadamu vile vile ni kutokuanza na ku-*appreciate* kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana katika Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Sasa inawezekana zile barabara zilizoko Mkoa wa Kigoma hazijafika Jimboni kwako, hilo nalikubali. Lakini kwamba tunatoa ahadi za uongo hatutumizi, lakini wakati ule ule Kigoma leo ukienda ina barabara nzuri, kidogo si mzuri sana. Nadhani ulitakiwa uanze na setensi moja nzuri tu halafu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

baadaye ndiyo unichape hilo swali. Kwa kifupi nilitaka kusema nini, nilitaka kusema tu kwamba kazi kubwa imefanyika Mkoani Kigoma, nadhani wananchi wa Kigoma wanajua. *(Makofi)*

Ni kweli barabara hiyo ni sehemu ya barabara ndani ya Mkoa wa Kigoma ambao tuliahidi kwamba itajengwa na mimi nataka nikuambie Mheshimiwa Machali itajengwa. Kuna kuchelewa, lakini kuchelewa haina maana kwamba halitanyika. Kwa sababu ni suala la Bajeti na namna mnavyoipanga. Sasa tumejitahidi tumetoa baadhi ya maeneo tukayapa kipaumbele usije ukafikiri kwamba pengine tumepuuza sana jambo hili.

Hapana mimi nataka nikuahidi barabara ile ni sehemu ya ahadi ya Serikali iko kwenye utaratibu ni kweli fedha inayotengwa inaweza ikaonekana ndogo, lakini barabara hiyo itajengwa tena mie naamini kabla ya 2015 tutakua tumeanza kujenga ile barabara.

Barabara ile unayoisema wewe kwangu mimi vilevile ina umuhimu wake, ni barabara hiyo hiyo unaanzia Nyakanazi, unakuja nayo unapita Kigoma, hiyo hiyo inakuja mpaka Mpanda. Ndiyo maana nasema barabara hiyo itajengwa na mimi nataka nikuhakikishie niwahakikishie na watu wa Kigoma tusiwe na mashaka juu ya jambo hili, kazi itafanyika. *(Makofi)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na majibu yako ambayo kidogo yanatia matumaini, lakini haya majibu siku zote na mara nyingi tumekuwa tukielezwa hivyo.

Nilikuwa naomba pengine kuweza kupata *commitment* ya Serikali kwa kuwa mwaka huu wa fedha ambao utaishia Juni, mwakani 2014. Serikali pia imetenga Biloni Kumi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ile. Unaweza pengine kunyahidi nini kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma na Watanzania wengine kazi hii ambayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOSES J. MACHALI]

tumekuwa tunasikia kwamba zabuni imeshatangazwa. Unaahidi nini kuhusiana na kusukuma suala hili ili kusudi sasa isije kuwa kwamba kila siku ni ahadi itafanyiwa, mchakato unaedelea na vinginevyo. Nini kauli ya Serikali Mheshimiwa Waziri Mkuu?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba ni swali la Kisekta, naomba wengine msulize maswali ya kisekta. Waziri Mkuu najua utajibu kwa sababu barabara yenyewe inawaunganisha nyie wote. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Moses Machali ushauri wako tutauzingatia. *(Makofi)*

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miaka mingi sasa tangu tupate Uhuru tumekuwa tukisikia kwenye vyombo vya Habari na vingine tukiona kwa maana kwenye TV na Magazeti Meno ya Tembo yakikamatwa kama ilivyo katika Madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya yakikamatwa kesi zikienda mwisho wa siku tumekuwa tukiona yanateketezwa. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa tumekuwa tukipitisha Bajeti na kwa kuwa meno mengi sana ya Tembo yamekatwa tunataka tufahamu Taifa limenufaika kiasi gani ama imeyauza wapi hayo meno ya Tembo ambayo yamekamatwa tangu mwaka 1961.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, zipo taratibu zinazotawala masuala ya nyara za Serikali. Kwa kawaida kinachotokea meno mengi yanayokamatwa haya yanahifadhiwa. Kwa hiyo, ukienda pale kwenye Jengo lile la Nyara pale ndiyo hasa Ghala kubwa ya Meno ya Tembo. Kumekuwa na jitiada za Serikali kujaribu kuona kama tunaweza kupata kibali kupitia vyombo vya Kimataifa. Turuhusiwe kuweza kuyauza yale Meno.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Baada ya kuyauza fedha zile tukazi-*ireinvest* kwenye sekta hiyo hasa kwenye suala zima la kuimarisha ulinzi pamoja na jitihada zingine zakupambana na ujangili. Lakini kwa bahati mbaya katika *attempt* tulizofanya hatukufaulu sana.

Lakini hatujakata tamaa bado tunadhamiria tujaribu tena kujieleza ili watuelewe dhamira yetu kwamba ni kujaribu kujenga uwezo wa vyombo vyetu ili tuweze kukabiliana na jambo hili kikamilifu. Kwa hiyo ni matumaini yangu kwamba wakituelewa pengine tutapa hiyo ridhaa ili tuweze kuendelea na zoezi hilo.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nakusukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru kwa majibu yako. Nakwakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amekiri, kwamba Sheria za Kimataifa mpaka sasa zinakataza kuuza Meno ya Tembo Nje ya Nchi. Kwa kuwa wanaokamatwa wanajua masoko yanapouzwa hayo meno ya Tembo sasa unajua Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu imeshapita miaka mingi mtueleze na ninyi hamuwezi kutumia namna hayo meno kuuzwa ili hiyo sekta iende vizuri?

SPIKA: Akawatafute wale wenye meno yao?
(*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufanya hivyo kama Taifa, kwa sababu unajua katazo hili ni la msingi ingekuwa ni kitu kinawezekana *of course* tungeweza na sisi tukawa majangili wa njia nyingine lakini kwa njia hiyo tutakuwa tunakosea sana taratibu za Kimataifa. Ndiyo maana hata kwenye *National Parks* unaweza ukaenda pale ukawa unakula ugali na maharage kila siku ingawa kila kukicha unaona Swala wako pale, Isha wako pale lakini ni katazo la msingi huwezi ukaua au ukala nyama ndani ya eneo lile hata ingekuaje, na sisi wa pande huo ni hivyo hivyo. Meno yapo lakini hatuwezi kufanya hili unalo nishauri kwa babau ni kinyume cha taratibu mpaka tupite kwenye mkondo huo huo tukikubalika *fine* ndiyo tunaweza tukalifanya hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya watu kupigana risasi barabarani na sehemu mbalimbali na inaonekana kwamba kuna idadi kubwa ya vijana wengi ambao wamemilikishwa Bastola ama kwa kutozingatia vigezo, ama kwa sababu zingine ambazo hatuzijui.

Je, Serikali ina mpango gani yakufanya *auditing* ya watu wanaomiliki silaha ndogo aina ya Bastola ili kuzuia majanga yanayojitokeza kwa sasa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ziko Sheria *of course* zinatawala umiliki wa Silaha ambazo kila Mtanzania mwenye Silaha anapaswa kuzingatia. Lakini ipo *element* vile vile ya uhalifu ambayo na wenyewe lazima vilevile tukubali ipo. Lakini wakati mwingine ni matumizi ambayo si sahihi ya Silaha hizo hizo ambazo unaweza ukawa unaimiliki kihalali lakini unaitumia vibaya.

Kwa hiyo, Serikali ambacho imekuwa ikifanya muda wote mara nyingi nikufanya *operations* katika baadhi ya maeneo na hasa kwenye Majiji Makubwa kama Dar es Salaam na mara kadhaa kweli wamekamata silaha.

Lakini mara nyingine wametumia utaratibu mzuri tu wa kutoa wito kwa Watanzania, kuwasilisha zile Silaha wenyewe kwa hiyari yao na kuweka *grace period* ya msamaha kwa wengine wamekuwa wakiridhika *effectively* lakini bado mimi nafikiri na nakubaliana na wewe kabisa kwamba tuendelee kama Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuchukua kila hatua itakayowezesha kupunguza matumizi mabaya ya Silaha zetu. Ndiyo maana mle unaambiwa kabisa usiazimishe Silaha kwa mtu hata kama ni ndugu yako kiasi gani kwa sababu nikinyume cha taratibu. Kwa hiyo mimi nadhani ushauri wa Ndugu Lema ni sahihi na ninafikiri Wizara imesikia na tutajitahidi kuona juhudi hizo ziendelezwe zaidi. (*Makofi*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kuna baadhi ya ushahidi upo hata kuna baadhi ya watu ambao wameshawahi kuwa vichaa na kulazwa hata Mirembe wanamiliki Silaha. Sasa ni kwa nini Serikali isifanye uchambuzi ya watu wanaomiliki Silaha kwa sasa *especially* katika Jimbo langu watu wengi sana wanamiliki Silaha kati ya vijana labda 100 unawakuta labda vijana 80 lakini ukiangalia *Contexts* ama jinsi alivyopata ile Silaha inaleta mashiko makubwa sana. Sasa ni kwa nini lisiwe agizo labda la Serikali kwamba watu wanaomiliki Silaha wafanyiwe uchunguzi waone kama bado wanastahili kumiliki silaha tofauti na utaratibu wa sasa ambao kila mtu anamiliki kihalali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Lema swali la nyongeza kama ifuatavyo. Bado nazani sijaukataa ushauri wako ni mzuri tu. Ukikumbuka siku za nyuma hapo, sikumbuki kama miaka miwili au mitatu hivi Mambo ya Ndani walichukua hatua la kujaribu kufanya hilo zowezi yaani ilibidi kila mmoja aende, yaani ilibidi kila mmoja aende kupeleka Silaha na kuthibitisha kwamba Silaha ile ni ya kwake pamoja na Hati ile *Document* ambayo inaitajika. Lakini jambo hili ni lazima kuendelea kuwa ni *processes* isiyo koma baada ya kumalizika. Nadhani iko haja yakuliendeleza kila wakati.

Kwa hiyo, bado umetoa *specifically* hasa kwa eneo lako la Arusha mimi nafikiri tutawashauri watu wa Mambo ya Ndani ya Nchi kama wakiona inawapendeza jambo hilo basi pengine waanza na Jiji la Arusha lile, baadaye twende kwenye maendeleo mengine. Lakini uchunguzi ni muhimu, ni muhimu sana. (*Makofi*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Bunge hili kwa muda mrefu Wabunge tumekuwa tukijenga hoja na kulalamika kuhusu uwezo mdogo wa Serikali kuongeza mapato. Uwezo mdogo wa Serikali kuongeza mapato, kimekuwa chanzo kikubwa kwa miradi mingi ya Maendeleo kutokutekeleza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID Z. KAFULILA]

Mheshimiwa Waziri Mkuu na miongoni mwa mapendekezo ambayo yametolewa kwa muda mrefu bila kutekelezwa ni pamoja na utekelezaji wa Sheria mpya ya manunuzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 ilifanyiwa madiliko mwaka 2011 lakini tangu mwaka 2011 leo ni mwaka wa tatu (3) Wizara ya Fedha, haijaleta Kanuni. Wabunge wote wa Upinzani na Chama Tawala mara kadhaa wamekuwa wakisisitiza kuhusu tatizo hili kwa sababu Sheria hi ya manunuzi ya leo bidhaa ya shilingi mia moja unanunua kwa shilingi mia nne mpaka mia tano.

SPIKA: Mheshimiwa Kafulila, unatosha huo huo mfano mmoja. Uliza swali.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali. Mheshimiwa Mkuu kwa kuwa Sheria hii sasa ya manunuzi imekuwa ni mzigo nimepigwiwa kelele kwa muda mrefu kwa takribani miaka mitatu (3).

Je, hauoni huu ni ushahidi kwamba Serikali hii ni mzigo kwa kushindwa kutengeneza Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya mwaka 2011?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tutakuwa tunatumia neno mzigo vibaya tu, kwa sababu haiwezekani kila jambo ni mzigo ni mzigo.

Kwa hiyo, hata Kanuni tu hapa hata Serikali ni mzigo, haiwezekani haiwezekani. Je, jambo hili linajulikana, sisi tunalijua na tumekuwa na wasiliano ya karibu. Tumejitahidi sana kuiangalia ili tuweze kulikamisha lile zoezi. Lakini *of course* ndani yake kuna mambo mengine ambayo inabidi tuyafanyie kazi kwa nguvu sana. Ni lazima vilevile tukubali kwamba Kanuni hazitakiwi kupingana na Sheria mama yenyewe.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Kwa hiyo kuna mawazo mle ambayo mengine ni mazuri sana lakini ki msingi pengine yatabadilika kwanza tufanye mabadiliko kwenye Sheria yenyewe. Vinginevyo hayo unayoyasema mengine yanaweza yasipate *room* ya kuweza kuwa *accommodated* kwa njia ya Kanuni. Tumeshirikiana sana na vyombo mbalimbali vya nje na ndani. Kwa hiyo, tunadhani tumeishafika pazuri, haitachukua muda mrefu sana kabla hazijatoka.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, miaka mitatu kwa kutengeneza Kanuni inatosha kuthibitisha Bunge hili kwamba ni muda mrefu kupita kiasi. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, siyo hiyo tu. Mwaka 2010, ilipitishwa Sheria ndani ya Bunge hili Tukufu iliyosainiwa na Mheshimiwa Rais mwezi wa Julai, tarehe 28. Sheria ya kutaka Makampuni ya Simu yaorodheshwe kwenye soko la mitaji kama moja ya njia ya kuhakikishia Serikali kupata mapato stahiki kupitia Makampuni haya ya simu ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakikwepa kodi.

Naomba nimwulize Waziri Mkuu hili nalo tangu Sheria hii imepitishwa leo ni mwaka wa tatu. Kanuni za kutekeleza Sheria hiyo bado hazijawa gazetted. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Mkuu wa Serikali ambaye hili jambo unalifahamu kwa kina kama chanzo cha mapato.

Je, na lenyewe bado ni kwa nini unaweza kuwaeleza Watanzania Kanuni zake bado hazijawa gazetted ili kusudi Serikali ipate mapato stahiki?

SPIKA: Mheshimiwa Kafulila kwa kweli swali hili na wewe mwenyewe *concisely* unajua siyo sawa, siyo nyongeza wala nini ni lingine. Ni lingine Kafulila tuache ubishi tu ni lingine hili swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ajibu kwa nini na mimi ndiye naendesha kikao! Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ujibu. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri cha msingi anachokisema Mheshimiwa Kafulila ni ile kwamba harakisheni hilo jambo na lenyewe liishe. Kwa hiyo,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

tutajitahidi na lenyewe liishe. Lakini usione kwamba tumelinyamazia ukafikiri hakuna sababu hapa, ziko sababu nzuri ambazo zinatufanya wakati mwingine tuchukue mda mrefu kidogo. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumemalizana ndani ya Serikali tutalikamilisha.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa kwa ujumla wake kumekuwa na tatizo kubwa sana la fedha za maendeleo kwenda katika maeneo mbalimbali zilizopitishwa na Bunge hili hili.

Kwa mfano, kwenye maeneo ya Halmashauri fedha haziendi, hasa za maendeleo, kwenye Wizara vilevile hasa Kilimo, Afya, Maji ambazo Wizara zinazogusa maendeleo ya kila siku ya wananchi wetu. Nataka nifahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu lipo tatizo gani Serikalini linalo sababisha sisi tunapitisha Bajeti hapa halafu fedha za maendeleo haziendi kwa wananchi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nafikiri ilikuwa jana, nathani alikuwa Mwenyekiti wa kamati ya Bajeti nadhani ndiyo aligusia jambo hili. Tatizo linalojitokeza katika uendeshaji wa shughuli za Serikali ni pale ambapo robo ya kwanza ya mwaka inakuwa ni robo yenye matatizo kwa maana ya makusanyo ndiyo msingi unaanzia pale. Lakini lilitoka wazo hapa kwanini Serikali isitafute namna nyingine yoyote ya kuweza kupata mkopo wa kutuwezesha mwanzo wa mwaka tuwe na fedha ambazo zinatuwezesha kwenda kwa ajili shughuli za maendeleo.

Sasa safari hii tuli-*attempt* lakini bado ilikuwa ni ngumu kutokana na taratibu za kifedha zilizavyo. Lakini bado hatujakata tamaa tunaendelea kulifanyia kazi, kwa sababu tukifaulu hilo, utaona *flow* yake sasa itakuwa ya uhakika zaidi.

Lakini makusanyo kusema kweli mie nilipozungumza na watu wa *TRA* wanaanza kupata auweni mwezi Septemba, Oktoba, Novemba, Desemba ndiyo inakuwa *the highest pick*. Kwa hiyo, iko haja ya kutazama hili suala kwa maana ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kuona *what can be done* kwenye *first quarter* ili tuweze kuwa na fedha za kutosha na *flow* nzuri ya fedha za maendeleo *all through*. Sasa zinapokuja kupatikana baadaye unakuta bado *effectiveness* inakuwa ndogo sana.

Kwa hiyo nakubalina kabisa na rai ya Mheshimiwa Nkumba lakini tunajaribu ku-*deal* na uwezekano wa kupata mkopo kutoka kwenye vyombo katika *quater* ya kwanza.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, swali dogo tu, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa ni ukweli usiopingika kwamba mgawanyo vilevile wa fedha kwa maana kwa maana ya mgawanyo wa fedha za utawala na zile fedha za maendeleo. Utaona kwamba fedha za utawala pamoja na kwama tuna fedha kidogo fedha za utawala zinapatikana lakini zile za maendeleo hazipatikani.

Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama utakubali ushauri wangu kwamba ingekuwa vizuri sasa katika Bajeti zinazofuata tukaangalia kwa namna ya pekee, ni namna gani tunaweza ku-*balance* hizi fedha kwamba angalau fedha za utawala zikaendelea lakini fedha za maendeleo na zenyewe zikaendelea ili kile tunachokigawana kika - *balance* kote kote utawala ukaendelea na shughuli zake. Lakini na Maendeleo ya wananchi wetu yakapatikana vilevile.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni ushauri mzuri na Serikalini tunajaribu kulizingatia lakini nataka nijaribu tu nimwonyesha kwamba siyo kweli sana kwamba fedha ya utawala ndiyo inapatikana kuliko fedha ya Maendeleo hapana. Kwa wale tulionko Serikalini wenzangu hapa wataungana nami mwezi Julai, 2013 kwa mfano hatukuwa na *OC* tuliyoitoa.

Mwezi wa Agosti, 2013 hatukutoa *OC* hata kidogo. Fedha ile ambayo tulikuwa tunafikiria ingeweza kutusaidia ndiyo tukajaribu tukaiwekeza kidogo kwenye *Development Budget* ili tuweze angalau mambo yaende. Ukienda Serikalini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kilio kikubwa tu ni kwasababu ya OC inayopatina ni kidogo sana kwa sababu tunajaribu ku-*balance* kwamba fedha za maendeleo kwa vyovyote vile lazima zipatikane ilia mambo yaweze kwenda hata kama tuna tatizo la ukusanyaji wa mapato.

Lakini *same time* lazima tuwashukuru sana TRA wanafanya kazi kubwa na niwaombe Watanzania kwa kweli, waendeleo kuungana na TRA katika jitiada zake za kuongeza mapato. Nashukuru sana jambo hili la mashine limeanza sasa kueleweka vizuri. Kwa hiyo, naamini na lenyewe litatusaidia sana kuweza ku-*capture* baadhi ya kodi ambazo zilikuwa hazipatikani kwa urahisi. (*Makofi*)

SPIKA. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali yamekwisha na muda umekwisha. Niwashukuru pia wote waliouliza maswali na tunapozungumza jambo tunapenda watu wasijenge *presidence* kwamba unapouliza swali la nyongeza unaleta swali lingine. Unauliza lile lile, unaongeza maelezo kwa lile swali la kwanza, ndivyo Kanuni zinavyo tudai. Kwa hiyo, naomba tuendeleo na hatua inayofuata, katibu. (*Makofi*)

MASWALI YA KAWAIDA

Na. 82

MHE. AZZA HILLAL HAMAD (K.n.y. MHE. AHMED ALLY SALUM) aliuliza:-

Jimbo la Solwa lina upungufu mkubwa wa Waganga kwenye Zahanati na Vituo vya Afya.

Je, Serikali itapeleka lini Waganga wa kutosha katika jimbo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunikaribisha tena, wanawasalimia watu wa Japan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Solwa lipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinganya ambayo ina upungufu mkubwa wa Watumishi sio katika Sekta ya Afya tu kama zilivyo Halmashauri nyingi za pembezoni. Serikali imeendelea na jitihada katika kuhakikisha watumishi wanapelekwa katika mikoa na Halmashauri ili kupunguza upungufu wa watumishi uliopo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ina jumla ya Vituo vya Afya 4 na Zahanati 31. Kwa upande wa watumishi wa Afya waliopo ni 203 katika fani mbalimbali za afya ambapo kuna upungufu wa watumishi 392 kwa mujibu wa ikama ya mwaka 2013/2014.

Serikali inatambua upungufu huo uliopo na imekuwa ikifanyia kazi kwa awamu katika kila mwaka wa fedha. Mwaka wa fedha 2012/2013 kulikuwa na Madaktari Wasaidizi 4, Matabibu 31 na Matabibu Wasaidizi 12. Mwaka wa fedha 2013/2014 kulikuwa na Madaktari 2, Madaktari Wasaidizi 4, Matabibu 31 na Matabibu Wsaidizi 12.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imekuwa ikiwasilisha maombi ya kuajiriwa kwa Wtaalam mbalimbali wa Afya katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambao wamekuwa wakitoa vibali vya kuajiri kulingana na upatikanaji wao kufuatia kukamilika kwa Mafunzo yao. Mwaka 2012/2013 Halmashauri iliomba kibali cha kuajiri waganga saba (7) na kupata kibali cha kuajiri watumishi (3). Aidha mwaka 2013/2014 wanasubiri kibali cha kuajiri waganga 10. Hivyo Serikali itaendelea kuwapanga watumishi wa kanda ya Afya kwa kadiri watavyopatikana kwenye soko la ajira.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kwa kutambua changamoto hii, imekuwa ikishirikiana na Shirika la Mheshimiwa Benjamin Mkapa (*BMAF*), ambapo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Shirika litapeleka Madaktari 2. Wataalam wa Maabara 2 na Manesi 2 jumla ya watumishi sita (6) katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Hii ikiwa ni katika jitihada za kukabiliana na upungufu huo wa watumishi. (*Makofi*)

MHE. AZZA HILLAL HAMAD: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri na jitihada kubwa ambazo inafanya kwa ajili ya kutupatia watumishi hao. Sasa ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri Swali Moja la Nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Jimbo la Solwa, kwa muda wa miaka mitatu (3) sasa haina Mganga Mkuu wa Wilaya kwa maana ya *DMO*.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu mkubwa wa kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Mganga Mkuu wa Wilaya? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Azza H. Hamad, kama ituatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli anachokisema. Hospitali hii inajengwa na tumekwenda kule tumeiona. Kutokuwa na Mganga Mkuu wa Wilaya ni upungufu mkubwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Lakini *all along* wamekuwa wanatumia Hospitali ya Mkoa pale ndiyo ambayo imekuwa inasaidia, anayo *point* ya msingi hapa tutaendelea kushirikiana na yeye. Na hili tunalichukua kukuhakikishia kwamba tutashughulika tuone kwamba tunampata Mganga Mkuu kwa ajili ya Wilaya. *(Makofi)*

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utawala bora, inasikitisha sana kuona watumishi hasa wa Wizara ya Afya kwa maana ya Zahanati na Vituo vya Afya wanapewa barua za uhamisho, kumtoa kwenye kituo kimoja kwenda kwenye kituo kingine bila kuleta mtumishi mwingine katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, ni nini kauli ya Serikali katika hili kwa maslahi ya wananchi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agripina Buyogera, kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema kwamba kama unamhamisha Daktari, unamwondoa eneo moja kumpeleka eneo lingine ni upungufu mkubwa. Kwa sababu pale alipondoka wananchi wale watakuwa hawapati huduma.

Tatizo langu ni kwamba nimeshindwa kumpata vizuri. Hapa anazungumzia katika *leve/ ipi*. Kwamba anahama kutoka Halmashauri moja anakwenda katika Halmashauri nyingine, au humo humo ndani ya Halmashari. Ambayo hiyo kama iko katika Wilaya ya Kasulu hilo ni la kwangu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Hilo ni la kwentu sisi wote kwa pamoja tutakwenda sisi tutazungumza na Mkurugenzi Mtendaji na tutaomba Mheshimiwa Mbunge atupatie hivyo vituo ambavyo watu wamehamishwa tu halafu hakuna *replacement*. Huwezi kujibu, jibu tu bila uhakika.

Hapa nikajibu tu haraka haraka, nikasema hivi unaweza kukuta pale ameondoelewa *Gainacologist*, amepelekwa kule. Halafu akinamama huku wanaendelea kujifungua halafu tukalionga ni jambo la kawaida.

Hili ni jambo ambalo tutalishughulikia Mheshimwa tunaomba utusaidie vizuri kuhusu hizo *transfer* unazosisema ili tuweze kuchukua hatua stahiki. (*Makofi*)

Na. 83

Ufumbuzi wa Migogoro ya Mipaka Wilayani

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Serikali imeshindwa kutatua migogoro ya mipaka kwenye Mikoa na Wilaya. Kwa mfano mgogoro uliozuka kwenye mpaka wa Wilaya ya Sikonge na Manyoni.

Je, ni mamlaka gani inayoweza kutoa ufumbuzi wa migogoro hiyo hususan kati ya Wilaya hizo mbili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John P. Lwanji, kama hivi ifuatavo:-

Mheshimiwa Spika, mamlaka zenye uwezo wa kutoa ufumbuzi wa migogoro ya mipaka kwenye Mikoa na Wilaya ni Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja Mikoa na Halmashauri zinazohusika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ulikuwepo mgogoro wa mpaka katia ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge ambao ulikuwua unahusisha Kijiji cha Kalangali. Mgogoro huu ulipatiwa ufumbuzi mwaka 2010 ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia kikao cha pamoja cha tarehe 22 Aprili, 2010 walikutana hapa mjini Dodoma.

Kupitia kikao hicho ilikubalika kuwa Tangazo la Serikali (GN) Na. 27 ya mwaka 1961 ndilo litumike kueleza mipaka kati ya Wilaya ya Sikonge na Manyoni. Ilionekana pia kwamba kijiji cha Kalangali kibaki katika Wilaya ya Manyoni kwa kuwa kwa muda mrefu wananchi wake wamekuwa wakipata huduma zote katika Wilaya hiyo. Hivyo azimio la kikao hicho liliuwa ni kurekebisha mpaka wa Wilaya hizi ili kijiji cha Kalangali kibaki katika Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maafikiano hayo Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, itakwenda kufanya marekebisho ya mpaka katika eneo hilo ili kuondoa utata uliokuwepo.

Mheshimiwa Spika, pia kumbukumbu ambazo Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inazo inaonyesha kwamba Mheshimiwa Mbunge aliwahi kuwasilisha barua ya tarehe 26 Februari, 2013 ikionyesha kuwepo mgogoro unaohusisha kijiji cha Matagata. Hata hivyo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 205 la mwaka 2009 kijiji hicho kiko katika Wilaya ya Sikonge.

Mheshimiwa Spika, endapo upo mgogoro mwingine mpya Serikali itakuwa tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mamlaka zilizopo ili kuupatia ufumbuzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninaweza kusema tu kwamba ninasikitika sikuridhika na majibu yaliyotolewa hapa. Kwa sababu hata Serikali yenyewe inakiri hapa kwamba katika kutanzia mgogoro wa eneo hilo Tangazo la Serikali *GN*. Na.26 la mwaka 1961, ndilo litumike kueleza mipaka katika ya Wlaya ya Skonge na Manyoni. Iko dhahiri kabisa. Kwamba *GN* hiyo ndiyo itumike.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni sababu zipi zilizopelekea kukiukwa kwa tangazo hili, na likaja tangazo lingine jipya la 205 la mwaka 2009. Kwa sababu ninafahamu kijiji hiki ni sehemu, si kijiji ni kitongoji ambacho ni sehemu ya kijiji cha Makale. Kwa hiyo, ningelipenda kujua sababu hiyo ya kuja kwa *GN* hii badala ya ile iliyoagiza kwamba tutumie?

Mheshimiwa Spika, la pili, ningelipenda kujua ni kwa nini hayajaelezwa hapa bayana kuhusu kijiji cha Mwamatiga?

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge swali la pili, umesemaje?

MHE. JOHN P. LWANJI: Mwamatiga hiki nacho ni kitongoji.

SPIKA: Swali la pili hatujalisikia

MHE. JOHN P. LWANJI: Kwa sababu katika ile barua nilipeleka malalamiko ya vijiji viwili, kijiji cha Mwatagata pamoja na Mwamatiga. Lakini ninaona Serikali iko kimya, haikuweza kutoa majibu kuhusu kitongoji cha Mwamatiga ambacho ni sehemu ya kijiji cha Kaju, katika Wilaya ya Manyoni, sasa ndiyo maana hapa napo ninasema kwamba majibu hayatoshelezi kabisa, na inaongelea zaidi tatizo ambalo lilikwisha tatuliwa kuhusu kijiji cha Kalangali, lakini ameachwa kijiji cha Mwatagata pamoja kijiji cha Mwamatiga.

SPIKA: Swali ni refu mno. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa John P. Lwanji, kama hivi ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninajua jitihada ambazo Mheshimiwa John Paul Lwanji, amefanya katika masuala anayoyazungumza. Mimi mwenyewe, Mheshimiwa Waziri wa Nchi na Mawaziri waliopita katika Wizara hii ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tunatambua jitihada za Mbunge huyu katika suala hili analolizungumza.

Mheshimiwa Spika, mimi ninamwomba Mheshimiwa kwamba pamoja na kumpongeza kwa kazi nzuri anazo fanya nimpeshelele mimi katika muhtasari huu ambao nimeu-*quote* hapa. Muhtasari huu Mheshimiwa Waziri Mkuu, (Mheshimiwa Mizengo K. Pinda) alizunguza habari hii, na akaelekeza toka alipokuwa Naibu Waziri, akawa Waziri wa Nchi, na mwisho akawa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Haya matokeo haya, huu muhtasari ninaousema hapa Mheshimiwa Lwanji ame saina na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, wamesaina wote kwa pamoja katika jambo hili. *Issue* iliyokuwa inazungumzwa humu ndani ilikuwa ni kijiji cha Kalangali, ndicho kilichokuwa kinazungumzwa. Ndicho hicho wakaridhia.

Mheshimiwa Spika, wameonyesha kilikuwa kijiji hiki kinaonekana kwamba kiko Sikonge lakini wakaridhia kwamba kirudishwe moja kwa moja kiletwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Hicho ndicho tulichokisema hapa. Hakuna ubishi wowote katika jambo hili, sisi tunakubaliana naye.

Sasa kuna hili la pili analolizungumza, na mimi kwa kujua kwamba jambo hili litaleta matatizo hapa, na kwa sababu ninaheshimu Kauli ya Mbunge, limekuja hapa anauliza anasema kwamba ile *GN* ya mwaka 1961 sasa sisi tuna-*quote* kitu kilichopo hapa. Kitabu ni hiki hapa.

(Hapa Kitabu Husika kilionyeshwa Bungeni)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 796 ambayo ni *GN*, hii ambayo nime-*quote*. Hapa inaonyesha Kata ya Kipili, Matagata, inaonyesha kwamba iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. *Development* unayoiona hiyo ya mwaka wa *GN* hii, ni *Development* ambayo haikiniani na ile ambayo tumeizungumza, sasa inawezekana kabisa kwamba Mheshimiwa John P. Lwani anasema hivi, jambo hili mnalolisema hapa, bado linafannana na lile lingine, menyamazia, mmenyazima.

Mheshimiwa Spika, mimi ni nani hapa, nisema nje ya kitabu hiki, kinavyosema hapa. Kama kweli anafikiri kwamba kuna tofauti hapa au kuna tafsiri ambayo si sahihi, sisi tuko tayari kukaa na Mheshimiwa Mbunge, lakini *document* hii ndiyo tunayoi-*quote* hapa, ndiyo ambayo inayotumbia kwamba kijiji cha Matagata kiko katika Halmashauri ya Sikonge.

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo lingine jipya limezuka, na mazungumzo haya yote niliyoyasema hakukuwako na Matagata, hii ni *new development*. Iko barua ninakiri hapa, ambayo imeandikwa ya Matagata, sisi tutakwenda kukaa, tukaangalie hili Mheshimi John P. Lwanji analosema sasa hivi kwamba labda kuna tafsiri ambayo ni tofauti, na kwamba tumekosema humu ndani ili tufanye marekebisho hayo. Lakini *as of now*. Huo ndio msimamo.

SPIKA: Mkaongee maana sisi hatuelewi. Niwagonganishe na Mheshimiwa Mbunge wa Sikonge, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, sasa kama analeta mgonganisho basi tena.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, nijnakushukuru. Kwa kuwa ninaamini kabsia kwamba Tanzania ni moja na Watanzania ni wamoja bila kujali mipaka iliyopo. Na kwa kuwa ninaamini kwamba mgogoro anaoutaja Mheshimiwa John P. Lwanji na Mheshimiwa Naibu Waziri hapa uliisha isha na tukafanya makubaliano.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SAID J. NKUMBA]

Mheshimiwa Spika, ninaomba niulize swali moja. Je, utaratibu wa kuzua migogoro mipya bada ya kutatua migogoro wa zamani, unaruhiwa Serikalini? (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Nilijua tu unaleta migongano hapa. Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba ujibu kwa kifupi lakini mkakae muelewane. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Said J. Nkumba, kama hivi ifutavyo.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba pia umemruhusu Mheshimiwa Saidi J. Nkumba, azungumze hapa kwa sababu wote hawa ni wadau muhimu. Hakuna utaratibu unaoruhusu watu kuzua migogoro ukalileta. Lakini tuwasikilize wote hawa. Mheshimiwa Said J. Nkumba tunamsikiliza, Mheshimiwa John P. Lwanji tunawasikiliza na Wabunge wote tunawasikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa tunajibu kwa niaba ya Serikali, tuangalie. Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi yuko hapa. Mimi nikipewa maelekezo hapa nenda kakae tena upya. Kaangalie upya habari ya Matagata, wanasema nini? Mimi ni nani hapa nibishane na Mbunge hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachosema hapa. Mtumishi wa Bwana niko tayari kwenda kufanya kazi niliyoagizwa, mimi sina ubavu wa kukataa jambo lolote. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ataniagiza niende na maagizo ya Waziri Mkuu, nitakwenda kufanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka kuweka *records* vizuri hapa, tusije tukawachanganya watu hapa wakarikiri kuna mtu anadhulumiwa hapa. Basi hilo tu. (*Kicheko/Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nimeona tu nisimame. Kwa sababu jambo hili ni la muda mrefu sana. Mimi toka nikiwa Naibu Waziri ndiye niliyehangaika nalo kwanza. Lakini mimi ninataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote wawili hawa. Wajue tu kwamba kikubwa pale ni maslahi ya watu kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikubali kama Serikali, kijiji cha Kalangali, tukipeleke Manyoni, Sababu yake ilikuwa ni kwamba huduma nyingi wanazipata upande wa Manyoni. Lakini *technically* kiko Sikonge. *Technically* kiko Sikonge. Lakini baada ya kukaa na pande zote mbili ndiyo tukaona sasa kwa mazingira haya sisi tunafikiri kwamba mngelikubaliana hivi kwa maslahi ya watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lilipomalizika lile likaja la Matagata. Mheshimiwa anaamini Matagata iko upande wa Manyoni. Walipo pale wanaamini wako upande wa Sikonge.

Kwa hiyo katika jitihada hizi ambazo alikuwa anaeleza Naibu Waziri, ikaoneka jamani kwa nini tusiache basi iendele kuwa Sikonge. Na nilifikiri hili jambo lingeliisha vizuri tu kwa sababu upande mmoja amekubali ku-*surrender* Kalangali iende Manyoni, kwa hiyo Matagata ile ikienda, na ni kitongoji tu kwa sehemu kubwa.

Lakini kama wanaona bado ni tatizo kubwa njia rahisi ni hii anayoisema Naibu Waziri, tumwombe TAMISEMI, kaa nao tena wote wawili, ikibidi nende mkazunguze na wavijiji kwenye pande zile zote mbili, ili jambo hili liishe. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsante, tuendelee na swali linalofuata.

Na. 84

Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Serikali imefanya jitihada kubwa ya kujenga barabara ya Mabasi yaendayo kasi katika Jiji la Dar es Salaam.

Je, ni lini mradi huo utakamilika na hatimaye mabasi hayo yaanze kazi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam unatekelezwa katika awamu sita. Ujenzi wa miundombinu ya mfumo Awamu ya kwanza iliyoanza kutekelezwa mwaka 2007/2008 umepangwa kukamilika na kuanza kutoa huduma hiyo kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ratiba ya ujenzi wa barabara inabainisha kuwa ifikapo Agosti, 2014, ujenzi wa barabara ya Morogoro kuanzia Kimara mpaka Kivukoni utakuwa umekamilika. Miundombinu ambayo imekuwa inajengwa ni barabara ya kilometa 20.9 kuanzia Kimara mwisho hadi Kivukoni ikijumuisha shehemu ya barabara ya Kawawa toka Morocco hadi Magomeni na barabara ya Msimbazi hadi eneo la Gerezani - Kariakoo, vituo 27 vituo vikuu 5 vituo milisho 4 na Karakana 2 kwa maana (*Depot*).

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Awamu ya kwanza ya Mradi inaghamiwa na fedha kutoka Benki ya Dunia kwa Dola za Kimarekani 325.37 na Serikali ya Tanzania metumia Shilingi bilioni 23.5 kwa ajili ya kugharamia ulipaji fidia ya mali zilizoathiriwa na miundombinu ya mradi na Sekta binafsi zinazotarajiwa kuchangia katika dola za kimarekani million 100 kwa ajili ya kuwekeza kwenye ununuzi wa mabasi na kuanzisha mfumo wa kisasa wa ukusanyaji nauli na utunzaji wa fedha zinazotokana na mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, Miundombinu ya barabara inajumuisha njia ya waenda kwa Miguu na baiskeli. Hivyo basi ujenzi unaoendelea ni pamoja na kukamilishwa mwezi Julai mwaka 2015 ni pamoja na barabara hiyo ya Kawawa kuanzia Magomeni mpaka Marocco na mtaa wa Msimbazi kutoka *Fire* mpaka Kariakoo - Gerezani (Maeneo ya Gerezani Kota) eneo ambapo zilikuwepo nyumba za Mamlaka ya Bandari na Shirika la Reli Tanzania.

Aidha kituo cha Gerezani Kariakoo kitaunganishwa na barabara ya Nyerere hadi Gongo la Mboto na Barabara ya Kilwa hadi Mbagala Rangi Tatu pindi zitakapokuwa zimejengwa na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuwapata watoa huduma katika sekta binafsi watakaohusika na shughuli za ununuzi na uendeshaji wa Mabasi, ukusanyaji wa nauli na Utunzaji wa fedha (Benki) kabla ya mradi kuanza mwaka 2015 yameanza na yanakwenda vizuri.

Hivyo, maandalizi yanayofanyika yanalenga kuwezesha mfumo kuanza kutoa huduma ya awali ya mabasi makubwa kuanzia Kimara Mwisho hadi Kivukoni ikiwa ni sehemu ya mafunzo na maandalizi ya mfumo kuanza kutoa huduma kamili pindi miundombinu ikikamilika mwezi Julai, 2015.

MHE. MARIAM KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ninaipongeza sana Serikali kwa kuwezesha mradi wa mabasi yaendayo kasi angalau kwa sasa yameanza kuonyesha sura katika Jiji la Dar es Salaam. Lakini nina swali la nyongeza moja.

Kwa kuwa, ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo kasi kuna baadhi ya maeneo katika Jiji la Dar es Salaam umekamilika kwa asilimia kubwa sana.

Je, Serikali haioni haja ya kufungua baadhi ya barabara ili kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji la Dar es Salaam?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kisangi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, mradi huu ni mkubwa na ni wa aina yake katika Afrika Mashariki na Kati, unagharimu zaidi ya bilioni 290 mpaka wote utakapokamilika na sasa upo kwenye hatua nzuri.

Katika maeneo ambayo yameanza kuonyesha kukamilika kwa taratibu za kihandisi bado hayajakamilika kwa sababu yale maeneo yakishakamilika yanatakiwa yachorwe, zile alama zote za kuchorwa kuonyesha mahali pa wapita kwa miguu, mahali pa *packing* na kuweka vituo vya alama za barabarani bado hazijakamilika. Kwa hiyo, tukianza ku-*involve* watu waanze kuvitumia tutakuwa tumempa faida Mkandarasi kuacha kumalizia zile hatua nyingine zilizotakiwa kukamilika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Kisangi pamoja na watumiaji wa barabara wa Jiji la Dar es Salaam kwenye mradi mashuhuri wa *BRT* tuwe na subira kidogo, mradi ulikuwa wa miezi 36 sasa imebaki kama miezi mitatu tu. Lakini nakubaliana na yeye pia kwamba katika maeneo ambayo yatakuwa yamekamilika katika hatua zote tutaanza kuyafungua ili yaweze kutumika kwa ajili ya watu lakini kwa sasa hivi bado maeneo hayo hayajakamilika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mradi huu ni muhimu sana na utapunguza foleni kwa kiwango kikubwa sana na ninashukuru sana mradi huu umechukua sehemu kubwa sana ya Jangwani katika Jimbo langu.

Je, Serikali iko tayari kushirikiana na Mbunge wa Ilala kuhakikisha na kudhibiti maji ya mvua hayataweza kuingia na kuharibu mradi mkubwa kama huu?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zungu, kama ifuatavyo:-

Tutashirikiana na Mbunge katika kudhibiti hayo maji!
(*Makofi*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ni changamoto hasi ambapo kwa siku moja tunapata hasara zaidi ya bilioni tano ambapo kwa mwaka ni zaidi ya trilioni mbili kwa sasa na Jiji la Dar es Salaam lipo *centrally locate* yaani tunaweza tukatumia safiri zote kwa pamoja yaani usafiri wa maji, reli, barabara na anga na kwenye misafara wakatamia anga ya helikopta kama wanavyofanya ndugu zetu wa Nairobi.

Je, Serikali fikra yakinifu ya sasa ya kuokoa umaskini huu ambao unasababishwa na msongamano janga katika Jiji la Dar es Salaam ikatumia miundombinu yote minne ili kuondokana na janga hili ambalo ni *very negative* hasa kwenye *efficiency* na *reliability* katika Jiji la Dar es Salaam?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbatia, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ni changamoto kubwa kama ilivyo misongamano katika Miji mingine pia duniani kwa sababu suala la msongamano ni suala mtambuka.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA UJENZI]

Lakini napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Watanzania kwamba mchangamano huu na changamoto hizi ambazo zimekuwa zikitokea katika Majiji yetu likiwepo Jiji la Dar es Salaam na miji mingine inayokua limeanza kutafutiwa ufumbuji katika awamu hii na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na ndiyo maana mtaona katika Jiji la Dar es Salaam kwa mfano, suala la barabara zimeanza kujengwa barabara nyingi ikiwa ni pamoja na barabara ya Mwenge kwenda Tegeta ambayo imepanuliwa, hii pia ni katika kupunguza msongamano.

Barabara ya kutoka Mwenge kwenda Morocco nayo itapanuliwa. Barabara ya kutoka Hoteli tatu kwenda Gerezani nayo itapanuliwa. Daraja la *Fly over la TAZARA* litaanza kujengwa mwaka unaokuja na zaidi ya shilingi bilioni 100 zimetengwa kutoka Serikali ya Japan ikiwa ni pamoja na daraja la Kigamboni linalojengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 214. (*Makofi*)

Lakini pia tutaanzisha usafiri wa majini kwa sasa hivi kuna Feri ambayo inatengenezwa Denmark ambayo itakuwa na vituo saba, kutoka Dar es Salaam mpaka Bagamoyo ambapo kwa wale watakaokuwa wanapenda kutumia njia ya maji nao waweze kutumia njia ya maji.

Lakini pia kuna treni ambayo nayo imeanzishwa na Serikali kwa ajili ya kupunguza msongamano.

Kwa hiyo, juhudi hizi zote kwa pamoja zinachukuliwa na Serikali katika kupunguza msongamano lakini juhudi kubwa nyingine inayotakiwa kuchukuliwa ni wananchi wenyewe *mind set* yao katika kuzingatia sheria kwa sababu hata zinapotengenezwa barabara zinatengenezwa *by pass*, hizo hizo barabara ndiyo zinakuwa magereji, hizohizo barabara ndiyo yanakuwa maduka, hizohizo barabara ndiyo panakuwa mahali pengine pa ku-*block* watu wengine wanaopita kwenye barabara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA UJENZI]

Kwa hiyo, hili ni suala mtambuka na ni suala linalotakiwa kuchukuliwa na Watanzania wote. Lakini pia suala la helikopta, ukienda sasa hivi *Sea Cliff* kuna helikopta zaidi ya tatu kila siku zipo ambazo ni za watu *private* wanaozitumika kwa ajili ya kukidisha kwa wale ambao hawataki kwenda msongamano wanapokwenda *airport*.

Kwa hiyo, hili suala ni la Watanzania wote tushikiane pamoja sekta binafsi tubadilishe *mind set* zetu lakini na Serikali nayo ikiwa inachukua hizi juhudi kubwa katika kupunguza msongamano. (*Makofi*)

Lakini hizi juhudi zinazochukuliwa pia zimeanza kuchukuliwa katika Mji wa Dodoma, Jiji la Mwanza, Jiji la Arusha na maeneo mengine. Kwa hiyo, hilo ndilo ninaloweza nikajibu katika swali hili kwa ujumla. (*Makofi*)

SPIKA: Haya, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Mheshimiwa Jenista Mhagama, atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Vita R. Kawawa.

Na. 85

Kuwasaidia Vijana Katika Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA) aliuliza:-

Kwa kuwa, wnanchi wamekuwa wakihamasika sana kuhusu miradi ya Uhifadhi wa Mazingira na ukomo wa bajeti katika Halmashauri zetu unafanya miradi hiyo bunifu ya vijana kukosa uwezeshaji na kwa sababu katika Bajeti tunapitisha fedha za uhifadhi katika Mafungu ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Je, Ofisi ya Makamu wa Rais iko tayari kuwasaidia vijana hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa sasa haina fedha za moja kwa moja kwa ajili ya kuwasaidia vijana katika miradi ya kuhifadhi mazingira, ila inaratibu maoni ya miradi ya kukhifadhi mazingira yanayodhaminiwa na Mfuko wa Mazingira Duniani, (*Global Environment Facility – GEF*) kupitia mpango wa ufadhili chini ya miradi midogo (*Small Grants Programme (SGP)*).

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNDP* kupitia mfuko wa *GEF* katika mpango wa *SGP* wamekuwa wakifadhili miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira kwa kufuata vigezo na miongozo iliyowekwa na *UNDP/GEF*. Aidha, maeneo lengwa ya *GEF* ambayo hupatiwa ufadhili ni:-

- Hifadhi ya Bioanuai;
- Mabadiliko ya tabianchi;
- Hifadhi ya ardhi;
- Maji ya kimataifa;
- Usimamizi endelevu wa misitu; na
- Usimamizi wa Kemikali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais iko tayari kuwasaidia vijana hao waweze kupata ufadhili katika shughuli za kuhifadhi mazingira. Ofisi itawaelekeza jinsi ya kuandaa andiko la mradi (*Project Proposal*) kulingana na miongozo iliyowekwa na *UNDP/GEF Small Grant Programme*, kwa kuzingatia maeneo lengwa *GEF* kama nilivyoeleza hapo awali. Aidha, bajeti ya mradi husika isizidi kiasi cha Dola za Marekani 50,000. Mwongozo wa *GEF* unapatikana katika tovuti ya (www.thegef.org).

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA]

Katika kipindi cha 2012/2013, miradi midogo 33 yenye thamani ya Dola za Marekani takribani milioni 1.3 ilipata ufadhili. Baadhi ya miradi hiyo ilitekelezwa Tanzania Visiwani na Bara katika Wilaya za Kilosa, Morogoro Vijijini, Moshi Vijijini, Same, Korogwe, Mbinga, Bagamoyo na Ilala.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, vijana wa Jimbo la Songea Vijijini na Vijana wa Namumbo wamekuwa wakihamasika sana na miradi hii ya uhifadhi wa Bionuai, kusimamia kukatwa kwa miti hovyoy ili kulinda uoto wa asili unaoleta mvua nyingi katika Mkoa wetu wa Ruvuma, lakini pia usimamizi endelevu wa misitu kwa kupanda miti katika vyanzo vya maji. Na kwa kuwa, vijana hawa

SPIKA: Uliza swali!

MHE. VITA R. KAWAWA: *Yes Sir! Ndiyo Madam! Ndiyo! (Kicheko)*

Je, kwa kuwa, vijana hawa ni wa vijijini na hawana utaalumu wa kuandika maandiko haya na hawana *access* ya *internet* ya kufuata mwongozo huu kwenye *internet*.

Je, Serikali inaweza kuwaletea wataalamu sasa hawa kuwasaidia kuandika andiko hili ili waweze kupata mradi huu kutoka *UNDP*?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, Ofisi ya Makamu wa Rais iko tayari na nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge, kama atakuwa tayari aje ofisini tutampatia wataalamu watawasaidia vijana ili waweze kuandika maandiko. *(Makofi)*

Na. 86

Uhitaji wa VETA – Meatu

MHE. MESHACK J. OPULUKWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi (VETA) Wilayani Meatu?

WAZIRI WA ELIMU NA MFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opolukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya zisizo na Vyuo vya Ufundi Stadi vya aina yoyote. Mpango huu utatekelezwa katika Wilaya 43 zisizokuwa na vyuo vya aina hii ambazo utambuzi wa stadi zinazohitajika umefanyika. Wilaya ya Meatu ipo katika awamu ya kwanza ambapo mpaka sasa eneo lenye ekari 50 limetengwa katika Kijiji cha Mwambiti kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho. Aidha, uongozi wa Wilaya unatakiwa ukamilishe utaratibu wa kupata Hatimiliki ili hatua za ujenzi zifuate.

Mheshimiwa Spika, wakati taratibu hizo zikiendelea, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Meatu kutumia Vyuo vya Ufundi Stadi vya Shinyanga, Tabora na Mwanza pamoja na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyo karibu na Wilaya ya Meatu kama vile vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Kisangwa (Wilaya ya Bunda), Mwanva (Wilaya ya Kahama), Malampaka (Wilaya ya Maswa), Nzega (Wilaya ya Nzega), Sengerema (Wilaya ya Sengerema) vinavyotoa mafunzo ya Ufundi Stadi sanjari na Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii chini ya usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, ukamilishaji wa kupata hili eneo la ekari 50 uko katika hatua za mwisho kabisa na kufikia mwaka kesho mwezi wa tatu kwa utaratibu tunaokwenda nao kwenye Halmashauri yetu tutakuwa tumeshapata hii Hatimiliki kwa ajili ya kujenga chuo hiki.

Je, Serikali iko tayari sasa kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa chuo hiki kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimwa Opulukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumejipanga kwa kadiri pesa zitakavyoweza kupatikana kujenga kwa haraka vyuo vya ufundi stadi hivi ambavyo tumevitaja katika Wilaya 13 mwaka huu wa fedha tumejipanga kujenga vyuo vitano katika Wilaya ya Ukerewe, Namtumbo, Kilindi, Ludewa na Chunya. Katika mwaka ujao wa fedha tutajitahidi kutenga fedha kwa wilaya nyingine ambazo zimeorodheshwa kama nilivyozitaja. *(Makofi)*

Tutaipa kipaumbele Wilaya ya Meatu kwa sababu Wilaya zingine hazijapata ardhi lakini Meatu wameshafanya juhudi hizi, hivyo tutajitahidi kuona namna ambavyo tutailingiza kwenye awamu hiyo inayofuata kwa mwaka unaofuata wa fedha. *(Makofi)*

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, kwa sababu taratibu hizi zimekuwa zikienda polepole sana na kama alivyofikia hapa Mheshimiwa Waziri anazungumzia leo kuhusu ujenzi wa Chuo cha *VETA* Meatu ni karibia miaka mitano toka suala hili tukijaribu kuli-*push*.

Sasa wakati hizi taratibu zinakwenda polepole sana Waziri anaweza kukubaliana na mimi kwamba sasa tunaweza kabisa kuanzisha vyuo hivi hata kwa kutumia nyumba za watu kwanza ili vijana hawa ambao hatuna mahali pa kuwapeleka sasa na wanahitaji mafunzo ya ufundi na wakaendelea na mafunzo hayo Wizara ikatoa Walimu sasa hivi wakaanza kutoa mafunzo hayo?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpina, kama ifuatavyo:-

Serikali itashukuru sana kama Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla watafanya juhudi ya kushirikisha nguvu za wananchi kwa ajili ya kujenga vyuo vya ufundi stadi kama vile ambavyo walifanya katika kujenga shule za sekondari za wananchi na Serikali itafanya kila juhudi kuwa-*support* na kuandaa Walimu kwa ajili ya vyuo hivyo.

Juhudi kubwa ambayo imefanywa na Serikali mpaka hivi sasa tumekopa pesa kutoka Benki ya Dunia, si fedha nyingi ni jumla ya dola milioni 52 ambazo hazitaweza kufanya kazi kama vile ambavyo tungependu lakini Serikali pia imejipanga kutenga fedha zaidi.

Kwa hiyo, juhudi za wananchi kupitia hamasa za Wabunge zitapokelewa vizuri na Serikali na tutawasaidia kwa kila namna inavyowezekana.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mary Chatanda!

Na. 87

Mahitaji Maalum kwa Wanafunzi Walemavu Katika Sekondari ya Wasichana Korogwe

MHE. MARY P. CHATANDA aliuliza:-

Shule ya Sekondari ya Wasichana Korogwe ina sehemu ya walimu maalum kwa wasioona na walemavu wa ngozi.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapatia wanafunzi hao wenye ulemavu mahitaji maalum na vifaa vya kujifunzia?

(b) Kuwepo kwa upungufu na kutokuwepo kabisa baadhi ya zana muhimu za kujifunzia, Serikali haioni kuwa inachangia kwa kaisi kikubvwa kuzorotesha mafanikio ya wanafunzi hao kielimu?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wa kutenga za kununua na kusambaza vifaa vya kujifunzia na visaidizi kwa ajili ya wnaafunzi wenye ulemavu wakiwemo wasioona na wenye ulemavu wa ngozi katika Vyuo vya Ualimu, Shule za Sekondari na Msingi kwa nchi nzima. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, fedha zilizotumika kununua vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ni shilingi milioni 394,250,000/=.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013 vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 1,000,480,000/= vilinunuliwa na kusambazwa katika shule mbalimbali ikiwemo Shule ya Sekondari ya Wasichana Korogwe.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Vifaa vilivyopelekwa katika Shule ya Sekondari Korogwe ni pamoja na karatasi za maandishi ya nukta nundu rimu 400 (*Braille paper 400 reams*), karatasi za braillon rimu 6 (*brailon paper 6 reams*) na mashine za Nukta Nundu.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara yuangu bado kuna upungufu wa vifaa vya kujifunzia na visaidizi katika shule mbalimbali ikiwemo shule ya Skondari ya Wasichana Korogwe. Hali hii inatokana na ufinyu wa Bajeti ambao husababisha kutokidhi mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafsi hii kuwashukuru wadau mbalimbali wanaosaidia kwa namna mbalimbali, uendeshaji na ugharamiaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule za Msingi na Sekondari nchini. Baadhi ya wadau hao ni pamoja na *UNESCO, UNICEF, Under The Same Sun (UTSS), Tanzania League for the Blind (TLB), Mamlaka ya Elimu tanzania (TEA), Rotary Club na Lions Club.*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wadau wote wa elimu kushiriki kikamilifu katika uchangiaji wa ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na visaidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wakiwemo wasioona na wenye ulemavu wa ngozi ili kurahisha ujifunzaji wao.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chatanda swali la nyongeza.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wanafunzi hawa ambao ni walemavu wanaonekana ni wachache katika Nchi nzima ni tofauti na wanafunzi wa kawaida. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi ili kusudi kumaliza matatizo yanayokabili kupata vifaa vinavyowahitaji kupata hawa walemavu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chatanda kama ifuatavyo.

Kwanza nimpongeze sana kwa kujali maslahi na elimu ya vijana wetu hawa walemavu katika shule hizi. Nikiri kwamba idadi yao sio kubwa ukilinganisha na idadi ya wanafunzi tuliokuwa nao katika shule zetu za msingi na Sekondari.

Katika miaka mitatu (3) mpaka mwaka 2012/2013 tumetenga zaidi ya shilingi billion 3 kwa ajili ya ununuaji wa vifaa kwa ajili ya wanafunzi hawa wenye ulemavu.

Lakini tumeweka azma ya kuhakikisha kwamba katika kila Bajeti ya kila mwaka tunaongeza fedha ambazo tunazitenga kwa ajili ya matumizi haya. Hizi ni fedha pamoja na vifaa mbalimbali na pia mazingira yale ambayo yanamwezesha kijana mwenye ulemavu kuweza kupata elimu kwa njia ya urahisi zaidi.

Pia kuweka miongozo ambayo ina wawezesha wazazi pamoja na walimu kuweza kumhudumia mwanafunzi huyu mwenye ulemavu vizuri zaidi kushinda hapo nyuma ambapo vitu vilikuwa vinaenda kama mazowea tu, bila kuwepo na miongozo mizuri, elimu nzuri kwa Waalimu, pamoja na Wazazi wenye watoto hawa. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, atauliza swali hilo.

Na. 88

Ziara ya Viongozi Wakuu wa Nchi

MHE. YAHAYA K. ISSA aliuliza:-

Wakuu wa Nchi wanapofanya ziara zao Nchi mbalimbali huenda kwa malengo ya kunufaisha Nchi zao au kule wanakokwenda na kwa kipindi hiki Tanzania imepokea ugeni wa Kiongozi Mkuu kutoka Marekani.

Je, Serikali inaweza kutueleza dhamira kuu ya Kiongozi huyo kuja Tanzania na faida ya ujio wake kwa Watanzania?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia mwaliko wa Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Barack Obama, Rais wa Marekani alifanya ziara nchini tarehe 1 Julai, 2013 mpaka tarehe 2 Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, Ziara hiyo fupi na ya kihistoria ni ya kwanza kwa Rais Obama kuitembelea Tanzania ikiwa Kiongozi wa Taifa hilo kubwa Duniani. Tanzania ilikuwa moja kati ya Nchi tatu ambazo Rais Obama alizitembelea Barani Afrika. Hii inatokana na juhudi za nchi yetu katika kuimarisha Utawala Bora unaozingatia misingi ya Kidemokrasia, Utawala wa Sheria na kudumisha hali ya amani na utulivu ambayo imeipa Tanzania heshima kubwa Duniani kote.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE]

Mheshimiwa Spika, dhamira kuu ya Rais Obama kuja Tanzania ni kuimarisha zaidi uhusiano na Ushirikiano mzuri uliopo kati ya Nchi hizi mbili. Alipokuwa nchini lieleza kuridhika na hatua tunazochukua za kukuza demokrasia Nchini, Utawala Bora na kuwekeza katika maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, Rais Obama pia alikuja kuzindua Mpango wa Serikali yake wa kusaidia maendeleo ya sekta ya Umeme katika Bara la Afrika (*Power Africa Initiative*). Mpango huo umetegewa kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 7 na Serikali ya Marekani na Makampuni binafsi ya Nchi hiyo yameahidi kuwekeza dola bilioni 9 katika mpango huo.

Kwa kuanzia Nchi sita za Afrika (Ethiopia, Ghana, Nigeria, Liberia, Kenya na Tanzania) zitahusishwa. Bila ya shaka mpango huo ukikamilika utasaidia sana kuimarisha upatikanaji wa umeme Barani Afrika, ambayo ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Yahya Issa, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA K. ISSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa muda huu wa miezi sita katika ahadi alizoahidi za maendeleo ya kiufundi kama Elimu, Afya, Kilimo, Barabara na kadhalika, ni lipi katika haya aliweza kwisha kutekeleza.

Je, kwa muda gani aliahidi atakamilisha ahadi zake zote pamoja na suala la umeme katika sekta ya umeme.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, niongelee *Power Africa*, maana ya *Power Africa* ni kwamba hawaleti fedha za mradi zinakufuata, ni wewe mwenyewe utengeneze miradi ambayo inaweza ikavutia pesa. Kwa hiyo Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, kuna namna mbili ya kutengeneza miradi Duniani. Fedha ziko pale mradi upo au mradi unatafuta fedha. Kwa hiyo sisi *Power Africa* Wizara ya Nishati na Madini ni kwamba katika zile billion 7 na billion 9, billion 9 zitakua ni sehemu za fedha za Makampuni ya Kimarekani na hapa kwetu utekelezaji mmoja wapo ni ule wa kujenga *megawatt 600* kule Mtwara halafu tunajenga *transmission line* ya kutoka Mtwara mpaka Songea ni karibu kilomita 650. Kwa hiyo, hiyo ni sehemu ya *Power Africa Initiative*.

Mheshimiwa Spika, ya pili ni hii ambayo sasa hivi wanasaidia *MCC Phase Two* ambayo kama mnafahamu ya kwanza ilipita Tanzania ilifanya vizuri ikaingia kwanye *MCC Phase Two* na sisi Tanzania tumepiga hatua tumeshapeleka miradi yetu mpaka kwenye Serikali ya Marekani.

Kwa hiyo, kwa upande wetu sisi Tanzania tunaenda vizuri na kama tulivyoongea na Wamarekani tunataka katika zile Nchi 6 Tanzania ndiyo iwe Nchi ambayo itapata fedha nyingi na tumefanya kwa vitendo kwa sababu miradi yetu tayari imeshafika ndani ya Serikali ya Marekani. (*Makofi*)

SPIKA: Hilo swali la kwanza limejibiwa na swali la pili lile! Mheshimiwa Zitto.

MHE. ZITTO Z. KABWE: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na kuratibu Ziara za Viongozi wa Nchi za Kigeni kuja nchini, lakini pili inaratibu ziara za Viongozi wetu kwenda Nchi za Nje. Hivi karibuni Tanzania ilikuwa na msafara wa Viongozi waliokwenda kwenye mazishi ya Mzee Nelson Mandela na tunafahamu historia ya Nchi yetu kwa Ukombozi wa Afrika ya Kusini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ZITTO Z. KABWE]

Lakini pili Tanzania ina mtu ambaye ndiye mmoja wa Waafrika wawili waliomwona Nelson Mandela akiwa jela ambaye ni Mzee John Samwel Malecela.

Aidha tuna Viongozi wastaafu Mzee Ali Hassn Mwinyi na Mzee Benjamin Mkapa. Ni sababu zipi zilipelekea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano Wa Kimataifa kuruhusu msafara wa Rais bila Viongozi hawa kwenda kutoa heshima kwa Mzee Nelson Mandela?

SPIKA: Swali lenyewe jingine kabisa, Mheshimiwa Naibu Waziri jibu tu kama unafahamu lakini ni jipya kabisa wala halifanani hata kidogo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli Wizara ya Mambo ya Nje inaratibu safari za Viongozi. Lakini ukweli pia kwamba safari za Viongozi ni viongozi wenyewe kwa kuzingatia mambo mbalimbali ndiyo wanaoamua baadhi ya Viongozi wengine ambao wataambatana nao katika misafara hiyo.

Kwa hiyo, kwa awamu hii ya kwanza kwa kuwa Mheshimiwa Rais atarudi tena Afrika Kusini kwa maziko yaliyopangwa kufanyika tarehe 15, lakini katika awamu hii ya kwanza busara zilizotumika ni kuambatana na Viongozi ambao alioambatana nao ikiwemo Katibu Mkuu wa CCM, kutokana na uhusiano uliopo wa CCM na ANC na Makamu wa pili wa Rais Zanzibar.

Kwa hiyo, katika awamu ya pili, Mheshimiwa Rais mwenyewe atatumia busara, kuona ni Viongozi wepi sasa aambatane nao katika Ziara hiyo, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Esther Lukago Minza Midimu, atauliza swali hilo.

Na. 89

Kuweka Uwanja wa Ndege Mkoa wa Simiyu

MHE. ESTHER L. M. MIDIMU aliuliza:-

Mkoa mpya wa Simiyu hauna kiwanja cha Ndege na uwanja mdogo uliopo katika Makao Makuu ya Wilaya ya Bariadi umesongwa na makazi ya watu na hivyo kutofaa kwa shughuli hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga uwanja wa Ndege Mkoa wa Simiyu?

(b) Je, Uwanja huo utajengwa katika eneo lipi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Minza Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na kiwanja cha ndege katika Mkoa huu mpya wa Simiyu, Serikali imeweka ujenzi wa kiwanja hiki kuwa miongoni mwa viwanja kumi na moja vinavyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Usanifu utakaofanyika utahusisha miundombinu yote ya kiwanja pamoja na kuandaa makabrasha ya Zabunni yatakayotumika katika kutafuta Mkandarasi mara fedha za ujenzi zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri unaendelea ambapo tarehe 5 Novemba, 2013 makabrasha ya Zabuni (*request for proposals*) yalikabidhiwa kwa Makampuni sita (6) ambayo yalipendekezwa (*shortlisted*) kwa kufuata taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI]

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza mchakato wa kutafuta eneo ambalo kiwanja hiki kipya kitajengwa. Baada ya wataalamu wetu kwenda na kutembelea maeneo mbalimbali kwa kushirikiana na Sekretariat ya Mkoa, ilionekana kuwa yapo maeneo mawili yanayofaa kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege yaliyoko katika Tarafa ya Dutwa. Mara Mhandisi Mshauri atakapopatikana ataonyeshwa maeneo yote mawili na atafanya tathmini itakayoivezesha Serikali kuchagua mojawapo kati ya maeneo haya.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Esther swali la nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba nimwulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Simiyu una wakazi wengi, Wafanyabiashara, Wakulima na Wafugaji, ambao wanahitaji usafiri wa haraka namuomba Waziri awahakikishie Wananchi wa Simiyu ni lini ujenzi wa uwanja huo utaanza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Uchukuzi, hata kiwanja hawajachagua.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi tumesema kwamba taratibu za ujenzi zimekwisha anza na kikwazo sasa hivi ni bado hatujapata Mhandisi mshauri atakayeishauri Serikali kuhusu eneo gani kati ya yale mawili yaliyopendekezwa uwanja ujengwe na baada ya taratibu hizo usanifu utakamilishwa na utafutaji wa pesa kwa ajili ya ujenzi utaanza. Kwa hivyo kwa sasa siwezi kusema tarehe kamili ya kuanza ujenzi huo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Vincent Nyerere, swali linalofuata.

Na. 90

Kujenga Kituo cha Polisi Kinesi-Rorya

MHE. VINCENT J. NYERERE aliuliza:-

Hali ya Kituo cha Polisi katika Mji wa Kinesi-Rorya ni duni sana kiasi cha kukosa hadhi ya kuhifadhi silaha.

Je, ni lini Kituo cha Polisi chenye hadhi kitajengwa katika Mji huo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa hali ya Kituo cha Polisi Kinesi-Rorya siyo madhubuti kwa matumizi ya baadhi ya shughuli za Polisi kama vile kuhifadhi silaha.

Kwa kutambua changamoto hiyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wananchi pamoja na Mbunge wa Jimbo la Rorya, Mheshimiwa Lameck Hairo, limejenga kituo kipya kitakachokuwa na ghala imara ya kuhifadhia silaha zinazohitajika. Kwa sasa ujenzi huo upo katika hatua za mwisho za kuweka milango na madirisha ili kianze kutumika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Spika, Naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mbunge wa Jimbo la Rorya kwa kuwa karibu na Wananchi wake na kuchangia juhudi za maendeleo yao. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wengine kuiga mfano huo kwa kutekeleza kwa vitendo dhana ya Polisi Jamii inayohimiza ushirikishwaji wa Umma katika shughuli za Ulinzi na Usalama kama chachu ya kuongeza usalama katika maeneo yao.

SPIKA: Mheshimiwa Vincent Nyerere, swali la nyongeza.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nasikitika tu kwamba majibu aliyonipa na majibu aliyosoma ni tofauti.

Pamoja na majibu ya Kisiasa anayojibu Waziri nilipenda kuuliza. Askari hao wa Rorya pamoja na Askari wengine wa Polisi waliahidiwa kupandishiwa *retion allowance* kutoka shilling 150,000/= mpaka shilling 225,000/= mwaka huu wa fedha, lakini mpaka sasa fedha hizo hawajazipata. Nini kauli ya Serikali?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waziri kivuli wa Wizara hii kama ifuatavyo:-

Wizara kupitia Serikali ilikuwa na mapendekezo kwenye Bajeti kwamba tuongeze fedha ya posho ya Askari kutoka shillingi 150,000/= hadi shillingi 225,000/= kama ilivyo kwenye Majeshi ya wapiganaji. Hata hivyo maombi yetu hayakuweza kufanikiwa na tuliomba ziada kutoka kwenye Kamati ya Bajeti ya Bunge ambayo pia nilisema kwa wakati huu haikuwezekana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Kwa hiyo, niwaombe tu waendelee kustahimili kwa sababu nia njema ipo kuna siku wataongezewa.

SPIKA: Tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata. Kwa niaba yake Mheshimiwa Zainab R. M. Kawawa.

Na. 91

Ongezeko la Wafungwa Gereza la Geita

MHE. ZAINAB R. M. KAWAWA (K.n.y. MHE. VICKY P. KAMATA aliuliza:-

Gereza la Geita lilijengwa mwaka 1947 kwa madhumuni ya kuchukua wafungwa 147 ila hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2010 gereza hilo lilikuwa na wafungwa 294 ambao wanaishi katika mazingira magumu kutokana na ufinyu wa nafasi jambo, linaloweza kuleta mlipuko wa magonjwa na kero nyinginezo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua gereza hilo ili kukidhi ongezeko la wafungwa?

(b) Je, kwa nini Serikali isitumie vifungo vya nje na upatanishi katika kupunguza mlundikano wa wafungwa na mahabusu?

SPIKA: Hongera sana kwa kupata *Baby. (Makofi)*

MHE. ZAINAB R. M. KAWAWA: Mheshimiwa Spika Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo ya ufinyu wa nafasi iliyopo katika magereza yote kote nchini likiwemo Gereza la Geita. Upanuzi wa sehemu ya Wanawake (*Female Wing*) umefanyika na upanuzi wa sehemu ya Wanaume unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Aidha, Gereza la Geita ni miongoni mwa magereza yaliyofanyiwa ukarabati wa mfumo wa Maji taka ambao kwa kiasi kikubwa umepunguza uwezekano wa kuzuka kwa magonjwa ya mlipuko.

(b) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza linao utaratibu wa kuwaachilia wafungwa wanaotumikia kifungo Gerezani kisichozidi miezi kumi na miwili na ambao wametimiza vigezo vya kwenda kifungo cha nje kama inavyoelekeza na Kifungu cha 72 cha Sheria ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967. Hata hivyo suala la upatanishi wa maridhiano ya pande mbili (Mshitaki na Mshitakiwa hufanywa na wahusika kabla hawajafikishwa gerezani.

SPIKA: Mheshimiwa Zainab R. Kawawa, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba upo mpango wa Parole ambao unaruhusu mfungwa kukaa nje ya Magereza yaani Uraiani na kupangiwa kazi maalum hadi kile kipindi chake cha kifungo kitakapomalizika, sasa ninaomba kujua:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ZAINAB R. KAWAWA]

Je, mpango huo umekwishatekelezwa kwa kiasi gani mpaka sasa?

Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia kwamba ni wafungwa takribani wangapi wanaotumikia kifungo cha nje mpaka sasa?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Zainab Kawawa, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza ni kuhusu *Parole*, ni kweli kwamba kuna sheria ya *Parole* ambayo ina masharti ya kumfanya mfungwa ambaye ametumikia theluthi moja ya kifungo chake kuweza kutumikia kifungo hicho nje na msingi wa kwanza ni kwamba kifungo chake cha awali kiwe miaka minne au zaidi.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu huu, kila mwaka kuna utaratibu wa kuwaachilia wafungwa au kuwatoa kwenye Magereza kwa ajili ya ya kumaliza kifungo chao nje kama inavyotakiwa na sheria.

Pili, wangapi wameachiliwa chini ya *Community Service*.

Nafikiri hili nitamjibu baadaye kwa sababu ni tarakimu, nitazitafuta na nitampatia baada ya kikao hiki.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba muwe mnaangalia muda. Hatuna muda, na kazi mbele yetu ni nzito.

Kwanza niwatambue wageni tulio nao. Wageni walioko kwenye Jukwaa la Spika, ni watoto wa Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro. Naomba wasimame watoto. Inhi, ahsante sana.

Pamoja nao, yupo Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dodoma – Mheshimiwa Salome Kiwaya, yuko wapi. Usimame pamoja na wajumbe wako wote. Wako pia Maofisa kutoka Ofisi Kuu ya CCM Makao Makuu – Dodoma. Wasimame walipo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, ambao ni Ndugu James – huyu ni Mjumbe wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo na Ndugu Selemani Matoroka – Katibu wa Uhamasishaji Vijana. Hawa wasimame walipo. Ahsante sana.

Tuna Bi. Nariku Joan Josephine Ole-Medeye, huyu ni nani. Ni mtoto wa Naibu Waziri Ole-Medeye, naomba asimame pale alipo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Matangazo ya Kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 5.00 kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa B.

Halafu Katibu wa Wabunge wa Chadema, Mheshimiwa David Silinde, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa Chadema kuwa kutakuwa na Kikao leo saa 7.00 mchana baada ya Kuahirisha kikao hiki, katika Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala imeundwa kwa mujibu wa kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hii inasema:-

(1) *Kutakuwa na Kamati za Kudumu za Bunge kama zilivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizi".*

(2) *Muundo na Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge yameainishwa Kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizi.*

Majukumu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala yameainishwa katika Nyongeza ya Nane Fasili ya 7(1) kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazosisimamia;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia;

(c) Kufuatilia utetendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inazosisimamia; na

(d) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina jukumu la kuzisimamia shughuli za Wizara zifuatazo kwa mujibu wa Fasili ya 6 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge:-

- (a) Ofisi ya Rais:
 - (i) Utawala Bora;
 - (ii) Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
 - (iii) Uhusiano na Uratibu; na
 - (iv) Tume ya Mipango.

- (b) Ofisi ya Makamu wa Rais:-
 - (i) Makamu wa Rais;
 - (ii) Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano;
 - (iii) Ofisi ya Waziri Mkuu; na
 - (iv) Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Shughuli zilizotekelezwa na Kamati. Kwa mamlaka uliyopewa kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliteua Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mnamo Mwezi Februari, 2013.

Kwa kuwa Ujumbe katika Kamati za Kudumu za Bunge wa Bunge la Kumi ulidumu hadi pale Mkutano wa kumi ulipoisha na ambao ulihitimisha nusu ya Kwanza ya maisha ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (7), uongozi wa mara ya kwanza wa Kamati ulikoma hivyo kulazimu uchaguzi mwingine kufanyika ili kupata Viongozi wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida na kwa masharti wa Kanuni ya 116 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala walifanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kutoka miongoni mwao na kumchagua Mheshimiwa Dkt. Pindi H. Chana (Mb) kuwa Mwenyekiti wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

Kamati, pamoja na Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb) kuwa Makamu Mwenyekiti. Viongozi hawa ndio wameiongoza Kamati toka walipochaguliwa Mwezi Februari, 2013 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ina wajumbe 20, kwa heshima na taadhima nitawatambua huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2013/2014. Kuanzia tarehe 25 Machi, 2013 mpaka tarehe 5 Aprili, 2013, Kamati ilikutana katika Ofisi ya ndogo ya Bunge, Dar es Salaam kwa lengo la kupitia na kuchambua Bajeti za Wizara inazosimamia kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Wizara zinazosimamiwa na Kamati ziliwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Shughuli zake kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Baada ya mawasilisho yaliyofanywa, Wajumbe wa Kamati walichambua na kupitisha vifungu vya Bajeti za wizara hizo na kutoa mapendekezo ya marekebisho mbalimbali pale ilipohitajika. Aidha, Kamati ilishauri na kutoa maelekezo mahsusi kwa kila Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 ya Ofisi ya Rais-Ikulu, Menejimenti ya Umumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma na Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Mafungu yaliyopitishwa Katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni Kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

- (i) Ofisi ya Rais Ikulu – Fungu 20;
- (ii) Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri - Fungu 30;
- (iii) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Fungu 32;
- (iv) Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma - Fungu 33;
- (v) Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma-Fungu 67;
- (vi) Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma - Fungu 94; na
- (vii) Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma - Fungu 9.

Katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja kwa mafungu yote yaliyotajwa hapo juu Kamati iliidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni mia tatu sabini na tisa, milioni mia tisa sabini na tisa, laki saba arobaini na saba elfu na mia nane (379,979,747,800) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/214.

Kamati ilipata fursa ya Kupitia taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Tume ya Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 katika Fungu 66. Katika Kasma hii Kamati iliidhinisha Jumla ya Shilingi Bilioni arobaini, milioni miantano tisini na sita na mia tisa themanini na nne elfu(40,596,984,000) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

Kamati ilielezwa kwamba fedha hizo zilikusudiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

(a) Utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015 katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano yaani 2011/2012 - 2015/2016.

(b) Utangazaji na Usambazaji wa nyaraka mbalimbali za Tume ili kuwaelimisha wananchi kuhusu Dira ya Taifa ya maendeleo, Mpango Elekezi, Mpango wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka.

(c) Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013 na ule wa Mwaka 2011/2012 - 2015/2016 kupitia ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo Mwaka 2012/2013.

(d) Kufanya Utafiti katika maeneo Mbalimbali ya kiuchuni na Kijamii.

(e) Kuratibu Mfumo Mpya wa Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia uzoefu wa Performance Management and *Delivery Unit* (PEMANDU) ya Malaysia kwa kuanzisha Kitengo cha *President's Delivery Bureau (PDU)* kitakachofanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ili kuleta Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now (BRN)*).

Kamati ilipitia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Katika Ofisi ya Makamu wa Rais Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Ofisi ya Makamu wa Rais inajumuisha Mafungu yafuatayo:-

(i) Makamu wa Rais - Fungu 26; na

(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais - Fungu 31.

Katika Mafungu yote mawili Kamati iliidhinisha Jumla ya Shilingi Biloni Hamsini na tano, milioni mia sita themanini na mbili na mia nne kumi na nane elfu(55,682,418,000) kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)
Mwaka wa Fedha 2013/2014. Fedha hizi zilikusudiwa kugharamia shughuli mbalimbali zinazofanywa na Makamu wa Rais katika majukumu aliyonayo ya Kikatiba ya kufanya kazi yoyote atakayoagizwa na Rais pamoja na kushughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2012/2013 Katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha Kamati ilijadili na kupitisha Makadirio ya mapato na matumizi Katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha, 2013/2014. Kamati ilijadili na Kupitisha mafungu yafuatayo;

- (i) Waziri Mkuu - Fungu 25;
- (ii) Msajili wa Vyama Vya Siasa - Fungu 27;
- (iii) Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 37;
- (iv) Mfuko wa Bunge - Fungu 42; na
- (v) Tume ya Taifa ya Uchaguzi - Fungu 61.

Kamati iliidhinisha Jumla ya Shilingi bilioni mia mbili thelathini na tatu, milioni mia sita sitini na nne laki saba na hamsini na saba elfu (233,664,757,000) kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali yaliyoko katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na Kuchambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2013/2014 na pia kuchambua Mafungu yafuatayo yaliyo chini ya Wizara hiyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

- (i) Tume ya Mabadiliko ya Katiba - Fungu 8;
- (ii) Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12;
- (iii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Fungu 16;
- (iv) Mkurugenzi wa Mashitaka - Fungu 35;
- (v) Mahakama - Fungu 40;
- (vi) Wizara ya Katiba na Sheria - Fungu 41;
- (vii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55; na
- (viii) Tume ya Kurekebisha Sheria - Fungu 59.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati ilipata fursa ya kupata taarifa kutoka Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu taasisi tatu (3) zilizo chini yake ambazo inazisimamia kama ifuatavyo; Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini (*RITA*), Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (*Law School of Tanzania*) na Chuo cha Uongozi wa Mahakama (*Institute of Judicial Administration* (Lushoto).

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti. Mara baada ya Kamati kutimiza wajibu wake wa kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi katika Ofisi, Wizara na Idara zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni katika baadhi ya maeneo kwa lengo la kuboresha utendaji wa Serikali. Kamati inatumia fursa hii kuendelea kuisitiza ushauri wake kwa baadhi ya maeneo ili kuhakikisha kuwa yanafanyiwa kazi. Ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

- (1) Kuhusu ufinyu wa Bajeti zinazotengwa kwa Wizara na Idara, Kamati inashauri kwamba Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafute vyanzo mbadala vya fedha ili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

kuwezesha kutengwa kwa fedha za kutosha kuwezesha kutekelezwa kwa mipango inayokuwa imepangwa kutekelezwa na Wizara na Idara kwa miaka husika

(2) Kiasi cha fedha kinachokuwa kimetengwa kama bajeti ya Wizara au Idara yoyote ya Serikali kwa mwaka husika, ni vyema kikawasilishwa chote kama kilivyopangwa na kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Serikali.

(3) Kuweka mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa ujenzi wa majengo kwa ajili ya kutumika kama ofisi za Serikali ili kuepuka kutumia Fedha nyingi katika kulipia pango. Ujenzi wa majengo haya utaipunguzia Gharama Serikali ya ulipaji wa Pango na hivyo kuokoa fedha zinazotumika ili ziweze kutumika kufanya kazi nyingine. Serikali iboreshe mishahara na marupurupu ya watumishi ili kuwaongezea motisha ya kufanya kazi ili kuleta tija katika utumishi wa Umma.

(4) Kuajiri Watumishi wa Kutosha Katika Wizara na Idara ambazo hazina Watumishi wa Kutosha ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi.

(5) Serikali ihakikishe inapeleka Fedha zinazokuwa zimetengwa katika Mwaka wa bajeti husika kwenye Wizara na Idara kwa wakati ili kuhakikisha kuwa zinayanya kazi inayokuwa imekusudiwa kwani ucheleweshaji wake unakwamisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

(6) Kamati inaishauri Serikali kuzingatia Ushauru uliotolewa na Kamati wakati wa upitishwaji wa Bajeti kuhusu kuanzishwa kwa Mfumo wa Kupima utendaji kazi kupitia mikataba (*Performance Contracts*) wa Mawaziri na Watumishi wengine ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwajibikaji wa Serikali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Miswada ya Sheria. Kuanzia Mwezi Februari hadi Desemba, 2013 Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala inashughulikia pamoja na mambo mengine miswada mbalimbali ya Sheria inayopelekwa kwake na Mheshimiwa Spika kwa ajili ya Uchambuzi ili kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Julai 2013 Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni (*The Referendum Act, 2013*) kwa kupokea maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge na pia kupokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu muswada huo.

Mheshimiwa Spika, wadau mbalimbali walifika mbele ya Kamati kutoa maoni yao kuhusu Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni ya Mwaka 2013. Miongoni mwa Wadau waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao kwa mdomo au kuwasilisha kwa njia ya Maandishi ni kama wafuatao:-

(1) Vyama vya Siasa ni: CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM), *THE CIVIC UNITED FRONT* (CUF), CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO, *UNION FOR DEMOCRATIC* (UMD), *NATIONAL CONVENTION FOR CONSTRUCTION AND REFORM* (NCCR-MAGEUZI), *NATIONAL LEAGUE FOR DEMOCRACY* (NLD), *UNITED PEOPLE'S DEMOCRATIC PARTY* (UPDP), *NATIONAL RECONSTRUCTION ALLIANCE* (NRA), *ANZANIA DEMOCRATIC ALLIANCE* (TADEA), *TANZANIA LABOUR PARTY* (TLP), *UNITED DEMOCRATIC PARTY* (UPD), DEMOKRASIA MAKINI (MAKINI), CHAMA CHA HAKI NA USTAWI (CHAUSTA), *DEMOCRATIC PARTY* (DP), *AFRICAN PROGRESSIVE PARTY OF TANZANIA* (APPT - MAENDELEO), JAHAZI ASILIA, SAUTI YA UMMA (SAU), *TANZANIA FARMERS PARTY* (AFP), CHAMA CHA KIJAMIII (CCK), *ALLIANCE FOR DEMOCRATIC CHANGE* (ADC), CHAMA CHA UKOMBOZI WA UMMA (CHAUMA).

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

(2) Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali: *WOMEN'S LEGAL AID CENTRE (WILAC), LEGAL AND HUMAN RIGHT CENTRE (LHRC), TANZANIA NETWORK OF LEGAL AID PROVIDERS (TANLAP), TANZANIA WOMEN LOWYERS ASSOCIATION (TAWLA), JUKWAA LA KATIBA (JUKATA) TANGANYIKA LAW SOCIETY (TLS) na CHAMA CHA MAJAJI WASTAAFU (TARJA).*

(3) Taasisi za Elimu ya Juu: *CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM na CHUO KIKUU HURIA.*

(4) Taasisi za Dini: *TANZANIA EPISCOPAL COUNCIL OF TANZANIA (TEC) na CHRISTIAN COUNCIL OF TANZANIA (CCT).*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilinufaika sana na maoni na ushauri uliotolewa na wadau hawa. Kamati inatoa shukrani za dhati kwao kwani waliacha majukumu waliyokuwa nayo na kuitikia wito ya kufika mbele ya Kamati.

Aidha Kamati inatoa rai kwao kuendelea kushirikiana na Kamati kila inapowaalika kutoa maoni Katika Muswada mwingine wowote utakaowasilishwa mbele ya Kamati kwa lengo la kuuchambua na kuuboresha.

Mheshimiwa Spika, Muswada huo ulikusudia kuweka muundo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya uendeshaji wa Kura ya Maoni, kuweka masuala ambayo maoni ya wananchi yatahakikiwa kupitia Kura ya Maoni na kuweka masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Baada ya kufanya uchambuzi wa kina na pia kuchambua maoni ya wadau, Kamati ilitoa maoni yake ili kuuboresha Muswada huo ambapo kimsingi ilikubaliana na Serikali kubadilisha maudhui ya Muswada huo ili ujikite katika kushughulikia Kura ya Maoni ya Katiba itakayopendekezwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

Hii ilitokana na ukweli kwamba Msingi wa Sheria ya Kura ya Maoni ulitokana na Marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kwa kuondoa Sehemu ya Tano iliyohusu uhalalishwaji wa Katiba inayopendekezwa hivyo Kamati iliona ni muhimu Sheria ya Kura ya Maoni ikajikita Katika Katiba Mpya peke yake kuliko kuchanganya na masuala mengine yanayohitaji maoni ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana mabadiliko ya msingi yaliyotakiwa kufanyika na baada ya Serikali kukubaliana na Maoni na Ushauri wa Kamati ulitolewa, Muswada huo ulichapwa upya na kushughulikiwa na Kamati na hatimaye Ulisomwa kwa Mara ya pili na ya tatu katika Mkutano wa 14 wa Bunge, Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Agosti 2013, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2013 (*The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013*). Muswada huu ulikusudia kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu vya Sheria ya mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 Toleo la 2012.

Marekebisho haya, kwa ujumla yalilenga kuiboresha Sheria hiyo kwa kurekebisha kasoro za kisheria pamoja na kuziba mianya iliyoachwa, ili Sheria hiyo iweze kukidhi matakwa halisi ya mchakato wa kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulikuwa na mjadala mpana hasa kutokana na marekebisho yaliyokusudiwa kufanyika hususan katika Muundo wa Bunge Maalum la Katiba lakini hatimaye Kamati kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa, ilikubaliana na Serikali mambo ya msingi kuhusu muundo huo.

Aidha, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mengine kwa Muswada uliowasilishwa kwa hati ya dharura mnamo tarehe 6 Novemba, 2013 kwa kuendelea kuiboresha Muundo wa Bunge Maalum na kufafanua vyema mamlaka ya uteuzi wa Wajumbe 201 katika Bunge hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI)]

Baada ya Kamati ya Uongozi kuridhika kuwa Muswada ulikidhi masharti ya Kanuni ya 80 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013 Muswada uliwasilishwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ajili ya uchambuzi. Kamati iliuchambua Muswada na hatimaye kutoa maoni yake Bungeni. Hatimaye Muswada ulisomwa kwa mara ya pili na ya tatu na kupitishwa kuwa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yamesaidia sana kupiga hatua muhimu mbele Katika safari yetu ya kuelekea upatikanaji wa Katiba Mpya. Ni swala lililo wazi kwamba Uchambuzi na hatimaye utungaji wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba pamoja na marekebisho yake umeonyesha kwamba Tanzania imekomaa kisiasa kwa kuweza kuhimili mawimbi makubwa ya Kisiasa ambayo kama yangeweza kutokea katika Nchi nyingine, yangeweza kusababisha Machafuko ya Kisiasa.

Uwepo wa Sheria nzuri ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, pamoja na Sheria ya kura ya Maoni umeweka msingi mzuri na imara kuelekea Katiba Mpya. Ni matumaini ya Kamati kuwa huko tuendako tutavuka salama na kuweka historia mpya ya kuwa na Katiba Mpya iliyoshirikisha Wananchi wengi Katika Utpatikanaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika vikao vya Kamati mwezi Novemba, 2013, Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2013 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act No. 3, 2013*].

Muswada huo ulipendekeza kufanya marekebisho katika Sheria 15 kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo; kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano katika Sheria hizo; kufuta baadhi ya vifungu ambavyo ama vinaleta mkanganyiko katika utekelezaji wa Sheria husika au vimepitwa na wakati; na kuweka masharti mapya kwa ajili ya utekelezaji madhubuti wa Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Mheshimiwa Spika, katika vikao vya Kamati mwezi Novemba, 2013, Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2013 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act No. 3, 2013*].

Mheshimiwa Spika, Muswada huo ulipendekeza kufanya marekebisho katika Sheria 15 kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo; kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano katika Sheria hizo; kufuta baadhi ya vifungu ambavyo ama vinaleta mkanganyiko katika utekelezaji wa Sheria husika au vimepitwa na wakati; na kuweka masharti mapya kwa ajili ya utekelezaji madhubuti wa Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sheria zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo:-

- (a) Sheria ya Usafiri wa Anga (*The Civil Aviation Act*), Sura ya 80;
- (b) Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Majimbo (*The Constituencies Development Catalyst Fund Act*), Sura ya 96;
- (c) Sheria ya Mfuko wa Elimu (*The Education Fund Act*), Sura ya 412;
- (d) Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (*The Films and Stage Plays Act*), Sura ya 230;
- (e) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (*The Higher Education Students' Loan Board Act*) Sura ya 178;
- (f) Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*The National Council for Technical Education Act*), Sura ya 129;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

- (g) Sheria ya Magazeti (*The Newspapers Act*), Sura ya 229;
- (h) Sheria ya Viapo (*The Official Oaths Act*), Sura ya 266;
- (i) Sheria ya Kanuni za Adhabu (*The Penal Code*), Sura ya 16;
- (j) Sheria ya Kuzuia Ugaidi (*The Prevention of Terrorism Act*), Sura ya 19;
- (k) Sheria ya Mashirika ya Umma (*The Public Corporation Act*), Sura ya 257;
- (l) Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi Jamii (*The Social Security (Regulatory Authority) Act*), Sura ya 135;
- (m) Sheria ya Vyuo Vikuu (*The Universities Act*), Sura ya 346;
- (n) Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi (*The Vocational Education and Training Act*), Sura ya 82; na
- (o) Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori - Sura ya 283.

Mheshimiwa Spika, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinazohusika na Sheria hizo zilipokea maelekezo mahsusi juu ya marekebisho hayo na zilitoa ufafanuzi katika maeneo fulani fulani ambayo Kamati ilihitaji ufafanuzi. Maelezo na ufafanuzi uliotolewa na Wataalam wa Idara husika ulisaidia sana Kamati Katika kuchambua Muswada na kutoa ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba ili kuhakikisha kuwa Miswada ya Sheria inafanyiwa uchambuzi wa kina na Kamati, ni vyema Mwenyekiti wa Kamati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA] inayopelekewa Muswada akaandikiwa barua mapema mara tu Muswada unapokuwa umesomwa kwa Mara ya Kwanza. Uwasilishwaji mapema wa Miswada utaiwezesha Kamati kuwa na muda mrefu wa kuisoma na hatimaye kuishauri Serikali.

Kwa Miswada kuwasilishwa mapema mbele ya Kamati Kutaiwezesha Kamati kuwatambua wadau muhimu na hatimaye kuwaalika kufika mbele ya Kamati au kuwasilisha maoni yao kwa maandishi kuhusu uboreshaji wa Miswada ya Sheria.

Serikali iharakishe kuleta mbele ya Kamati Sheria zote ambazo utekelezaji wake ni mgumu kutokana na kupitwa na wakati ili ziweze kufanyiwa marekebisho na hatimaye kuboresha utendaji katika Wizara na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Semina na Mafunzo, katika Kuongeza uwezo na weledi wa kutimiza majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni, Kamati ilishiriki katika Semina Mbalimbali. Semina hizo ni Kama ifuatavyo:-

Semina kuhusu mfumo Mpya wa kusimamia utekelezaji, ufuatiliaji na Tatmini ya Miradi ya Mendeleo kwa kutumia uzoefu wa *Performance Management and Delivery Unit (PEMANDU)* ya Malasyia na Uanzishwaji wa Kitengo cha *Presidents Delivery Bureau (PDB)* iliyotolewa na Tume ya Mipango. Kamati ilielezwa kuwa Kitengo cha *President's Delivery Bureau* kimeshaanzishwa na kwamba awamu ya kwanza ya Ufuatiliaji na Tathmini ilizinduliwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 22 Februari, 2013 na awamu ya kwanza ilikuwa inahusisha masuala ya Elimu, kilimo, nishati, mapato, maji na miundombinu ya uchukuzi.

Semina kuhusu majukumu ya Bunge Maalum la Katiba Katika kujadili na Kupitisha Katiba Mpya iliyotolewa na Programu ya Utungaji wa Sheria inayodhaminiwa na Umoja wa Mataifa (*The Legislative Support Programme*). Semina hii ilifanyika Mwezi Agosti, 2013, Jijini Dar es Salaam.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Semina Kuhusu hatua zilizofikiwa katika kushughulikia Kero za Muungano pamoja na Changamoto zake iliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. Semina hii ilifanyika tarehe 27 Machi, 2013 Katika Ofisi ya Bunge, Dodoma.

Lengo la Semina hii ilikuwa ni kuiwezesha Kamati kujua namna ambavyo Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano inashughulikia Kero za Muungano ili kuziondoa kero hizo kwa lengo la kuimarisha Muungano.

Semina kuhusu mapambano dhidi ya rushwa iliyofanyika Mwezi Februari, 2013, hii ilifanyika Dar es Salaam kwa Wajumbe wote wa Kamati. Mwezeshaji Katika Semina hii alikuwa ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU).

Lengo la Semina hii ilikuwa ni kuiwezesha Kamati kufahamu hatua mbalimbali ambazo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inazichukua katika kukabiliana na vitendo vya rushwa pamoja na changamoto ambazo taasisi inakabiliana nazo katika mapambano hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala katika Mwaka 2013 ilifanya ziara mbalimbali ndani na nje ya nchi. Ziara zilizofanywa ndani ya nchi zilikuwa na maelengo ya kuangalia utendaji wa Serikali na Taasisi zake (*oversight function*) na pia kujifunza masuala mbalimbali. Kwa upande wa ziara zilizofanywa na Kamati nje ya nchi, lengo lilikuwa ni kujifunza kuhusu masuala mbalimbali ya utekelezaji wa Mabunge na Kamati za Bunge katika nchi hizo lakini mahsuszi zaidi, kujifunza kuhusu mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Machi, 2013 Kamati katika kuetekeleza wajibu wake wa usimamizi wa miradi ya maendeleo, ilitembelea miradi ya *TASAF* katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Pwani ambapo Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya wananchi iliyotekelezwa kwa ushirikiano na mfuko wa maendeleo ya jamii (*TASAF II*) iliwasilishwa kwa Wajumbe wa Kamati.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea ili kujionea Mradi wa Uhawilishaji Fedha katika Kaya Maskini katika Kijiji cha Mataya, Kata ya Kiromo, Bagamoyo ambao upo katika awamu ya tatu ya Utekelezaji wa Miradi (*TASAF III*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba *TASAF* imeweza kutekeleza mradi huu katika vijiji 43 na kwamba katika awamu ya kwanza vijiji vya majaribio vilikuwa 17, na baada ya mafanikio kwenye vijiji hivyo mradi uliendelea.

Aidha, Kamati ilipata ushuhuda kutoka kwa walengwa masikini waliopewa ruzuku kwa kupewa fedha na kujikwamua kwa kununua chakula, mavazi kwa watoto wa shule, huduma za matibabu kwa wazee wa miaka 60 na zaidi pamoja na walengwa kujianzishia miradi kama ufugaji kuku, mbuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala la Shule ya Sekondari Dunda ambapo Kamati ilielezwa kuwa mradi husika ulibuniwa na wananchi wa kijiji cha Dunda mnamo mwaka 2006 ambapo Kamati ya Ujenzi iliundwa na kuanza kutekeleza mradi kwa kushirikiana na *TASAF* ambao walichangia kiasi cha Sh. 52,789,165/= ili kugharamia ununuzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na gharama za ufundi.

Mtendaji wa Kijiji pamoja na wananchi walichangia kiasi cha Sh. 8,210,835/= kwa ajili ya kusafisha eneo, kuchimba msingi wa jengo, kuchimba mashimo ya taka, kusomba vifaa, gharama za mafundi wasaidizi na usafiri wa wana Kamati ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Aprili, 2013 Kamati ilifanya ziara ya kutembelea Jengo la Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo, Ufilisi na Udhamini (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency-RITA*) lililopo Mtaa wa Makunganya, Jijini Dar es Salaam. Kamati ilielezwa kwamba Jengo hili lina urefu wa Ghorofa 30 na linajengwa kwa ubia kati ya *RITA* na *NSSF*. Ujenzi ulikuwa katika hatua nzuri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo, Ufilisi na Udhadini kwa kubuni mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ambao kwa kiasi kikubwa utaupunguzia Wakala tatizo la upungufu wa Ofisi pamoja na kujiongezea Kipato kwa kupangisha Ofisi kwa Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba Katika ujenzi wa jengo hili Serikali kupitia wakala ilipaswa kutoa kiasi cha Shilingi bilioni 17 sawa na asilimia 69 ya gharama za mradi lakini hadi kufikia mwezi Aprili, Serikali haikuwa imetoa kiasi chochote cha fedha na hivyo kulazimu Fedha zote kutolewa na *NSSF*. Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi hicho haraka ili kuepuka riba kubwa inayoweza kujitokeza na hatimaye Serikali kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, mnano mwezi Oktoba, 2013 Kamati ilipata fursa ya kutembelea nchi ya Zimbabwe kwa madhumuni ya kujifunza masuala mbalimbali kama ilivyoelezwa awali. Kimsingi, Kamati ilipata fursa ya kuonana na viongozi wa Bunge la Zimbabwe, watu na Taasisi muhimu zilizohusika katika mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya.

Mwezi Novemba, 2013 Kamati ilipata fursa ya kuzuru nchi za Kenya na Ghana ambapo katika ziara ya Kenya, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake, na pia ilipata fursa ya kukutana na taasisi mbili muhimu katika utekelezaji wa Katiba Mpya ambazo ni Tume ya Kurekebisha Sheria Kenya (*Kenya Law Reform Commission*) pamoja na Tume ya Utekelezaji wa Katiba (*The Constitution Implementation Commission*).

Katika ziara iliyofanyika nchini Ghana, Kamati ilipata fursa ya kuonana na viongozi mbalimbali wa Bunge la Ghana na kufanya kikao cha pamoja na Kamati ya Katiba, Sheria na Masuala ya Bunge. Aidha, katika ziara hiyo, Kamati ilikutana na watu mahsusi ambao walihusika katika mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya ya mwaka 1992 na vilevile kuonana na Tume ya Marekebisha ya Katiba ambayo inahusika na mapendekezo ya marekebisha mbalimbali katika Katiba ya Ghana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Mheshimiwa Spika, ziara za Kamati katika nchi zilizotajwa zilikuwa za manufaa makubwa kwani Wajumbe wa Kamati wamejengewa uwezo wa kuisimamia Serikali vizuri zaidi na pia kuwaongezea maarifa hasa katika kipindi hiki ambacho nchi ya Tanzania iko katika mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya. Katika ziara hizo Kamati ilijifunza yafuatayo:-

Mambo ya Msingi ya kujifunza katika Ziara ya Kamati nchini Ghana. Nchi ya Ghana inaheshimu Tunu muhimu katika uendeshaji wa Shughuli za Bunge, mfano vikao vya Kamati kuanza kwa sala.

Kwa mujibu wa Katiba ya Ghana, Spika wa Bunge la Ghana hatokani na Wabunge. Endapo Spika mteule aliyechaguliwa anatoka miongoni mwa Wabunge basi anapaswa kujuzuru mara moja nafasi ya Ubunge. Sababu za msingi za Spika kutotoka miongoni mwa Wabunge ni kuhakikisha kuwa anafanya kazi zake bila upendeleo na hasukumwi kwa namna yoyote ile na misukumwi ya Chama chake.

Muswada wowote ule ni lazima upitie Katika Kamati ya Bunge ya Katiba na masuala ya Bunge kwa lengo la kuuchambua na kuuboresha. Hii inatokana na matakwa ya kikanuni kuwa Kamati ya Katiba, Sheria na Masuala ya Bunge ndiyo yenye mamlaka kuchambua na kupitisha Miswada ya Sheria.

Asilimia 15 ya Wabunge wa Bunge la Ghana wanaweza kuitisha kikao cha Bunge mara baada ya kumwandikia Spika kuhusu kusudio la kuitisha kikao cha Bunge. Spika akishapokea barua kwa maandishi anawajibika kuitisha kikao cha Bunge ndani ya siku saba. Rais wa Ghana hana mamlaka Kikatiba kulivunja Bunge.

Raslimali na mali asili za Ghana Kama madini, gesi na mafuta yanalindwa kikamilifu Kikatiba ili kuhakikisha kuwa hakuna uvunaji wa holela na kuhakikisha kuwa wananchi wa Ghana wananufaika kikamilifu na mali asili za nchi yao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Asilimia arobaini ya wananchi wa Ghana wanaweza kufanya mabadiliko ya vipengele muhimu (*Entrenched Provisions*) vya Katiba kupitia kura ya maoni. Ili mabdiliko haya ya vipengele muhimu yakubalike asilimia 75 kati ya asilimia 40 ya wapiga kura waliojiandikisha kupiga wanapaswa kuyakubali mabadiliko hayo. Nchi ya Ghana inawaenzi kikamilifu Waasisi wa Taifa kwa kujenga eneo zuri la kihistoria linalotunza kumbukumbu ya Mwasisi wa Taifa hilo litwalo *Dkt. Kwame Nkrumah Memoria Park* lililopo, Accra, Ghana.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mambo ya msingi ya kujifunza katika ziara ya Kamati nchini Kenya. Kwa muhtasari, Wajumbe wa Kamati walijifunza masuala yafuatayo katika ziara waliyofanya nchini Kenya:-

Kwamba mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya, ulianza siku nyingi na ulishika kasi kuafuatia machafuko ya kisiasa kufuatia uchaguzi wa mwaka 2007.

Tofauti na mapendekezo yaliyopo kwenye mchakato wa Tanzania, Kenya hawakuwa na Bunge Maalum na badala yake, Bunge la kawaida lilijigeuza na kuwa Bunge la Katiba. Mara baada ya Bunge kupitisha Katiba kura ya maoni iliitishwa ili kuhalalisha Katiba iliyopendekezwa. Katiba iliyopatikana ilibadili mfumo wa kiutawala, wa Bunge na Taasisi nyingine kutokana na mapendekezo ya wananchi.

Katiba iliyotungwa iliweka mfumo wa kuhakikisha utekelezaji wa Katiba unakuwa wa ufanisi. Taasisi hizo ni Tume ya Utekelezaji wa Katiba (*The Constitutional Implimentation Committee*), Kamati ya Bunge ya Utekelezaji wa Katiba (*The Constitutional Implimentation Oversight Committee*), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (*The Attorney Generals' Office*) na Tume ya Kurekebisha Sheria ya Kenya (*The Kenya Law Reform Commission*). Kwamba, baada ya kutungwa kwa Katiba, utungaji wa sheria mbalimbali kwa madhumuni ya utekelezaji wa Katiba hiyo ni suala ambalo linapaswa kufanyika kwa haraka na kwa ufanisi na kushirikisha kikamilifu taasisi zenye wataalam wa kutosha katika masuala ya sheria.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Bunge la Kenya lina Mfumo wa Mabunge Mawili katika ngazi ya Taifa *Senate* na *National Assembly*. Aidha, kuna Mabunge ya Serikali za majimbo, yaani (*County Assemblies*).

Katiba mpya ikiandaliwa ni muhimu kutambua taasisi muhimu kikatiba za kusimamia utekelezaji wa Katiba. Taasisi hizo ni; Tume ya Kurekebisha Sheria ya Kenya, Tume ya Utekelezaji wa Katiba (*The Constitutional Implementation Commission*) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kamati ya Bunge ya utekelezaji wa Katiba (*The Constitutional Implementation Oversight Committee*).

Mambo ya msingi ambayo kamati imejifunza katika ziara ya kamati nchini Zimbabwe. Mchakato wa uundwaji wa katiba katika nchi yoyote unapaswa kuwa wa wananchi na kwa kiwango kikubwa unapaswa kumilikiwa na wananchi. Lengo la Serikali au Taasisi nyingine kutoingilia mchakato ni kutoa uhuru mpana kwa jamii kuweka mifumo ya kiutawala ambayo wao wanadhani itakuwa thabiti katika uendeshaji wa Serikali yao. Mchakato wa Katiba Mpya Katika nchi yoyote unapaswa kuwa wa kisiasa zaidi.

Serikali inapaswa kuwa sikivu kwa wananchi ili kuhakikisha kuwa pale wananchi wanapohitaji kuandika Katiba Mpya ni vyema wakasikilizwa ili kuepuka machafuko yanayoweza kupelekea maafa makubwa katika harakati za kudai Katiba Mpya kama ilivyotokea nchini Zimbabwe.

Katiba inayoandikwa ni muhimu kutambua mahitaji ya makundi yote ya kijamii na kuyapa nafasi ya kushiriki kwa namna moja au nyingine katika mifumo ya utawala wa nchi. Katika kuzingatia hili, Katiba Mpya ya Zimbabwe imetambua uwepo wa machifu wa kijadi kama mojawapo wa Wabunge wa Bunge la *Senate*.

Uteuzi wa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi unapaswa kufanyika kupitia njia iliyo huru na ikibidi ya ushindani kwa wananchi wote wenye sifa. Mara baada ya kupatikana wajumbe kupitia njia huru naya ushindani, ndipo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Rais ateue mwenyekiti miongoni mwa wajumbe hao. Hii itaongeza imani kwa wananchi juu ya uhuru wa Tume Huru ya Uchaguzi kama inavyofanyika katika uteuzi wa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi nchini Zimbabwe.

Kuaminiana na kuheshimiana ni nyenzo muhimu katika uendeshaji wa mchakato wa Katiba kwani mazingira yoyote ya kutoaminiana yanaiweka jamii katika hali ya hofu. Wakati wowote kunapotokea migogoro au mkwamo katika mchakato wa Katiba, suluhu bora ni kwa pande zinazohusika kukaa chini na kuzungumza ili kuondoa tofauti hizo.

Katika mchakato wa Katiba maslahi ya nchi yanapaswa kuwekwa mbele wakati wote na kuweka pembeni itikadi zozote za vyama, dini, rangi, kabila au tofauti nyingine zozote.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Pia, namshukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote ambao Wizara, Idara na Taasisi zao zinasimamiwa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee Kamati inapenda Kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah kwa utayari wake wakati wote na usikivu wa hali ya juu aliouonyesha katika kipindi chote. Katibu wa Bunge ameipezeshwa kwa kiasi kikubwa sana Kamati kutimiza majukumu yake kwa kuipatia nyenzo na vitendea kazi vinavyohitajika ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. Aidha Kamati inatoa Shukrani kwa Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. B. BLANDES – KAIMU MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

SPIKA: Ahsante. Nasikitika kwamba nakala uliyowasilisha Mezani hakuna. Kitabu chenu, kiko wapi? Kitabu chenu hakipo.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa niaba yake, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa John Lwanji.

MHE. PAUL J. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Machi hadi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, naomba majina 17 ya Wajumbe wa Kamati yaingie katika *record* ya Hansard.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati, Wajumbe wa Kamati waliteuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 113, Kanuni za Bunge, Toleo la April, 2013, mwezi Machi, 2013 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla - Mwenyekiti, Mheshimiwa John Paul Lwanji Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe ni Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mheshimiwa Eugen Elishiringa Mwaiposa, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mheshimiwa Eng. Athuman Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Sylvester

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Masele Mabumba, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeundwa kwa mujibu wa kanuni ya 116 ya Kanuni za kudumu za Bunge na majukumu yake yamefafanuliwa katika nyongeza ya Nane kifungu cha 7(1) kuwa ni kushughulikia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa); kushughulikia Miswada ya sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; kushughulikia utekelezaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya TAMISEMI, kushughulikia taarifa za utekelezaji za kila mwaka za Ofisi hiyo, na kufuatilia utekelezaji unaofanywa na TAMISEMI kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hiyo, Waheshimiwa Wabunge wataelewa tofauti iliyopo katika Kamati hii mpya na ile ya LAAC, ya Hesabu za Serikali.

Aidha, Kifungu cha 7(2)(c)(i) kinaipa Kamati hii jukumu mahususi la kuchambua Sheria Ndogo zilizotungwa na Halmashauri za Miji, Wilaya Manispaa na Majiji ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za kisera zinazotekelezwa na Halmashauri zote nchini kama ilivyoelezwa katika Nyongeza ya Nane kifungu cha 7(c) (ii) cha Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, msingi wa utekelezaji wa majukumu, msingi wa Kamati kutekeleza majukumu yake unatokana na ibara ya 96 ya Katiba inayolipa mamlaka Bunge kuunda Kamati zake kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kwa msingi huo, Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama chombo kimojawapo kilichoundwa kwa mujibu wa ibara hiyo, hutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Katiba ya nchi na Kanuni za kudumu za Bunge kwa niaba ya Bunge.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa, kusimamia Mikoa, Halmashauri na kufuatilia utekelezaji wa sera. Katika kipindi hiki Kamati imetekeleza majukumu yake kwa kuisimamia Mikoa 25 ya Tanzania Bara, Halmashauri za Jiji tano, Halmashauri za Manispaa 18, Halmashauri za Wilaya 130, na Halmashauri za Miji midogo 10 kwa namna mbalimbali ikiwemo ziara na kupitia ushauri na maoni ya kamati katika nyakati mbalimbali. Aidha, Kamati imefuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za utekelezeji wa Sera ya Elimu ya Msingi na Sekondari, Sera ya Afya, masuala ya miundombinu iliyo chini ya mamlaka ya Serikali za Mitaa, masuala ya Ardhi yaliyo chini ya mamlaka ya Serikali za Mitaa masuala ya maji, masuala ya mazingira na mali asili chini ya mamlaka ya Serikali za Mitaa, pamoja na masuala ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanya na Kamati ni kusimamia Taasisi na mashirika mbalimbali yaliyo chini ya Wizara. Taasisi hizo ni pamoja na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Mfuko wa *Pension* wa *LAPF*, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (*DART*), Shirika la Elimu Kibaha, Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam (*UDA*), na Mfuko wa barabara wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa awali, jukumu mojawapo la Kamati hii ni kuchambua sheria ndogo za Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji ili kujiridhisha kama zinakidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria mama na Sheria nyingine za nchi. Msingi wa jukumu hili ni kuwa kutokana na majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na Bunge, chombo hicho kimekasimu baadhi ya madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka mbalimbali.

Kwa kutambua kuwa mamlaka zinaweza kutumia vibaya fursa hiyo, Kamati yangu imepewa jukumu la kufuatilia na kuzisimamia sheria hizo ili kuona kama haziendi kinyume na matakwa ya kikatiba na sheria mama. Endapo kutotokea dosari yoyote ni jukumu la Kamati hii kulishauri Bunge kuzichukulia hatua zinazostahili mamlaka zote zilizokiuka matumizi ya sheria hizo. Hata hivyo, pamoja na jukumu hilo,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

katika kipindi hiki Kamati haikuwahi kutekeleza jukumu hilo kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Kamati ilitekeleza jukumu la kupitia taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Fungu 56 pamoja na taarifa za utekelezaji za Mikoa 25 ya Tanzania bara na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Mamlaka za Mikoa 25 ya Tanzania Bara kwa mwaka 2013/2014 kuanzia tarehe 26 Machi, 2013 hadi tarehe 06 Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuridhika na ufafanuzi uliotolewa na Serikali Kamati ilipitisha Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Mikoa yote 25 na kuwasilisha maoni yake Bungeni ikiwa ni pamoja na kuliomba Bunge lipitisha makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Mikoa 25 ya Tanzania barakatika Mkutano wa kumi na moja wa Bunge hili la kumi jumla ya Shilingi trilioni 4,107,009,288,802/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa jukumu la kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 na uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya 2013/2014 kwa Fungu 56 pamoja na bajeti za Mikoa yote 25 ya Tanzania bara lilitekelezwa kikamilifu na hatimaye kuhitimishwa na Bunge lako Tukufu kukubali na kupitisha bajeti husika.

Mheshimiwa Spika, ziara na taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Mkoa, Halmashauri, Mashirika na Taasisi mbalimbali. Katika kufuatilia kwa vitendo utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mikoa, Halmashauri na Taasisi mbalimbali za Wizara, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara ya kukagua miradi katika baadhi ya Mikoa, Halmashauri, Mashirika na Taasisi mbalimbali ikiwemo:-

- Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;
- Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

- Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo);
- Kupokea taarifa kuhusu Mfuko wa Barabara wa Serikali za Mitaa;
- Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (*DART*);
- Mradi wa Dar es Salaam *City Council Business Park (Machinga Complex)*;
- Kupokea taarifa ya uendeshaji wa Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam (*UDA*);
- Miradi ya maendeleo katika Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam (Temeke, Ilala na Kinondoni);
- Taarifa ya utendaji wa Mfuko wa *Pension wa LAPF*;
- Miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Jiji la Arusha;
- Miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi;
- Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha; na
- Kupokea taarifa ya mwenendo wa ukusanyaji wa kodi za majengo (*Property tax*) na ada za Leseni za Biashara kutoka Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, semina kwa kutambua kuwa semina zina umuhimu wa pekee katika kupanua uelewa wa Wajumbe kuhusu masuala mbalimbali. Katika kipindi hiki Kamati ilipata Semina mbalimbali zilizolenga kuongeza uelewa katika maeneo inayosimamia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, ukiondoa semina zilizoratibiwa na kuwezesha na Ofisi ya Bunge, Semina ya kwanza ilitolewa na LAPF tarehe 21/04/2013 na ilihusu majukumu na uendeshaji wa Mfuko wa Pensioni wa LAPF. Semina hii iliawezesha Wajumbe kupata uelewa kuhusu Mfuko wa Akiba za Pensheni za Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF) majukumu yake na namna unavyojendesha kwa manufaa ya wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, Semina nyingine ilifanyika tarehe 21/4/2013 katika ukumbi uliopo Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI Dodoma. Semina hii iliandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kupitia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ilihusu majukumu na uendeshaji wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Semina hii iliwaongezea uelewa Wajumbe kuhusu majukumu na uendeshaji wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.

Aidha, Kamati ilipata Semina kuhusu muundo na majukumu ya Idara ya Uratibu wa Elimu. Semina hii iliandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kupitia Idara ya Uratibu wa Elimu na ilifanyika katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo tarehe 04/05/2013. Kupitia semina hii Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kuyatambua vyema majukumu na kuongeza uelewa kuhusu uratibu wa Elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria Semina kuhusu majukumu na uendeshaji wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo iliyofanyika katika Chuo hicho tarehe 04/05/2013. Semina hii iliwapa uelewa mpana Wajumbe kuhusu majukumu na uendeshaji wa Chuo cha Serikali za Mitaa ikizingatiwa kwamba uwepo wa Chuo hiki ni muhimu sana katika kuwajengea uwezo watendaji wa Serikali hususani watendaji wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata Semina kuhusu mfumo wa kisasa wa kielektroniki wa ukusanyaji wa kodi za majengo unaotumiwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha. Semina hii iliandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na ilifanyika katika ukumbi wa Wizara hiyo. Semina hii iliwapa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

uelewa mzuri Wajumbe wa Kamati kuhusu mfumo huu mpya wa kisasa wa ukusanyaji wa kodi za Majengo katika mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Semina hizo zilikuwa na manufaa makubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ikiwa katika utekelezaji wa moja ya majukumu yake makuu ya kuisimamia Serikali ilifanya ziara katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro na Pwani. Halmashauri zilizotembelewa katika Mikoa hiyo ni:-

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Ilala, Kinondoni, Halmashauri ya Jiji la Arusha, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi na Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, ikiwa katika ziara hizo Kamati ilijika katika kukagua Miradi ya maendeleo katika Sekta ya Miundombinu ya utawala, miundombinu ya barabara, miundombinu ya huduma za afya, miundombinu ya huduma ya elimu, miundombinu ya huduma ya maji, miundombinu ya kilimo, masuala ya ardhi, utawala bora na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kuelezea matokeo ya ziara za Kamati na mambo ambayo Kamati iliyabaini katika maeneo niliyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Dar es Salaam kuanzia tarehe 16 - 23 Oktoba, 2013. Baadhi ya miradi iliyotembelewa na Kamati katika Mkoa kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Temeke ni mradi wa ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Temeke, kuhakiki ununuzi na bei za magari manne yaliyonunuliwa na Halmashauri kwa jumla ya Shilingi milioni 240, ukarabati wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa gharama ya Shilingi milioni 57,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Msingi Keko kwa gharama ya Shilingi milioni 45.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa ukarabati wa Machinjio ya vingunguti, upanuzi wa jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) katika Kituo cha Afya Pugu Kajiungeni, ujenzi wa jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Pugu Kajiungeni (*theatre*), ununuzi wa madawati katika Shule ya Msingi Hekima Buguruni, kukagua ujenzi wa kipande cha barabara ya Magore, kutembelea na kukagua Soko la Samaki Feri.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea na kukagua Miradi ya ujenzi wa Choo katika Shule ya Msingi Mugabe Sinza na Shule ya Kilimani iliyopo Manzese, ujenzi wa Machinjio ya kuku katika Soko la Mtambani Kinondoni, ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje *OPD* katika Hospitali ya Mwananyamala, Ujenzi wa *National Insurance Ward* katika Hospitali ya Mwananyamala, kukagua manunuzi wa vifaa vya kitaalamu *Ultra Sound machine, X-Ray Film Processor, Dental Chair Unit* vilivyoununuliwa na Hospitali ya Mwananyamala.

Mheshimiwa Spika, katika miradi mingi iliyotembelewa katika Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam Kamati ilibaini upungufu mbalimbali ikiwemo ubora hafifu wa miradi ya maendeleo ikilinganishwa na thamani halisi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, licha ya kazi iliyofanyika kutoakisi thamani halisi ya fedha zilizotumika katika miradi husika, Kamati ilibaini upungufu mbalimbali katika majengo yaliyojengwa kama vile nyufa katika kuta za majengo na sakafu ikizingatiwa kuwa baadhi ya miradi hiyo haijamaliza hata mwaka mmoja tangu kukamilika kwake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wenye thamani ya bilioni 15.2. Taarifa ya utekelezaji wa mradi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

huo ilibainisha changamoto mbalimbali ikiwemo bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya mradi husika; mtriko wa fedha zilizoidhinishwa kutoridhisha; fedha za mradi husika kutopelekwa kwa wakati ama kutopelekwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya changamoto zimeshaanza kufanyiwa kazi na Serikali ikiwemo kuongeza kiasi cha Shilingi bilioni moja katika bajeti ya mwaka 2013/2014 ili kuchochea kasi ya ujenzi wa mradi huu ili kuepuka gharama zitakazotokana na riba ya deni kwa mkandarasi pamoja na gharama za kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilipata fursa ya kutembelea Mkoa wa Kilimanjaro hususan Halmashauri ya Manispaa ya Moshi na Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, ikiwa katika Mkoa wa Kilimanjaro hususan Halmashauri ya Manispaa ya Moshi na Halmashauri ya Wilaya ya Siha Kamati ilikagua miradi mbalimbali katika sekta ya afya, elimu, maji na kilimo.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni Mradi wa uchimbaji wa Visima vitano wenye thamani ya Shilingi milioni 230 mpaka kukamilika kwake, Mradi wa ujenzi wa nyumba ya Mganga Mkuu wa Zahanati ya Longuo "B" wenye thamani ya Shilingi milioni 79, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) katika Kituo cha Afya cha Pasua wenye thamani ya Shilingi milioni 85.36, Mradi ya Ujenzi wa Madarasa manne katika Shule ya Sekondari Moshi Ufundi, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu katika Shule ya Sekondari Karanga wenye thamani ya Shilingi milioni 22, Mradi wa Ujenzi wa Maabara katika Shule ya Sekondari Msasani wenye thamani ya Shilingi milioni 108, pamoja na mradi wa ununuzi wa Maabara manne zinazohamishika (*Mobile Laboratories – 4*) na Mradi wa Ujenzi wa Mfereji wa umwagiliaji wa Ng'ambo wenye thamani ya Shilingi milioni 33.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya Siha Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya Siha wenye thamani ya Shilingi bilioni tatu, Mradi wa Ujenzi wa nyumba tano za watumishi wa Halmashauri hiyo wenye thamani ya Shilingi milioni 345.92, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Majaribio ya Lawate Kibong'oto yenye urefu wa Kilometa 13.48 wenye thamani ya Sh. 1,765,000,000/=, mradi wa maji katika kijiji cha Wiri wenye thamani ya Shilingi milioni 741, Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Magadini ambao mpaka sasa umeshatumia kiasi cha Shilingi milioni 85.9 na Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya unaokusudiwa kugharimu kiasi cha Shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kamati iliridhishwa na utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Kilimanjaro. Hata hivyo, Kamati inautaka uongozi wa Mkoa kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Kamati kuhusu kurekebisha kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika Halmashauri tulizozitembelea.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida wenye thamani ya Shilingi bilioni 150 mnamo tarehe 21 Machi, 2013. Taarifa iliyowasilishwa na Katibu Tawala wa Mkoa ilibainisha changamoto mbalimbali ikiwemo kasi ndogo ya mtiririko wa fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya kutekeleza mradi huu na bajeti ndogo inayotengwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua jitihada za Serikali baada ya kukubali kuongeza kiasi cha bilioni mbili kwenye bajeti ya mwaka 2013/2014 katika mradi husika.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwepo kwa changamoto hizo Kamati pia ilibaini mapungufu kadhaa katika utekelezaji wa mradi husika mfano gharama kubwa iliyotajwa kutumika kujenga kibanda cha kuchomea taka za hospitali ikilinganishwa na hali halisi ya kibanda hicho. Mfano *BOQ* ilionyesha kuwa kibanda hicho kilitumia bati 600 zenye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

geji 28 na urefu wa mita tatu zenye thamani ya milioni 10 wakati bati zilizotumika katika kibanda hicho hazidi bati 100. (Makofi)

Aidha, Kamati ilibaini kuwepo kwa upungufu mbalimbali katika utekelezaji wa mradi kama vile, nyufa kwenye kuta mbalimbali za majengo ambayo yameshakamilika na kukabidhiwa; mfumo mdogo wa hewa kwenye *theatres* na sehemu za mapumziko ya wagonjwa na sehemu ya mapokezi ya wagonjwa; na Kutokuwepo kwa barabara ya uhakika (barabara ya lami) kutokea mjini hadi Hospitali.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati yangu ilifanya ziara ya kukagua na kupokea taarifa ya Mradi wa upanuzi wa Hospitali ya Tumbi Kibaha siku ya tarehe 24 Oktoba, 2013 kwa lengo la kujionea maendeleo ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Elimu Kibaha, Kamati ilielezwa kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa ujenzi wa jengo kuu hatua ya kwanza ya kwamba ujenzi huo ulioanza tarehe 15 Aprili, 2009 na ulikamilika 28 Julai, 2011 kwa asilimia 99, ambapo jumla ya Sh. 3,375,569,344/= zilitumika.

Aidha, Kamati ilielezwa kwamba awamu ya pili ya ujenzi iliyoanza rasmi 25 Julai, 2011 imefikia asilimia 15 tu ambapo kiasi cha Sh. 1,554, 589,795/= kimeshatumika mpaka sasa. Kamati ilielezwa kuwa mradi huo ulipaswa kukamilika 22 Julai, 2012 lakini mpaka sasa umefikia asilimia 15 na ujenzi wake umesimama kutokana na ukosefu wa fedha za kuendeleza ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa na kutembelea eneo la Mradi Kamati imebaini kuwa changamoto kubwa inayoukabili Mradi wa Upanuzi wa Hospitali ya Tumbi ni ukosefu wa fedha. Hii inatokana na kutoletwa kwa fedha kiasi cha Shilingi bilioni 2.5 kila mwaka kama ilivyoahidiwa na Serikali Kuu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya ziara katika Mkoa wa Arusha hususan katika Halmashauri ya Jiji la Arusha kwa lengo la kupokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo na kukagua baadhi ya Miradi kuanzia tarehe 9 - 12 Oktoba, 2013. Miradi ifuatayo ilitembelewa na Kamati:-

- (i) Ujenzi wa Miundombinu ya maji katika maeneo manne ya Sino, Sokon 1, Mkonoo na Nadosoito ulitengewa kiasi cha Sh. 895,645,751.70;
- (ii) Mradi wa ujenzi wa madarasa manne ya ghorofa Shule ya Sekondari Themu uliotengewa kiasi cha Sh. 179,757,000/=; na
- (iii) Mradi wa ujenzi wa madarasa manne Shule ya Sekondari Sombetini uliotengewa kiasi cha Sh. 272,518,200/=.

Katika ziara hiyo Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Halmashauri ya Jiji la Arusha na Mkoa kwa ujumla. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

- (i) Kuchelewa kufika kwa fedha za ruzuku ya Maendeleo na fedha za Ruzuku kufika pungufu ya bajeti;
- (ii) Mapungufu katika ujenzi wa miradi ya maendeleo hususani viwango vya ubora; na
- (iii) Kutofuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Bunge la Uingereza mnamo tarehe 25 Novemba, 2013 ambapo ilikutana na Mwenyekiti wa Kamati teule inayohusika na mambo ya Serikali za Mitaa.

Katika ziara hiyo Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kubadilishana uzoefu na Mwenyekiti huyo kwa kuuliza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

maswali mbalimbali yanayohusiana na utendaji kazi wa Kamati yetu hususan namna ya usimamizi wa Serikali za Mitaa kwenye maeneo ya afya, elimu na miundombinu, utawala bora pamoja usimamizi wa Sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ziara hiyo ilikuwa na manufaa makubwa katika kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika eneo la kusimamia Serikali za Mitaa katika nchi yetu. Hivyo, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuona busara na kutoa kibali cha kwa Kamati ili kufanya ziara hiyo.

Kamati hii ilikutana na Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam na Halmashauri zake zote siku ya tarehe 23 Oktoba, 2013 kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa ya makusanyo ya mapato ya kodi za majengo na ada za leseni za biashara kuanzia Julai 1 hadi Septemba 30, 2013.

Dhumuni kuu la kikao hicho ilikuwa ni kutaka kujua mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika maeneo tajwa ili kupata mwelekeo wa utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, Kamati ilitaka kujua changamoto zilizopo katika ukusanyaji wa kodi za majengo na ada za leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, changamoto za ukusanyaji wa kodi za majengo kutokana na taarifa iliyowasilishwa, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto zifutazo katika ukusanyaji wa kodi za majengo na ada za leseni za biashara:-

- (1) Kutokamilika kwa jedwali la uthamini kwa wakati kulikosababisha ucheleweshaji wa utoaji hati za madai (*demand notes*). Ilielezwa kuwa hati za madai zilianza kutolewa na TRA mwishoni mwezi April, 2013;
- (2) Kutokuwiana kwa mfumo uliotumika kuandaa jedwali jipya la uthamini na mfumo unaotumiwa na TRA (*TRA-ITAX*);

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

- (3) Kutokuwepo kwa chombo cha kusikiliza malalamiko ya wenye majengo kwenye jedwali jipya la kodi ya majengo (*Property tax Rating Tribunal*);
- (4) Imeelezwa pia, Majengo ya Serikali hayalipiwi kodi za majengo mfano Benki kuu, Hazina, Wizara mbalimbali, *TRA* pamoja na majengo ya Taasisi mbalimbali;
- (5) Ukosefu wa vitendea kazi muhimu kama vile magari ilitajwa kuwa ni changamoto katika ukusanywaji wa kodi za majengo;
- (6) Kutokuwa na taarifa za walipakodi na ambao hawajalipa kwani malipo yanayopelekwa kwenye Halmashauri hayana viambatanisho vya kuonesha majina yanayoendana na kiasi kilicholipwa;
- (7) Kutokuwepo kwa kanuni (*Regulations*) zinazoongoza mwenendo mzima wa ukusanyaji wa kodi ya majengo; na
- (8) Mfumo wa *TRA* kushindwa kutoa hati ya madai inayojumuisha madeni ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, Taarifa zilizowasilishwa zilibainisha changamoto zifutazo:-

Ilielezwa kuwa Kitengo cha biashara kutounganishwa na mfumo wa *MRECOM* katika ukusanyaji wa ada za leseni za biashara; Ukosefu wa usafiri wa uhakika katika Kitengo cha Biashara; Wafanyabiashara wengi kutoitika wito wa kulipa ada za leseni za biashara baada ya sheria kuruhusu kutoza ada za leseni ni changamoto nyingine katika ukusanyaji wa ada za leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu Mfuko wa barabara wa Serikali za Mitaa tarehe 14 Agosti,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

2013 na 8 Novemba, 2013. Katika taarifa hizo Kamati ilielezwa kuwa pamoja na majukumu mengine Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI imepewa jukumu la kusimamia uendelezaji na uratibu wa matengenezo, ukarabati pamoja na ujenzi wa barabara na madaraja chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ilielezwa pia kuwa sehemu kubwa ya utekelezaji jukumu hilo, unategemea fedha za Mfuko wa barabara ambapo mapato yake yanatokana na ushuru wa mafuta ya petroli na dizeli na faini za magari yaliyozidisha mizigo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya barabara ya mwaka 2007 ilianzisha mtandao wa barabara za Halmashauri zenye jumla ya urefu wa kilometa 56,625. Hata hivyo, imeelezwa kuwa Sheria hiyo ilitungwa wakati utambuzi wa barabara katika Halmashauri (*Local Government Road Inventory and Condition Survey*) ulikuwa haujakamilika, hivyo kupelekea baadhi ya barabara za Halmashauri kuachwa.

Vilevile Kamati ilielezwa kuwa mtandao wa barabara za Halmashauri umezidi kuongezeka kutokana na kuanzishwa kwa maeneo mapya ya utawala. Kutokana na sababu hizo, ilielezwa kuwa mtandao wa barabara uliowasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hivi sasa unafikia jumla ya Kilometa 96,096 kutoka 56,625 za awali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko hilo kubwa la mtandao wa barabara za Halmashauri kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

(1) Fedha za mfuko wa barabara za Serikali za Mitaa hazitoshelezi mahitaji halisi. Mgawanyo wa fedha za barabara kwa uwiano wa 30% kwa barabara za Halmashauri na 70% kwa barabara za *TANROADS* kwa mujibu wa Sheria ya barabara hauendani na ukweli kwamba mtandao wa barabara za Halmashauri ni mkubwa kuliko mtandao wa barabara za *TANROADS*. Aidha, mgawanyo huu haujazingatia umuhimu wa barabara za Halmashauri na umuhimu wa kuweka viwango sawa vya ubora wa barabara za Halmashauri na barabara za *TANROADS*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

(2) Changamoto nyingine iliyobainika ni kuchelewa kutolewa kwa fedha za barabara na wakati mwingine fedha hutolewa baada ya mwaka fedha husika kupita na hivyo kuhesabika kama sehemu ya bakaa. Mfano, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha Shilingi bilioni 24 zilipokelewa mwezi Julai na Agosti, 2013 na kupelekea kuhesabika kama bakaa hivyo kutotumika kutekeleza miradi iliyokusudiwa kwa wakati.

(3) Ukosefu wa vifaa vya kupimia ubora wa kazi za barabara katika Halmashauri hivyo kutegemea Maabara za *TANROADS* zilizopo mbali na Makao Makuu ya Halmashauri nyingi.

(4) Upungufu wa Wahandisi hasa waliosajiliwa na Mafundi Mchundo kwa ajili ya kusimamia kazi za matengenezo na ujenzi kikamilifu.

(5) Ukosefu wa Wakandarasi wenye uwezo na vifaa vya kazi katika Halmashauri hasa zile za pembezoni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Kuwa Serikali ichukue hatua ya kutatua changamoto zilizotajwa ili Mfuko wa barabara wa Serikali za Mitaa uweze kuendeshwa kwa mafanikio na ufanisi mkubwa ili kuwaletea wananchi walio wengi maendeleo kwa kuboresha miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yanayohitaji kuangaliwa na Serikali, ni migororo ya ardhi. Tatizo hili katika nchi yetu linazidi kukua kila siku kiasi kwamba sasa hivi kila kona ya nchi yetu matatizo ya umiliki wa ardhi yamekuwa yakiripotiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili lilijitokeza pia wakati Kamati ikiwa katika ziara ya kukagua Miradi ya maendeleo katika Jiji la Arusha ambapo malalamiko ya Wananchi na viongozi wa Mkoa wa Arusha na Wawakilishi wa wananchi katika Mkoa huo wa Arusha. Kutokana na malalamiko hayo Kamati iliamua kutembelea maeneo yanayolalamikiwa na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

kubaini kuwepo kwa tatizo kubwa la migogoro ya ardhi iliyosababishwa na watumishi wasio waadilifu na waminifu kugawa na kumilikisha maeneo ya wazi na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kijamii kama vile michezo, maeneo ya Hospitali na masoko.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyobainika kuwa na mgogoro mkubwa ni eneo lilikuwa dampo Njiro ambalo kwa sasa linatambulika kama "Kitalu 'E' Njiro Arusha", Kitalu hicho kwa sasa kina viwanja 20 ambavyo ni Kiwanja Na. 471/1, hadi 471/20. Viwanja vyote hivyo kwa mujibu wa maelezo ya Afisa ardhi na Afisa Mipango Miji wa Jiji vimeshamilikishwa na taarifa hizo zilithibishwa na Msajili wa Hati Kanda ya Kaskazini kwa kuwasilisha nakala za hati za umiliki kwa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yenye mgogoro ni kiwanja Na. 632, Kitalu 'HH', Themis Arusha, kiwanja Na. 68, Kitalu 'W' eneo 'F' Arusha, Kiwanja Na. 40, Kitalu 'A,' *Bruka Estate*, Arusha, na Kiwanja Na. 523, Kitalu 'D,' Njiro Arusha.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kutembelea maeneo hayo yenye mgogoro na ilibaini ukiukwaji wa wazi wa taratibu za umilikishwaji wa ardhi katika maeneo hayo na iligundua kuwa upo uwezekano mkubwa kwamba maeneo yenye mgogoro yote yanamilikiwa aidha na watumishi ambao waliwahi kufanya Kazi katika Halmashauri ya Jiji ambao baadhi yao inasemekana walishaacha kazi kwa kutoa notisi ya masaa 24 kwa Waajiri wao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ikiwa katika ziara za kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na Halmashauri ya Jiji la Arusha ilibaini uwepo wa migogoro ya kiutawala katika Mamlaka hizo baina ya viongozi wa kisiasa (Mameya) na Watendaji Wakuu (Wakurugenzi).

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwahoji wahusika wa migogoro ya kiutawala katika Halmashauri hizi mbili, Kamati ilibaini kuwepo kwa tatizo la kuingiliana katika utekelezaji wa majukumu ya Kazi. Kwa mfano, katika Halmashauri zote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

ilionekana kuwa matatizo haya huanza tu pale ambapo Mkurugenzi au Mtendaji Mkuu anapoonekana kupinga/kutotekeleza baadhi ya matakwa ya Viongozi wa kisiasa (Mameya) kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwepo wa migogoro hiyo Kamati iliilagiza Serikali kupitia kwa Waziri wa nchi - TAMISEMI kutafuta ufumbuzi wa haraka wa migogoro ya kiutawala katika Halmashauri hizo na Halmashauri zote nchini na kuwasilisha taarifa ya utekeleji wa agizo hilo mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia uzoefu ilioupata katika Halmashauri hizi mbili, Kamati inachukua fursa hii kuwaasa Viongozi wote wa kisiasa na Watendaji Wakuu (Wakurugenzi) kote nchini kuzingatia misingi ya Utawala Bora kwa kufuata kanuni na taratibu za kazi zao. Aidha, Kamati inashauri viongozi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya kazi ya kuwatumikia Wananchi kwa kuheshimu mipaka yao ya kazi na kwa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (*DART*) Kamati iliamua kutembelea na kukagua ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo haraka unaoendelea mpaka katika Barabara ya Morogoro kuanzia Kimara mpaka Kivukoni kwa lengo la kujionea hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa lengo kuu la mradi huu ni kuongeza tija na ufanisi katika kuchochea kasi ya maendeleo katika Jiji la Dar es Salaam na Taifa zima kwa ujumla hasa ikizingatiwa kwamba zaidi ya 80% ya pato la ndani la taifa linachangiwa na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unaogharamiwa na fedha toka Benki ya Dunia (Dola za kimarekani 325.37 milioni, Serikali ya Tanzania inachangia Shilingi bilioni 23.5 kwa ajili ya kugharimia ulipaji wa fidia kwa mali zilizoathiriwa na miundombinu ya mradi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Aidha, imeelezwa kuwa sekta binafsi inatarajiwa kuchangia Dola za Kimarekani milioni 100 kwa ajili ya kuwekeza kwenye ununuzi wa mabasi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Huku wadau wakuu wakitajwa kuwa ni Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Tume ya Mipango, *SUMATRA*, *TANROADS*, Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika Jiji la Dar es salaam, Benki ya Dunia na Chama cha Wamiliki wa Daladala *DARCOBOA*).

Mheshimiwa Spika, licha ya hatua nzuri iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu changamoto mbalimbali ziliweza kujitokeza katika utekelezaji wake ambazo ni:-

(1) Kasi ndogo ya ujenzi wa mradi;

(2) Tatizo la wafanyabiashara kuvamia maeneo ya ujenzi wa mradi huu katika eneo la Mansese, Magomeni na Ubungo. Wafanyabiashara hawa wanasababisha usumbufu kwa mkandarasi wakati wa kupitisha mitambo yake. Aidha, wafanyabiashara hao wanaharibu miundombinu ambayo imekwishajengwa kabla ya kuanza kutumika rasmi;

(3) Tatizo la wamiliki wa mahoteli pembezoni mwa barabara kutiririsha maji taka kwenye mitaro ya barabara za mradi huu kinyume cha sheria; na

(4) Kituo cha kivukoni kimejengwa bila kuzingatia viwango vilivyowekwa kwenye mkataba.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea taarifa ya pamoja ya uendeshaji wa Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam tarehe 16 Agosti, 2013 na 1 Septemba, 2013. Baada ya kuwasikiliza wadau wote wa Shirika la *UDA* Kamati ilibaini kuwa kwa hatua ilipofikia sasa hakuna namna yeyote Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

inaweza kulikomboa Shirika hilo kutokana na ukweli kwamba Shirika hili liliuzwa kwa kufuata Sheria zote na taratibu za uendeshaji wa Makampuni ambapo kupitia Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hisa zisizogawiwa (*un allotted shares*) ziliuzwa kwa Kampuni ya *Simon Group*. Kinachosikisha hapa ni kwamba hisa hizo ziliuzwa kwa bei ya kutupwa mithili ya mali isiyokuwa na mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupitia taarifa ya pamoja iliyowasilishwa mbele ya Kamati, ilielezwa Kampuni ya *Simon Group* iliuziwa hisa zisizogawiwa kwa bei ya Shilingi 145 tu kwa kila hisa moja wakati uthamini uliofanywa kupitia Kamani ya Ushauri ya *KPMG* ulionyesha kuwa thamani halisi ya hisa moja ni kati ya 1618 kama shirika litauzwa na madeni yake na 2632 kama Shirika litauzwa bila madeni. Hivyo kupitia uthamini huu unaweza kuona ni jinsi gani watu waliohusika kuuza hisa za Shirika walivyokosa uzalendo.

Mheshimiwa Spika, watu waliohusika katika mchakato wa uuzwaji wa hisa (*un allotted shares*) za Shirika kwa Kampuni ya *Simon Group* ni dhahiri kabisa hawakuwa wazalendo na wala hawakujali maslahi mapana ya taifa. Hivyo, kutokana na ukweli na sababu hizo Kamati iliamua kukubaliana na uamuzi wa Serikali kupitia Msajiri wa Hazina na uamuzi wa Halmashauri ya Jiji wa kutaka kuuza hisa zao zote kwa mbia mwenzao Kampuni ya *Simon Group* ili wajiondoe katika umiliki wa Shirika baada ya kuzingatia taratibu mbalimbali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono uamuzi wa Serikali kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mchakato wa uuzwaji wa hisa zake na zile za Jiji unafanyika kisheria kwa kuingiza makubaliano yote kwenye mkataba kinyume na inavyosemekana sasa kuwa makubaliano hayo yapo kwenye hati ya makubaliano yaani *Memorandum of Understanding (MoU)* hiyo inatokana na ukweli kwamba kwa mujibu wa Sheria za Mikataba *MoU* sio mkataba hivyo mtu hawezi kutumia kushitaki wala kushitakiwa Mahakamani kwa kuvunja makubaliano yaliyomo kwenye hati ya makubaliano.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya uendeshaji wa Mradi wa *DCC Business Park* na baadaye iliamua kutembelea jengo hilo maarufu kama *Machinga Complex* ili kujionea hali halisi ya Wafanyabiashara wadogo waliopo katika jengo hilo. Aidha, Kamati ilitaka kujua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wanaofanya biashara katika jengo la *Machinga Complex*.

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilielezwa kuwa jengo la *DCC Business Park* lilijengwa na Shirika la Hifadhi ya Jamii *NSSF* kwa makubaliano ya mfumo wa Jenga na Kabidhi (*build and transfer*). Katika makubaliano hayo *NSSF* ilikubali kutoa mkopo na kusimamia ujenzi na baada ya kumaliza ujenzi ilikadhi jengo hilo kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wake na kurejesha mkopo wa bilioni 12.7 unaotakiwa kurejeshwa katika kipindi cha miaka 10 pamoja na riba ya asilimia 14.40 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ilielezwa kuwa katika upembuzi yakinifu mradi ulikadiriwa kuzalisha mapato kiasi cha bilioni 3.76 kwa mwaka. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali zilizoлезwa lengo hilo halijaweza kufikiwa mpaka sasa hivyo kusababisha ulipaji wa deni kuwa mgumu. Kwa mfano, mwaka wa fedha wa 2012/2013 *DCC Business Park* ilikisia kukusanya kiasi cha Shilingi milioni 949 lakini ni Shilingi milioni 306.5 ndizo zilizokusanywa, hii ikiwa ni sawa na asilimia 32.29 tu ya malengo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa na baada ya kujionea hali halisi katika jengo la *Machinga Complex* kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

(1) Udanganyifu katika upembuzi yakinifu ambapo ulibainisha kuwa jengo lina uwezo wa kupangishwa kwa wafanyabiashara 10,000 wakati uhalisia ni kwamba jengo lile lina uwezo wa kupangishwa kwa wafanyabiashara 4,206 tu. Hii imeleta athari za moja kwa moja kwenye mapato yaliyokusudiwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

(2) Kamati pia ilibaini kwamba mradi huu ulibuniwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama wamachinga na wafanyabiashara wenye ulemavu bila kuzingatia ukweli kwamba mazingira ya biashara kwa sasa ni soko huria. Hivyo ni vigumu kwa mradi huu kujikomesha kibiashara na kuweza kurudisha mkopo.

(3) Vilevile ilibainika kwamba miundombinu ya kuwezesha wateja kufika katika eneo la soko haikuzingatiwa wakati wa kubuni mradi. Kutokuwepo kwa Kituo cha Daladala, jengo kutokuwa na *lift*. Kutokuwepo kwa miundombinu hiyo kunasabisha wateja kushindwa kufika eneo la soko kwa urahisi.

(4) Kuruhusiwa kwa wafanyabiashara wengine wanaofanya biashara kama zinazopatikana katika jengo la *Machinga Complex* maeneo ya jirani kama vile soko la Mchikichini. Kuwepo kwa gereji bubu na *car wash* katika eneo la soko kunasababisha usumbufu kwa wateja hivyo kuwafanya wakose kuja katika soko.

(5) Ukosefu wa sehemu ya kutosha ya kuegesha magari ya wateja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa maoni na ushauri, maoni mahususi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma Kamati inatambua uamuzi wa Serikali wa kuongeza kiasi cha Shilingi bilioni moja, katika bajeti ya 2013/2014, kwenye mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Hata hivyo, kwakuwa lengo la Kamati ni kuona mradi huu unakamilika mapema iwezekanavyo, Kamati inaagiza mambo yafuatayo yafanyike:-

(i) Serikali kupeleka fedha zote zilizoidhinishwa kwenye bajeti kwa wakati; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

(ii) Serikali kutenga fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ikizingatiwa Mkoa wa Dodoma ni Makao Makuu ya nchi hivyo Mkuu wa Mkoa kukosa Ofisi nzuri na ya uhakika ni aibu kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua pia uamuzi Serikali wa kuongeza kiasi cha Shilingi bilioni mbili katika bajeti ya 2013/2014 kwenye Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Singida. Hata hivyo, kwa kuwa lengo la Kamati ni kuona mradi huu una kamilika haraka ili uweze kuanza kutoa huduma ya uhakika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa wa kutenga kiasi cha Shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa ajili ya mradi huu, utachukua zaidi ya miaka 70 mpaka kukamilika kwa mradi huu. Hivyo Kamati inaagiza kuchukua hatua za makusudi kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(1) Serikali itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutenga na kupeleka Shilingi bilioni nne kwa njia ya ombi maalumu ikiwa ni sehemu ya Shilingi bilioni 8.1 ambazo aliahidi wakati akiwa ziarani Mkoani Singida. Aidha, Serikali ihakikishe ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuharakisha upatikanaji wa Shilingi bilioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hii inatekelezwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaitaka Serikali kupeleka kiasi cha Shilingi milioni 700 ili kuwezesha majengo yaliyokamilika yaanze kutumika, Serikali inashauriwa isiogope kukopa kama inaweza kwenye miradi yenye faida kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaitaka Serikali katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kufanya ukaguzi maalumu (*special forensic audit*) ili kujiridhisha juu ya taratibu na gharama zilizotumika katika kujenga kibanda cha kuchomea taka.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Kamati inaishauri Serikali isiuachie Mkoa suala la ujenzi wa hospitali hii. Serikali ipeleke watumishi wa kutosha na kusaidia ujenzi wa nyumba za watumishi ili kwenda sambamba na ujenzi wa hospitali hii.

Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia Mfuko wa Bima ya Afya na wadau wengine, kwa ajili ya kupata mkopo utakaowezesha kukamilisha ujenzi wa Hospitali hii kwa haraka ili iweze kuwanufaisha Wananchi wa Singida na Mkoa wa jirani kama Tabora, Shinyanga, Dodoma na Manyara.

Kamati inaiagiza Serikali kujenga wodi za wagonjwa wa nje, jengo la kuhifadhia maiti, na majengo mengine ya lazima haraka ili hospitali hii ianze kutumika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, maoni kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Tumbi - Kibaha. Kamati inaona umuhimu wa Hospitali ya Tumbi kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani na Watanzania kwa ujumla na hivyo Kamati inaitaka Serikali kutekeleza mambo yafuatayo kwa haraka:-

Kamati inaitaka Serikali kutenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 2.2 kwa mwaka 2014/2015 kwa ajili ya kununulia vifaa tiba na kufanya marekebisho mbalimbali ili jengo ambalo limekwishakamilika liweze kuanza kutumika.

Aidha, Kamati inaitaka Serikali kutafuta na kutenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 17.5 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa awamu ya pili, ununuzi wa vifaa tiba na mafunzo kwa Madaktari na Wauguzi ndani ya miaka miwili ijayo.

Vilevile Kamati naikumbusha Serikali kutekeleza ahadi yake ya kutenga kiasi cha Shilingi bilioni 2.5 kila mwaka ili kukamilisha ujenzi wa hospitali ya Tumbi haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, baada ya kubaini ukiukwaji wa wazi wa ugawaji na umilikishwaji wa maeneo ya wazi na yale

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

yaliyotengwa kwa ajili ya huduma za jamii, Kamati imefikia uamuzi wa kuishauri Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

Kamati inaiagiza Halmashauri ya Jiji kutotoa vibali vya ujenzi wa aina yeyote katika viwanja vyenye mgogoro katika eneo la dampo kiwanja namba 471/1 hadi 471/20, Kitalu 'E' Njiro, Kiwanja Namba 523, Kitalu 'D' Njiro, Kiwanja namba 68, Kitalu 'W' Eneo 'F', kiwanja Na. 632 Kitalu 'HH', Themi, na Kiwanja Na. 40, Kitalu 'A', *Bruka Estate*.

Kamati inaagiza Serikali kupitia Mamlaka husika kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote waliohusika katika zoezi za ugawaji na umilikishwaji wa viwanja katika maeneo yote yenye mgogoro.

Kamati inaishauri Serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu uhalali wa umilikishwaji wa maeneo tajwa na endapo itaridhika kwamba umilikishwaji wake haukuwa halali basi Mheshimiwa Rais achukue hatua ya kuvitwaa viwanja hivyo ili vitumike kwa shughuli za kijamii kwa manufaa mapana ya umma.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto na upungufu uliyojitokeza wakati Kamati ilipotembelea mradi wa Mabasi yaendayo haraka *DART*, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- Mkandarasi aliyejenga kituo cha Kivukoni awajibishwe kwa kushindwa kujenga kituo kwa viwango vilivyokubaliwa kwenye mkataba.

- Serikali ifanye jitihada za kuwaondoa wafanyabiashara wanaofanya biashara katika eneo la Mradi ili Mkandarasi aweze kufanya kazi bila usumbufu.

- Serikali iwachukulie hatua wamiliki wa mahoteli wanaodaiwa kutiririsha maji taka kutoka kwenye mahoteli yao kwenda kwenye mitaro ya barabara zinazojengwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

- Serikali imbane Mkandarasi ili aweze kukamilisha ujenzi wa miundombinu kwa muda uliopangwa ili kupunguza adha ya msongamano wa magari uliopo sasa.

- Serikali iharakishe kulipa fidia kwa wananchi wanaodai fidia zao kupisha ujenzi wa miundombinu katika maeneo ya awamu zinazofuata ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi ya Mradi wa *DDC Business Park (Machinga Complex)*, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- Kamati inaagiza ujenzi wa kituo cha daladala katika eneo la soko ufanyike haraka ili kuwezesha wateja kufika katika soko.

- Kamati inaagiza Uongozi wa Jiji kuanzisha utaratibu wa Gulio siku ya Jumamosi na Jumapili ili kusaidia kuchangamsha na kuwavutia wateja kuja kwenda kwenye soko.

- Kamati inaelekeza huduma ya mabasi ipite katika jengo la *Machinga Complex* kama ilivyokuwa imeelekezwa awali na Mkuu wa Mkoa ili kuwezesha wateja kufika katika eneo la soko.

- Kamati inaagiza kuondolewa haraka kwa *car wash* iliyopo katika eneo jirani ili kuweza kuboresha mazingira ya soko.

- Serikali na *NSSF* wakamilishe utaratibu wa makabidhiano ili mapungufu yaliyopo katika jengo la soko kama vile kutokuwepo kwa lift na tatizo la kuingia kwa maji ndani ya jengo wakati wa mvua yaweze kuchukuliwa hatua ya kurekebishwa.

- Kamati inaagiza uchunguzi ufanyike ili kubaini kama kulikuwa na uzembe wakati wa kubuni mradi na kama mkandarasi aliyejenga soko alikiuka makubaliano yaliyomo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

kwenye Mkataba basi wachukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza.

- Kamati inaishauri Serikali kutazama uwezekana wa kutoa msamaha wa *VAT (exemption)* ili kupunguza mzigo wa deni.

- Kamati inashauri Serikali iunde timu ya wataalamu ya ushauri ili ifanye uchunguzi wa kina wa namna ya kuboresha soko la *Machinga Complex* na aina ya biashara inayofaa kufanyika katika jengo la *Machinga Complex*.

- Kamati inashauri kwamba, ubunifu (*designing*) wa miradi mingine kama huu lazima uzingatie mahitaji ya wafanyabiashara wenyewe ili iweze kufanikiwa.

- Kwakuwa deni la *Machinga Complex* ni kubwa na linaendelea kuongezeka hivyo Kamati inaishauri Serikali kulichukua deni hilo la *Machinga Complex* ili kuepusha madhara ya kukua kwa deni kwakuwa imeonyesha dhahiri kwamba mradi huu haujiendeshi kibiashara hivyo kulifanya Jiji la Dar es Salaam kushindwa kulipa deni hilo ikizingatiwa kwamba wadau wote wa mradi huu ni mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa ukusanyaji kodi za majengo. Kwa kuwa muda wa kisheria uliotolewa kwa Mamlaka ya Mapato kukusanya kodi za Majengo kwa niba ya Halmashauri kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Fedha (*The Financial Laws Miscellaneous Amendments Act, 2008*). Aidha, kwakuwa *TRA* baada ya muda waliopewa kisheria kuisha hakuna tena mwongozo wowote wala Sheria inayoelekeza vinginevyo kuhusu ukusanyaji wa kodi ya majengo katika Halmashauri zetu, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- Kuzifanyia marekebisho Sheria zifuatazo ili kuzirejeshea Halmashauri za Serikali za Mitaa Mamlaka yake ya kukusanya kodi za Majengo ikizingatiwa kuwa Halmashauri hizo zimeshajengewa uwezo wa kutosha katika kukusanya kodi hiyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

- (a) Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (*The Tanzania Revenue Authority Act, (CAP 399)*);
- (b) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (*The Local Government Finance Act, (CAP 290)*); na
- (c) Sheria ya tozo za kodi ya Majengo (*The Urban Authorities Rating) Act, (CAP 289)*).

Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha *Property Tax Rating Tribunal* Kisheria ili liweze kutumika kutatua malamiko na migogoro inahusiana na kodi za majengo.

Serikali kupitia kwa Waziri husika iharakishe mchakato wa kupisha kanuni za kutoza kodi za majengo. Kamati inashauri Serikali kupitia Halmashauri kurekebisha jedwali la kodi za majengo kwa kufanya uthamini upya wa majengo ya zamani na uthamini wa majengo mapya ili yaingizwe kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya jumla, Kamati inaigiza Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kutenga fedha za kutosha katika miradi ya ujenzi wa miundombinu hususan majengo ya utawala katika Mikoa na Wilaya zote mpya ili iweze kukamilika mapema.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaiagiza Serikali kupeleka fedha kwenye Halmashauri zote nchini hususan fedha za miradi ya maendeleo Kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili miradi iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kuhakikisha zinafuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa mujibu wa mikataba ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inaonekana katika miradi hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia upya Sheria ya Mfuko wa barabara ili kuweka uwiano sawa wa mgao wa fedha za barabara kwa barabara za Halmashauri na barabara za *TANROADS* ambapo kwa sasa uwiano ni asilimia 70 kwa barabara za *TANROADS* na asilimia 30 kwa barabara za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinashauriwa kutotegemea sana fedha za Wahisani na Ruzuku kwani uzoefu unaonyesha fedha hizo hufika ama kwa kuchelewa ama kutofika kabisa. Hivyo, Kamati inazishauri Halmashauri zote nchini kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kujiongezea mapato ya ndani yatakayotumika kutekeleza miradi mingi zaidi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inatoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inayotumika katika miradi ya maendeleo inaonekana katika Miradi husika. Hakika Kamati haitasita kuzichukulia hatua Halmashauri zikazokiuka misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inachukua nafasi hiii kuziagiza Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini kuiga mfano wa Manispaa ya Moshi ili kuweka madhari ya Miji yetu katika hali ya kuvutia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ilibaini utaratibu ambao Halmashauri inautumia wa kupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwenye Ofisi za Watendaji wa Kata kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasaidia kuondoa urasimu wa ulipaji wa malipo kwa mkandarasi. Inawezakana kabisa utaratibu huu ukawa na nia njema.

Hata hivyo, Kamati inaona kwamba utaratibu huu unaweza kutumika vibaya na Wajanja wachache kwa kuwa usimamizi wake haujawekewa taratibu za Kisheria. Hivyo Kamati inashauri utaratibu huu usitumike ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Wananchi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kufanya jitihada za makusudi ili kukaa meza moja ya mazungumzo na Waalimu ili kutatua matatizo yanayowakabili Waalimu na Sekta ya Elimu kwa ujumla ikiwa ni sehemu ya kutatua tatizo la kupromoka kwa kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaitaka Serikali kufanyia kazi malalamiko ya kila mara ya Waheshimiwa Wabunge dhidi ya watendaji wa Halmashauri mbalimbali kwa kuwa inaonyesha wazi kuwa kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha na mali za umma. Kwa lugha nyepesi watendaji hawa wanafanya vitendo vya kifisadi wamekuwa mchwa wa kutafuna fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Naibu Mawaziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Ndugu Jumanne A. Sagini, Katibu Mkuu, Ndugu Deo Mtasiwa Naibu Katibu Mkuu (Afya), Ndugu Zuberi Samataba Naibu Katibu Mkuu (Elimu) na Ndugu Kagyamkama Kiliba Naibu Katibu Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge pindi walipohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kumshukuru Mheshimiwa John Paul Lwanji (Mb) Makamu Mwenyekiti, kwa msaada anaonipa kuiongoza Kamati wakati ninapokuwa natekeleza majukumu mengine ya kitaifa. Kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa kamati waliotajwa hapo juu kwa namna ambavyo wamekuwa wakinipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya kamati. Aidha, nawashukuru kwa kuweza kutoa maoni na michango yao katika kuandaa taarifa hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. J. LWANJI – MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah na Katibu wa Kamati Ndg. Mossy Lukuvi kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, ninaomba *speech* yangu yote iingie katika *Hansard*. Nashukuru kwa kunipa nafasi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante kwa uwasilishaji.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji ni wengi, hizi ni Wizara mbili na zote zinatakiwa tumalize kuziadili leo. Kwa hiyo, hivi sasa mpaka saa 7.00 naweza kupata watu watano tu. Labda tutashauriana baadaye hata muda wa wanaojibu hoja, sijui kama itategemea namna wanavyoongea. Tukiwapa hawa saa moja ya kujibu maana yake inakula kwa wachangiaji pia. Sasa tuanze. Tutakaoanza sasa hivi ni Mheshimiwa Ntukamazima, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Godbless Lema na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis. Hawa wanatosha kwa asubuhi hii. Mheshimiwa Ntukamazina.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie katika taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Nitakachofanya, ni kujaribu kuboresha taarifa yetu na hasa kueleza ushauri ambao tuliutoa kwenye Wizara zinazohusika pamoja na Idara tunazozisimamia.

Nianze na Ofisi ya Rais Ikulu. Ofisi ya Rais Ikulu tulipokutana na viongozi wa Ikulu tuliwaambia kwamba Ofisi hii ndiyo Ofisi Kuu ya nchi nzima na mnatakiwa kuwe na *helicopter view* ya Ofisi nyingine zote katika nchi nzima. Sasa kwa sababu nyinyi ndio Ofisi Kuu, mnatakiwa waajiriwa wa Ofisi hiyo ya Rais wawe *the best and the brightest* na *best* katika uwezo lakini pia *best* katika *competence and character*. Nikasema muige mfano wa John F. Kennedy mwaka 1960 alipoingia madarakani aliteua *the best and the brightest* kwenye *Cabinet* pamoja na kwenye Ikulu ya Marekani. Kwa hiyo, tukasema, kwa kweli lazima watu wenu wawe ni *people of the highest integrity*. Katika Ofisi ya Ikulu haitakiwi kuwepo na rushwa, hakutakiwi kuwepo na ucheleweshaji wa maamuzi. Inatakiwa iwe ni Ofisi ya Rufani yenye uwezo wa kusimamia Ofisi zote za nchi hii. Kwa sababu *Chief Secretary* ambaye ni *Head of Public Service* yuko kule. Kwa hiyo, tulijaribu kuwashauri sana Ofisi ya Rais kuhakikisha kwamba wanafanya kazi yao.

Sasa Mheshimiwa Spika, katika Ofisi hii pia ndiyo kuna *Presidential Delivery Bureau* ambayo inasimia *the Big Results Now*. Sasa hapa napenda niwashauri Wabunge wenzangu, kwamba *Big Results Now* imeanza juzi tu, na Rais ameziweka nadhani Wizara sita kwenye *Big Results Now* na Mawaziri wamewekwa kwenye *performance contracts*. Rais ndiye anawateua Mawaziri na Watendaji Wakuu na ndiye amewaweka kwenye *contracts* hizo kuona kama wata-*delivery under Big Results Now*.

Sasa tumpe Rais muda wa kutosha kuwapima Mawaziri hao wa Kilimo, wa Maji, wa TAMISEMI na kadhalika. Tusianze kupiga kelele kwamba waondolewe. Ni muda mfupi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. A. NTUKAMAZINA]

wamepewa. Mimi nashauri kama *senior citizen* kwamba tuwape nafasi.

Jambo lingine ambalo tulieleza kule Ikulu ni kwamba msiogope kumshauri Mheshimiwa Rais katika uteuzi kwa sababu Rais sio Mungu. Rais ni binadamu ambaye ana upungufu wake. Lakini nyinyi kama *system* yake mnatakiwa mumshauri ateue watu kutokana na sifa, siyo mambo ya ukabila, siyo mambo ya udini, siyo mambo ya urafiki. Tukasema nyinyi ni vyombo vya Rais, kwa hiyo, lazima mfanye kazi hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba Ofisi ya Mipango imeanza kazi yake vizuri kama *think tank*. Lakini tukiwapa kazi ya kusimamia mipango huko Mikoani, lazima tuiwezeshe tuwape wataalam zaidi. Tume ya Mipango imeanza kazi vizuri sana. Taasisi za *TASAF* pamoja na MKURABITA ni za kumkomboa Mtanzania wa kawaida. Naomba tuzisaidie kuziongezea bajeti ziweze kufanya kazi vizuri. Kwa mfano, *TASAF* ya tatu, kazi yake inataka kuinua hali za kaya masikini sana na wanafanya kazi nzuri na wana *Chief Executive* mzuri. Naomba tuisaidie Taasisi za *TASAF* pamoja na MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, hapa hapa naomba kama *senior citizen* niwashauri Wabunge wenzangu, wanasiasa. Wakristo wanaosoma, Biblia Zaburi ya 141 mstari wa tatu; Mfalme Daudi alimwomba Mwenyezi Mungu ampe mlinzi wa mdomo wake asianze kutoa mambo ambayo hayatakiwi kwenye mdomo. (*Makofi*)

Sasa sisi tukiwa hapa tunaangaliwa na nchi nzima, tunaanza sisi wenyewe kudhalilishana. Mimi kama *senior citizen* inaniumiza sana. Tuchunge midomo yetu. Tumwombe Mwenyezi Mungu aweke mlinzi kwenye midomo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nianze kwa kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Celina Kombani kwa kuendeleza *Reforms*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. A. NTUKAMAZINA]

ambazo tulianzisha miaka ya 1990. Uboreshaji wa utendaji kazi wa Serikali. Amefanya kazi vizuri katika *TEHAMA*. Amejariibu kudhibiti watumishi hewa katika *Payroll* ya Serikali. Lakini tulipokuwa tunazungumza naye, tulimweleza kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo bado hawajafanya vizuri. Kwa mfano, bado watumishi hawajabadilika mtazamo; kuwa na mtazamo chanya, yaani *change of mind set*, bado wanakwamisha huduma mbalimbali zinazotolewa.

Kwa hiyo, tukasema ni vizuri kuhakikisha kwamba hawa watumishi wanabadilika *mind set* na wajue kwamba Serikali iko kwenye ubia pamoja na Sekta Binafsi. Kwa hiyo, wasikwamishe maendeleo watumishi wenyewe. Wawe na mtazamo chanya, wawe *aggressive and proactive*, wawe na mtazamo wa kijasiriamali. Vile vile tukasema pia bado *OPRAS* haija-*role out* kwenda nchi nzima. *Open Performance Review and Appraisal System (OPRAS)* ni mpango mzuri sana. Unawaweka watumishi kwenye mkataba. Ukiwaweka watumishi kwenye mkataba ukawapa malengo yanayojulikana, inaimarisha uwajibikaji. Kwa hiyo, tulimshauri Mheshimiwa Kombani ahakikishe kwamba *OPRAS* inatekelezwa katika sehemu mbalimbali.

Pia Menejimenti ya Utumishi wa Umma wamekasimu madaraka ya kuteua Wakurugenzi, na Wakurugenzi Wasaidizi pamoja na watumishi wengine kwenye Wizara mbalimbali. Hizi Wizara hazina taaluma ya *Human Resource Management*. Kwa hiyo, *as result* unakuta kuna watu wanakaimu wengi sana, watu hawajathibitishwa kazini kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tumeishauri Utumishi wahakikishe kwamba wanafuatilia utekelezaji wa madaraka ambayo waliyakasimu kwenye Wizara mbalimbali. *They should not delegate with abdication*. Hiyo ndiyo tuliwashauri.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye Sekretarieti ya Ajira. Imeanzishwa Sekretarieti ya Ajira ambalo ni jambo zuri sana kuhakikisha kwamba ajira ni kwa nchi nzima. Lakini ajira inafuata sifa. Lakini tumeiomba Sekretarieti ya Ajira iziruhusu Halmashauri ziendeele kuajiri watumishi wa chini, yaani *Operational Service*, kama Madereva na Makarani. Hawa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. A. NTUKAMAZINA]

hawawezi kuajiriwa kutoka Dar es Salaam. Lakini pia tumeishauri Sekretarieti iache Vyuo Vikuu viendeleo kuajiri wataalam wake kusudi kuhakikisha kwamba wana-*maintain standards*.

Mheshimiwa Spika, wakati tunazungumza na Mheshimiwa Kombani na Uongozi wake tulisema kuna Mashirika ya Umma ambayo yanaajiri bila kuzingatia msingi wa sifa. Wanaajiri kwa ukabila, kwa udini na tukatoa mfano, kwamba kuna Shirika la Umma moja mwaka juzi liliajiri vijana 100, kati ya vijana 100 vijana 96 walikuwa ni wa dini ya Mtendaji Mkuu wa Shirika hilo. Sisi hatuwezi kukubali kuendeleza ubaguzi wa dini namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Wizara ya Sheria. Wizara ya Sheria inafanya kazi nzuri sana, lakini wana tatizo la bajeti na hasa kwenye Mahakama. Mahakama ni chombo muhimu sana cha kutoa haki. Wameanza utaratibu mzuri wa kupeleka vijana, *young graduates* kwenye Vijiji, katika Mahakama za Mwanzo. Sasa tunaiomba Serikali iongeze bajeti iboreshe mazingira ya hao vijana waweze kufanya kazi vizuri, wawape nyumba na usafiri.

Mheshimiwa Spika, safari za nje, tunakushukuru sana kwa kuruhusu Kamati ya Katiba na Sheria kutembelea hizi nchi ambazo zimepitia kwenye mchakato wa Katiba wa kuandika katiba. Nadhani taarifa yetu tumeeleza lakini ninachoweza kusema ni kwamba Zimbabwe wao Bunge la kawaida lilijigeuza kuwa Bunge la Katiba. Hawakuleta Waswahili kutoka nje. Halafu Ghana tulichoijifunza, hii Kamati ya Katiba na Sheria lazima itoe *input* kwenye Miswada ya Kisekta.

Kenya wakati sisi tumefanya vizuri sana kwenye *Decentralization by Devolution D by D* wao bado wana mvutano mkubwa sana. Watendaji wa Serikali Kuu hawataki kuachia baadhi ya *functions* ziende kwenye *counties*. Sasa tumejifunza mambo mengi, nadhani yatatusaidia tutakapokuja kwenye mchakato wa Bunge la Katiba.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. A. NTUKAMAZINA]

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo ya kuongezea kwenye Kamati yetu. Nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Nilimesema atakayefuata ni Mheshimiwa Zitto halafu Mheshimiwa Mabumba atafuatia. *(Makofi)*

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nami napenda kushukuru kupata fursa ya kuchangia katika taarifa ya Kamati zetu mbili. Nitajikita zaidi kwenye Kamati ya Katiba na Sheria, nikipata muda nitagusia kidogo tu kwenye Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza nilikuwa naomba utusaidie suala la Kanuni kwa sababu Kanuni ya 123 kuhusu muundo wa Taarifa za Kamati, imeelekeza namna gani ambavyo Kamati zinapaswa kuandika taarifa zake na kifungu (c) cha Kanuni hiyo kinazungumzia maoni na mapendekezo, ili jioni tunapokuja kupitisha hapa, tunakuwa tunajua ni maoni gani na mapendekezo gani ambayo tunataka Bunge lipitishwe kwa ajili ya utekelezaji.

Ukisoma taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, utapata taabu sana kupata maoni na mapendekezo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo hili liweze kuangaliwa kama ni tatizo la Kamati au ni tatizo la waandishi wa taarifa kwa maana ya Makatibu, liweze kutambulika kwa sababu nimejaribu kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukafanya marekebisho kwenye maoni na mapendekezo, nimeshindwa. Kwa sababu kuna mapendekezo ambayo nilikuwa nataka nipendekeze hapa kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, la pili Kamati hii ndiyo ambayo inasimamia Tume ya Taifa ya Uchaguzi *NEC*, Fungu Na. 61 na umeleza kwamba katika mwaka huu wameshughulikia masuala ya bajeti ya *NEC*. Kuna tatizo kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inafahamika kwamba sasa hivi tupo kwenye mchakato wa kuwa na mfumo mpya wa kupiga

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. K. Z. ZITTO]

kura, wanaita *Bio-Metric Voter Register* ambayo ni ya kisasa kabisa na imeanza kutumia katika sehemu mbalimbali.

Mwanzoni mwa mwaka huu mpaka katikati ya huu kulikuwa na mchakato na wa kununua mtambo na mfumo wa kuweza kupata hii *Biometric Voters Register* lakini bahati mbaya sana mchakato huu ukawa umeingiliwa na matatizo ya kiutaratibu ambayo inawezekana kabisa kwamba pia yakawa ni matatizo ya rushwa na ubadhirifu kwa sababu ni mradi mkubwa sana wa fedha nyingi sana, zaidi ya Shilingi bilioni 126, mwezi Agosti, 2013 na Tume ikawa imetoa zabuni kwa kampuni hiyo. Lakini baadaye kukawa kuna malalamiko, na moja ya malalamiko yalikuwa ni kwamba kampuni iliyopewa kazi hiyo ya kutengeneza hiyo *Biometric Voters Register* ndiyo Kampuni ambayo iliandaa *Tender Documents*.

Kwa hiyo, iliandaa *Tender Documents* halafu ikaenda kwenye Tenda ikashinda Tenda hiyo. Nikiwa kama Mbunge, niliandika barua kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na *PPRA* kwa ajili ya kullitazama jambo hili. Nashukuru juzi *PPA*, ile Kamati ya Rufaa ya *PPRA* imeifuta tenda ile na kuagiza itangazwe upya kwenye kesi namba 20 ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo tunapaswa kujuliza hapa ni kwamba, mfumo ambao ulikuwa utumike katika *Biometric Voters Register* tunataka kununua ndiyo mfumo huo huo ambao ulitumika Malawi ukaleta matatizo na leo tunavyozungumza, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Malawi yuko Gerezani. Kwa mfumo huu huu, ndiyo ambao ulitumika Kenya na kuleta matatizo na mwezi uliopita Mtendaji Mkuu wa Tume ya Taifa ya Kenya amekamatwa. Tunataka kujua ni nini ambacho kinaendelea? Bahati nzuri Waziri anayehusika na Tume ya Uchaguzi ya Taifa yuko hapa Mheshimiwa Lukuvi. Ni nini ambacho kinaendelea? Kwa sababu hatuwezi kuishia kuondoa zabuni na kuitangaza upya bila kuchukua hatua za kiuwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, fedha ni nyingi sana. Kampuni ambayo ilipewa zabuni hii yenyewe na iliyoshinda iliyokuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. K. Z. ZITTO]

na gharama ndogo zinapishana Shilingi bilioni 20 kwa ubora tofauti na kwa kiwango kidogo cha fedha. Nini ambacho kinatokea miaka miwili kabla ya uchaguzi? Kwa bahati mbaya sana, naomba radhi, lakini ndiyo bahati mbaya sana, Waziri anahusika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ningependa Serikali iweze kutoa taarifa hapa ndani ya Bunge kwamba ni nini ambacho kimetokea Tume ya Taifa ya Uchaguzi? Taarifa ije hapa! Ndiyo moja ya pendekezo ambalo nataka Kamati iweze kulichukua, Mheshimiwa Blandes kwamba lije tulifanyie azimio ili Waziri anayehusika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi atoe kauli hapa Bungeni ni nini kilitokea na hatua gani zimechukuliwa kwa sababu tunajua mfumo uliotumika, umetumika Malawi umeleta matatizo; umetumika Kenya umeleta matatizo na Ghana, Tume ilikwenda huko juzi ilikuta ndiyo kesi imekwisha ya uchaguzi wa Ghana; kulikuwa na tatizo la *Biometric Voters Register* ni nini ambacho kinatokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba kwamba Waziri anayehusika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi awajibike katika hili. Siyo kuwajibika kwa maana ya kuondoka, kuwajibika kwa maana ya kuleta maelezo kwenye Bunge, yajadiliwe kabla ya Mkutano huu wa Bunge kwisha na Wabunge waweze kuona hasa ni nini ambacho kinatokea.

Mheshimiwa Spika, la pili, mambo ya uchaguzi ni *sensitive*, ni mambo ambayo yana wadau wengi. Ili kuweza kuondoa matatizo na minong'ono na kadhalika ni vizuri katika mchakato wa zabuni wa chombo kama hiki wadau hasa vyama vya siasa wahusishwe. Kwa mfano, hatusemi waingie kwenye tenda, wanaweza wakahusika katika kipindi cha *evaluation* ili kila mtu ajiridhishe. Kwa sababu uchaguzi ni *trusts*, watu wajiridhishe twende tupate mtu ambaye anaweza akatupa mfumo ambao unaweza ukasaidia nchi. Kwa hiyo, hilo ndilo pendekezo la pili ambalo nalipendekeza kwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwamba mchakato utakapotangazwa upya, uhusishe wadau wa uchaguzi ambao ni Vyama vya Siasa ili kuweza kujenga *trust*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. K. Z. ZITTO]

katika nchi tuwe na mfumo wa uchaguzi, hiyo *Biometric Voters Register* ambayo itaweza kutufanya tuwewe kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka kulizungumza Kamati hii, natambua kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inahusika, inaenda na kupeleka masuala yake na utendaji wake katika Kamati ya Katiba na Sheria. Jana nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu akielezea kuhusu kuomba muda zaidi kwa ajili ya kuweza kupata taarifa kuhusiana na uchunguzi ambao sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unafanya kuhusiana na watu ambao wametorosha fedha nje.

Mheshimiwa Spika, tatizo siyo Sheria za Kimataifa, tatizo ni *willingness* ya Serikali yetu kulfanya jambo hili liishe. Kwasababu tayari sasa hivi kuna kampeni ya Kimataifa ya kutaka kudhibiti utoroshaji wa fedha, na kampeni hii tayari kuna *conventions* mbalimbali ambazo zimesainiwa. Kuna *conventions* kwa ajili ya kupashana taarifa. Afrika zimesaini nchi tatu tu; Ghana, Afrika Kusini na Nigeria. Tanzania bado hatujasaini. Utapataje Taarifa haujasaini *conventions* kama hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *topic* sasa ni mabilioni ya Uswiss. Ni zaidi ya mabilioni ya Uswiss! Uswiss kuna bilioni 319, Geese Kisiwa kimoja Uingereza kina zaidi ya trilioni moja za Watanzania. Mkikaa mtjadili, na Watanzania wanapenda vitu vyepesi vyepesi, watakwambia taja majina! Taja majina! Haitasaidia kwasababu suala zima hapa ni la mfumo.

Kwa hiyo, tunahitaji Serikali iweze kueleza ni namna gani ambavyo itafanya kuingia mashirikiano haya ya Kimataifa, tuweze kupata taarifa ili tuweze kuziba myanya ya utoroshaji wa fedha. Hatuoni! Ndiyo maana hatuoni *impact* yake, lakini asilimia tano ya pato la Taifa Tanzania linapotea kwenye utoroshaji. Wanaotorosha sio watu *individual* tu peke yake, Makampuni makubwa yanashiriki katika utoroshaji. Tunahitaji nguzu ya Serikali katika jambo hili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. K. Z. ZITTO]

Mheshimiwa Spika, suala la Mnadhimu Mkuu wa Serikali kuomba muda zaidi lakini watoe na maelezo. Kwasababu walikuwa watoe taarifa hii mwezi Aprili, 2013, hawajatoa; Bunge la Bajeti tulibadilisha mfumo. Bunge lililofuata hawajatoa. Sasa hivi, hawataki kutoa. Kwa hiyo, watakapoomba muda wa kuongezewa kwa ajili ya jambo hili waombe na waeleze kwanini wamechelewa na kwanini Serikali yetu haijaingia kwenye *conventions* hizi za Kimataifa kwa ajili ya kupashana taarifa ili ziweze kutusaidia. Tunaelewa kwamba suala hili ni mchakato hatuwezi kulimaliza mara moja. Lakini tuanze basi hatua ambazo zinaweza kutusaidia ili kuweza kuiokoa nchi hii kuondokana na tatizo kama hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa kulichangia katika Kamati hii, ni suala la Kamati ya Katiba na Sheria. Tumeambiwa kwamba Kamati ilikwenda Ghana na wameeleza mambo mengi ambayo Kamati imejifunza Ghana. Lakini hawakutuambia kwamba moja ya jambo ambalo walijifunza Ghana ni *Artical 162* ya Katiba ya Ghana ambayo inatoa uhuru wa habari kwenye Katiba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. KABWE Z. ZITTO: Ni kengele ya pili au ya kwanza?

MBUNGE FULANI: Ya kwanza.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kwenye Katiba ya Ghana *Artical 162* inatoa uhuru wa habari. Kwanza Katiba ya Ghana imesema dhahiri kabisa kwamba hakuna *censorship* Ghana. Kwa hiyo, mambo ya kuwa sijui na maelezo ya akina Hassan Mwambene na kadhalika na nini, hakuna. Jambo hili mbona hamjaliweka kwenye ripoti ya Kamati kwamba *no censorship?*

Ghana ukitaka kuanzisha chombo cha habari, hakuna kuomba leseni. Imo ndani ya Katiba ya Ghana. Ndiyo! Naomba nisaidie Katiba ya Ghana Mheshimiwa Lissu. Hiyo hapo!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Endelea kujadili, usisikilize maneno ya watu.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, wametuletea taarifa ya safari ambazo wamezifanya. Kwa hiyo, nataka tuone tunajifunzaje? Maana Ghana ni Afrika hii. Siyo Marekani, siyo Uingereza, ni nchi ya Kiafrika ambayo tunaweza tukajifunza. Kifungu cha 162 (3) kinasema: "*There shall be no impediments to the establishment of private press or media; and in particular, there shall be no law requiring any person to obtain a licence as a prerequisite to the establishment or operation of a newspaper, journal or other media for mass communication or information.*" Ndani ya *Constitution*, wala siyo sheria! Sasa hapa kwetu...

MBUNGE FULANI: Ni ya Ghana?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Ndiyo, ni Ghana! Ni Afrika! Tuna mambo mengi ya kujifunza. Mheshimiwa Mwenyekiti naomba mweke hii mliyojifunza Ghana ije hapa tuazimie Serikali ikatutengenezee, hata kwenye Katiba mpya tutakapokuja kwenye Bunge la Katiba, tuweze kuweka uhuru huu ili wananchi waweze kuwa na uhuru wa habari, uhuru wa mawazo na kuweza kuhakikisha kwamba mambo ya Waziri kuamka na kufungia gazeti na kadhalika yanakwisha ili tuweze kuwa na *freedom* ya kweli Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, umemaliza? (*Kicheko*)

Sasa namwita Mheshimiwa Mabumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Taarifa za Kamati hizi mbili, lakini nitajikita zaidi kwenye Kamati ya TAMISEMI ambayo mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. M. MABUMBA]

Taarifa ya Kamati ya TAMISEMI imeeleza mambo mengi, lakini napenda niboreshe yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye ziara za Kamati tulipotembelea Mradi wa Mabasi yaendayo kwa haraka Jijini Dar es Salaam, wengi hapa wameonesha shauku yao katika mradi huu, na hata wengine kutoa hata takwimu kwamba usafiri Dar es Salaam unasababisha Serikali kupoteza mapato yake kwasababu wananchi wanatumia muda mwingi, lakini siyo Dar es Salaam peke yake, nadhani hata Miji mikubwa ya Mwanza, Arusha, Mbeya na Tanga.

Mheshimiwa Spika, ili mradi huu na katika maeneo haya ambayo nimeyataja, uweze kuleta tija ni lazima Watanzania tukubaliane kwamba kuletwa kwa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam, yatachagua kupunguza msongamano, lakini hautakuwa mwarobaini mzuri iwapo tutaachia bila kuweka utaratibu wa kwamba hao wenye magari binafsi, kama hakuna ulazima wa kuingia na gari lake katikati ya Mji, basi Serikali kupitia TAMISEMI ianzishe *parking fee* isiyopungua Sh. 20,000/= kwa siku. Hii itasaidia sana kwasababu mabasi yaendayo kasi hayatakuwa mwarobaini kama watu wataendelea kuingia na magari yao mjini. Kama kuna umuhimu wa kuingia na gari mjini, basi; inawezekana Sh. 20,000/= ni nyingi, lakini tukae tuone namna gani watu hawataingia na magari yao madogo madogo mjini ili kusaidia kupunguza foleni katika Miji yetu mikubwa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, eneo la kwenda kwa nusu saa, unatumia masaa matatu, hivyo utendaji wa kazi wa watumshi wa Umma na hata sekta binafsi hauonekani kwasababu ya muda ambao tunaupoteza. Naomba hili tuliangalie na wataalamu wanaweza wakakaa chini kuangalia ni kiwango gani hasa kitozwe ili kuhakikisha kwamba kama hakuna ulazima, mtu asiingie na gari lake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie kuhusu Soko la *Machinga Complex* pale Ilala. Mradi ule ulikusudiwa kusaidia wafanyabiashara ndogo ndogo wapate eneo zuri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. M. MABUMBA]

la kufanya biashara zao katika mazingira mazuri na iweze kuwa na tija kwao.

Mheshimiwa Spika, mradi huu tulipoutembelea, kwanza vile vyumba ambavyo wafanyabiashara wamepewa wafanyie biashara, haviko katika mazingira mazuri. Lakini kwa bahati mbaya pia wamelazimishwa wafanye biashara ndani kama nia njema ilivyokuwa, lakini bahati mbaya chini pale wameachiwa watu wengine wafanye biashara. Kwa mfano, kuna *competition* baina ya *Machinga Complex* na lile soko la Mchikichini. Kwa hiyo, wanunuzi, wateja, wengi sana wanaishia kwenda soko la Mchikichini, matokeo yake lile soko la *Machinga Complex* limekuwa kama *white elephant*, sababu biashara ambazo ziko pale ni ndogo ndogo, na kwakweli hakuna wateja wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nashauri Uongozi wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Ilala wakae chini waone pengine waondoe Soko la Mchikichini, watumie soko hili kubwa la *Machinga Complex*, baadaye waone namna gani ya kugawana mapato yatokanayo na kodi ambazo zinazolipwa na wafanyabiashara, kuliko kuwa na masoko mawili haya ambayo yana- *compete*, mwisho wa siku *Machinga Complex* haiwezi kufikia malengo na azma iliyokusudiwa na Serikali, au na Uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Tunasema tunajenga nyumba moja, kwa hiyo, Jiji na Manispaa waone hilo, kwasababu wote wako chini ya Mkuu wa Mkoa mmoja, basi awakutanishe wajadiliane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nataka nizungumzie hapa ni kwamba tumefanya ziara nyingi katika baadhi ya Mikoa, Wilaya na Halmashauri. Baada ya kukutana na watendaji katika Wilaya na Mikoa, imeonekana dhahiri kwamba fedha wanazopewa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa *ceiling* yao ni ndogo sana. Wakuu hawa wanapashwa kusimamia mambo yote yanayoendelea katika maeneo yao utawala. Lakini kama fungu wanalopewa halitoshelezi, siyo rahisi kwao kufanya kazi yao kama ipasavyo. Wakuu hawa wa Wilaya na Mikoa ndio wanaosimamia hata hii *program* ya Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*). Sasa *Big Results Now* kama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. M. MABUMBA]

haisimamiwi, kwasababu tunaamini kabisa kazi kubwa inafanyika katika Wilaya na Mikoa, na ili wafanye kazi yao vizuri lazima rasilimali fedha iwe ya kutosha na ipatikane kwa wakati, waweze kuwa na vitendea kazi, waweze ku-*move*, kutembelea miradi ambayo inatekelezwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka tulipisha bajeti hapa ya trilioni 4.2 kwa TAMISEMI. Ku- *approve* ni jambo moja, lakini kuhakikisha fedha hizi zinakwenda sasa kutekeleza zile kazi ambazo walipangia hizi pesa ni jambo muhimu sana. Naiomba Serikali ihakikishe Wilaya zetu na Mikoa na Halmashauri zinapewa fedha za kutosha kama tulivyopitisha hapa ili waweze kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, tumeelezea pia ziara ya Kamati kwenye ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. Tulipofika pale Kamati ilisikitishwa kuona kwamba mkandarasi yuko pale lakini hafanyi kazi kutokana na ufinyu wa fedha ambazo zinapelekwa kufanikisha ujenzi huu. Lakini mkandarasi hukaa bure, maana yake ni hasara kwa Serikali, maana yake inabidi alipwe huyu, kwasasabu vifaa vyake havifanyi kazi viko pale, lakini ana wataalamu pia ambao wako pale hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba pamoja na nia ile ya kuongeza Shilingi bilioni moja, nadhani bado haitoshelezi na hasa tukizingatia kwamba Mkoa wa Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Serikali yetu, Makao Makuu ya nchi yetu, na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa namna ilivyo haioneshi kwamba kweli Dodoma ndiyo *centre* ya nchi yetu. Naiomba Serikali isimamie tamko lake la kufanya Mkoa wa Dodoma kuwa Mji Mkuu. Kwa hiyo, Mkuu wetu wa Mkoa awe na Ofisi nzuri, kwasababu wageni wengi wanafika pale. Ofisi yake aliyonayo haioneshi kwamba hii ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambayo ni Makao Makuu ya nchi. Naomba Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pia kuhusu ujenzi wa Hospital ya Mkoa wa Singida; bajeti ya ujenzi ya Hospitali hii ni Shilingi bilion 150, lakini fedha zinazopelekwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. M. MABUMBA]

kama Makamu Mwenyekiti alivyoelezea itachukua miaka 70 ili kukamilisha Hospitali ile. Hii ni aibu kwetu. Aibu hasa inakuja kwamba Mkuu wa Mkoa Dkt. Kone alibahatika kupata msaada wa vifaa vya Hospitali kutoka Marekani. Vifaa vile tayari viko pale, baada ya muda vifaa vile vitaharibika vyote. Je, wahisani wataendelea kutuamini sisi? Tuone aibu! Vifaa vimeletwa halafu tutumie miaka 70 kujenga. Aibu! Bora tuahirishe mambo mengine tuhakikishe Hospitali hii inakamilika kwa wakati, na vifaa hivi tunaviokoa na wahisani wapate moyo wa kuendelea kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie Shirika la *UDA*. Shirika la *UDA* kamati ilipokwenda pale, kwanza tulivunjika moyo namna ambavyo Kamati ilipokelewa pale, lakini tukaona kuna ubabaishaji mkubwa sana katika *process* nzima ya ubinafsishaji wa Shirika hili la *UDA*. Thamani halisi ya *assets* ya Shirika hili ni kubwa, ni mabilioni ya Shilingi, lakini wajanja wachache wameweza kunufaika sana. Ingawa suala hili ni la kisheria, tunaamini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaweza kupitia upya mkataba wa Ubinafsishaji wa Shirika hili ili Taifa linufaika sana na Shirika la *UDA*.

Mheshimiwa Spika, leo hii tuna taarifa kwamba maeneo ambayo yako chini ya Shirika hili, Kampuni ya *Simon Group* imeyakodisha na inapata karibu Shilingi milioni 500 kila mwezi, lakini yenyewe imelipa Serikalini huku Shilingi bilioni mbili. Unapata Shilingi milioni 500 kila mwezi, wewe umelipa huku Shilingi bilioni mbili! Serikali yetu imepigwa na tusikubali Serikali yetu ipigwe.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mwanasheria Mkuu aitische mafaili ya Mkataba wa ubinafsishaji wa Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa Nimwite Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar ajiandae na Mheshimiwa Felix Mkosamali atafuatia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini vile vile naipongeza Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hasa pale ilipotembelea Jimboni kwangu, ilifanya kazi nzuri na ya maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zangu nyingi nitazijenga huko, lakini kabla sijafika huko, nilikuwa naomba baadaye Kamati ya Sheria itakapokuwa inatoa ufafanuzi wa mambo kadhaa iniambie na AG anisaidie kwamba suala la fedha la Uswiss imekuwa ni ngonjera ya muda mrefu sana. Tunapokuwa tunaongelea wizi wa mabilioni ya pesa na wananchi wanasikia huko nje na hakuna *action* inayochukuliwa, tunaendelea ku-*circulate pain* miongoni mwa wananchi wetu, na wanaendelea kuona kwamba Serikali inaendelea kupuuza jambo la msingi kama hilo. Kwabahati nzuri sana, alipo AG na Mheshimiwa Zitto hakuna mita nne na Mheshimiwa Zitto ameshawahi kusema ana majina ya walioficha fedha Uswiss; kwa hiyo, nashauri, kuliko hii ngojera iendelee, ni hayo majina apelekewe AG kwasababu Kamati imekwishaundwa ya walioficha pesa Uswiss na kama mnaogopa kuwataja, mimi nitawasaidia kuwataja mkinipa hayo majina nje ya Bunge na ndani ya Bunge. Sihitaji kinga kutaja mwizi, nahitaji kumjua mwizi na kumtaja. Sihitaji *immunity* kumtaja mwizi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema haiwezekani kila saa na kila siku tuna ngojera ya mabilioni yaliyofichwa halafu kuna vibaka wako ndani kwa wizi wa baiskeli kwa miaka saba, nane nje na tunaambiwa tuna majina. Lakini vile vile sina hakika kama kuwa na pesa nje ni wizi. Niweke hilo wazi kwa sababu naogopa kama nitakuwa na akaunti Namibia, siku moja na mimi nitaonekana mwizi. Lakini kwa vile majina ya wezi Mheshimiwa Kabwe Zitto anayo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunakuomba sana, na kama AG hutayataka hayo majina, basi na wewe utakuwa ni kati ya wale walifocha pesa Uswiss, ili hii ngonjera sasa ifikie mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda sasa kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kamati ilipofika Jimboni kwangu ilibainisha mambo ya yafuatayo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. J. LEMA]

Ilibainisha viwanja vya wazi na viwanja vingine vilivyokuwa vimetengwa makusudi kabisa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali. Kiwanja hicho kilichukuliwa na Kampuni moja inayoitwa *Hercon* na baadaye kiwanja hicho kikapelekwa kwa Kampuni nyingine inayomilikiwa na Watanzania wenye asili ya Kiasia. Walipoona kimeanza kufuatiliwa, kiwanja hiki kiliwekwa Benki, kikachukuliwa fedha. Ni kiwanja cha ekari saba ambacho kiko eneo la Njiro.

Mhehsimiwa Spika, kitu kinachonipa mashaka ni kwamba Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya kufuta hati kama inakuwa na mashaka na kiwanja hiki kilikuwa kimetolewa kwa ajili ya Hospitali ya Jiji la Arusha Mjini. Kiwanja hiki kimekwenda kwenye mikono ya watu na sasa ni muda mrefu, ni takraiban miaka minne miaka mitano kiwanja hiki kinapigiwa kelele, lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba kama Serikali yenye Mkuu wa Mkoa yenye Mbunge husika wa eneo hilo, yenye Wenyeviti wa Halmashauri, inaweza ikakosa mamlaka ya kumnyang'anya mtu aliyechukua kiwanja cha kujenga hospitali chenye malengo ya kujenga hospitali ya mama na mtoto, Serikali ikakosa nguvu ya kumnyang'anya mtu huyo kiwanja hicho, na wakati *planning* za awali zinaonyesha hivyo; kwa kweli inatia uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, Arusha siyo hiyo tu, kuna viwanja vingi sana. Kuna kingine tulikuta ilikuwa ni kwa ajili ya Mahakama, nyumba za wafanyakazi wa Serikali, Kituo cha Polisi na kiwanja cha kuchezea mpira. Kiwanja hicho pia kilichukuliwa na hata Kamati ilipokuwa inafanya utafiti iligundua kwamba hata Halmashauri hawana muhtasari wowote juu ya kugawanya viwanja hivyo. Lakini viwanja hivyo leo bado ni milki ya wale watu na wana hati miliki ya viwanja hivyo kutoka kwa Msajili wa Hati za Ardhi, lakini viwanja hivyo ni mali ya Umma, ni mali ya Serikali, ambapo vilistahili kujengwa Mahakama, kujengwa Kituo cha Polisi, nyumba za wafanyakazi wa Serikali, lakini leo kiwanja hicho kimegeuka kimekuwa viwanja vya watu binafsi mbalimbali. Pamoja na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. J. LEMA]

kukosekana mihtasari mbalimbali ya kuonyesha hivyo viwanja viligawiwa vipi; kwa sababu hadi Kamati ilijiongeza muda pale Arusha, ikasema tunaongeza siku mbili zaidi tupate nyaraka na mihtasari ya hivi viwanja vimegawiwa vipi; bado haikuja. Lakini mpaka leo viwanja hivyo, na hata hivi nilivyotoka Arusha Jimboni kuja Bungeni, nimeona kama wengine wameshaanza kuweka *fence*.

Mheshimiwa Spika, kwa ukweli ambao mimi na wananchi wangu tumeugundua, tuna mpango wa kwenda kuweka magoli ya mpira, kwenye lile eneo ambalo ni kiwanja cha mpira ili kama Polisi sasa watakuja kuzuia wananchi wenye hasira kali kuchukua mali yao, basi tutakwenda Mahamani kutetea jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 wakati ninaomba kura ya kuchaguliwa kuwa Mbunge, niliwaahidi wakazi wa Jimbo langu *Machinga Complex*. Lakini nimetembelea baadhi ya *Machinga Complex* kwa ajili ya kujifunza. Ukiangalia *Machinga Complex* iliyoko Dar es Salaam Ilala, utaona kabisa haijatoa matokeo ambayo Serikali ilikuwa imekusudia. Kwanza, Machinga ni watu wanaotembea na kukimbia pande mbalimbali kwa sababu ya kutatufa soko. Sasa unapokuwa na Machinga wengi katika sehemu nyingi, maana yake ni kwamba unapokwenda kuwa *-station* sehemu moja, maana yake ni kwamba unawapunguzia nguvu ya Soko.

Mimi ushauri wangu ni kwamba, kwa sababu fedha za barabara zinazotoka Serialini, asilimia 70 huwa inakwenda *TANROAD* na asilimia 30 huwa inakuja Halmashari, nashauri barabara za ndani za kwenye Majiji yetu na Miji mikubwa ambako kuna misongamano ya Machinga zingetengenezwa. Kwa sababu kinachosababisha Machinga kuwa sehemu moja au kukimbiakimbia katikati ni kwa sababu ya hilo soko analolitafuta. Sasa njia peke yake ya kupunguza Machinga mjini, isiwe ni Serikali kujenga kufikiria kujenga *Machinga Complex*, lakini vile vile iwe ni Serikali kufikiria kuboresha hadhi za Kata ndani ya Miji yetu tunayotoka ili wale watu waweze kubakia huko huko.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. J. LEMA]

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, suala hili linaenda sambamba na watu kuahamia kutoka vijijini na kuja mijini. Kama sehemu ya pembeni ya Miji ingelikuwa kuna maji, kuna umeme kuna barabara nzuri, bado ingeliweza kutoa fursa ya vijana wetu kujajiri pembeni ya Miji na siyo kukimbilia katikati.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba pamoja na mkakati wa *Machinga Complex* lakini Serikali lazima ikaliangalia sana kwamba siyo tija sana kiuchumi kuwa-*station* Machinga sehemu moja, na kwa sababu kazi ya Machinga imekuwa ni kutafuta soko, ni vyema sasa Serikali ikaanza kufikiria kutengeneza barabara. Ndiyo sababu nikasema, ni bora hii fedha ya barabara, hii asilimia 30 inayokuja kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya kujenga barabara za Miji yetu ingeongezwa ili tutengeneze barabara kwenye Kata mbalimbali, ili tuweze kuzuia idadi ya watu wengi kuja katikati ya Miji na kufanya biashara, wabakie huko kwenye Kata. Kwa sababu hakuna mtu anayeweza kwenda kununua kitu mahali ambako barabara ni mbovu, mahali ambako ni *squatters*. Nilikuwa naomba hilo pia nishauri hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini Miji yetu inaendelea kuwa *squatters*. Arusha inaendelea kuwa *squatters* kwa kiwango kikubwa, Dar es Salaam, Mbeya, nafikiri na Iringa na Miji mingine tu Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami. Lakini cha kushangaza sana, Halmashauri zetu bado hazijatengeneza Sheria mbalimbali ya kuwaelekeza hata wale wanaouza mashamba yao ambayo hayajapimwa wayauze katika utaratibu gani na katika mpango gani ili kuacha barabara na kuacha sehemu muhimu kwa ajili ya maeneo hayo kuweza kuwa maeneo salama ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, leo Arusha kuna eneo linaloitwa kwa Morombo. Eneo hilo katika miaka sita au kumi nyuma lilikuwa ni mashamba ya wazi kabisa, ilikuwa ni kama pori. Leo kwa Morombo mtu anapata kiwanja miguu nane kwa miguu 10; ni *square meter* 80, *square meter* 100 *square meter* 60. Imekuwa ni sehemu kubwa, ni kimji kikubwa, lakini imekuwa ni *squatters*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. J. LEMA]

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba itengenezwe Kanuni, utaratibu na Sheria kwamba hata kama shamba ni lako na unaliuza kwa madhumuni ya watu kujenga nyumba, basi kuwepo na mkakati na utaratibu maalum kwamba hata kama unauza shamba, shamba lako utaliuza katika utaratibu huu; na kabla hujapokea fedha ni lazima watu hawa waje waonane na Ofisi za Mipango Miji za Halmashauri ili kupata maelekezo na utaratibu wa kuuza mashamba yao ambayo yanataka kutumika kujenga nyumba. Kwa sababu sehemu ambazo zimepimwa mpaka sasa katika Taifa hili ni chache. Kwa hiyo, hizo ambazo hazijapimwa pia zitengenezewe utaratibu na sheria kwamba hata kama unauza shamba kwa ajili ya mtu kujenga nyumba, utaratibu wako utakamilika utakapofika katika Ofisi za Halmashauri na kuonana na Baraza la Madiwani ili uiambiwe shamba lako hili utaliuza hivi na anayetaka kujenga, atajenga katika utaratibu huu na mfumo huu.

Hii inaweza ikasaidia kwamba *squatters* tulizonazo tukaendelea kuzi-*maintain* zisiongezeke, lakini zile ambazo sasa zinataka kujitokeza, tukaendelea kabisa kuzizuia zisiwepo, na huko baadaye ikawa ni rahisi sana kwa Serikali kuweza kutengeneza mpango mkakati ambao nimeona sasa *National Housing* wameshaanza wa kuanza kuratibu *squatters* ambazo sasa ziko katika Miji yetu.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nimekisikia hapa kwenye taarifa ni kwamba majengo ya Taasisi hayalipiwi kodi. Siyo tu majengo, mimi kwangu nilikotoka, Idara ya Maji inasema inaidai Serikali takriban karibu Shilingi milioni 300 na zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ama Taasisi ambazo zinatakiwa ziwe mfano wa kulipa kodi kwenye *report* hii inasema ni moja ya changamoto, kwamba hawa hawalipi kodi. Hawa hawalipi kodi husika zinazotakiwa. Kwa hiyo, ni vyema sana, Serikali ama majengo ya Serikali, majengo ya Taasisi ama Halmashauri ambao wao ndiyo mfano wa Serikali, wao ndiyo Serikali, wao ndiyo Mamlaka na wao ndiyo wajibu mkuu, wangukuwa wanalipa kodi zao kwa wakati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. G. J. LEMA]

unaotakiwa ili watakapoanza sasa kuzingatia sheria dhidi ya wale ambao hawajalipa wao wawe ni mfano juu ya mambo hayo.

Mhehsimiwa Spika, nilitaka niongelee Hospitali ya Singida ambayo imetengewa Shilingi bilioni 150, lakini kila mwaka inapelekewa Shilingi bilioni mbili, lakini nashukuru Mheshimiwa Mbunge mwenzangu ameshallongelea vizuri, kwahiyo, kwa hayo machache, naishia hapo. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Fakharia Shomar, na Mheshimiwa Mkosamali atafuatia.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kuzipongeza hizi Kamati mbili; Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, na Kamati Kamati ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nina machache tu nataka kuzungumzia ambayo mengi nitajikita kwenye Kamati ya Katiba. Kwanza sina budi kuipongeza *RITA*, kwa sababu *RITA* ilipojiona iko katika matatizo ya kutokuwa na Ofisi ya kufanyia kazi, ikaingia ubia na *NSSF* kwa kuweza kujenga jengo lenye ghorofa 30, ndani yake itasaidi wao kuweza kupata ofisi na kusaidia wengine kuwakodisha ofisi. Jambo hili ni la kupongezwa na la kupigiwa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo dogo lililojitokeza hapa ni kwamba hivi sasa bado *RITA* kuna fedha maalum ilikuwa wachangie, lakini bado hawajaweza kuchangia, na *NSSF* wanaendelea na ujenzi. Sasa huko kunakoendelea mbele wajue kutakuwa na tatizo kwenye kulipa riba kubwa wakati wangeweza kufanya katika kipindi hiki, wakaleta hicho kiwango kidogo walichowekewa wakalipa. Mimi ningewashauri bora wangeangalia, wakajibana lakini wazilipe.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia Sekreterieti ya Maadili. Nakubalina kwa kazi nzuri ya Sekretarieti ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Maadili ya kufuatilia viongozi na kujua mwenendo wao kuhusu mali zao na jinsi wanavyozipata mali hizo, ni suala zuri kwa Taifa. Lakini bada ya shughuli hii kuifanya sijaona tathmini wanayoitoa, kuonesha mafanikio waliyoyapata, changamoto, na katika viongozi ambao waliokuwa wamewachunguza nini wameona faida yake na nini wameona hasara yake. Nadhani kitu kama hiki, kama watakifanya kitasaidia katika kufanya kazi zao vizuri na kuboresha utekelezaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tulizungumza, kuna kada ambapo pia zinatakiwa ziangaliwe, kama Kada ya Uhasibu, kada za manunuzi, hata Wakurugenzi kama vile *Ma-DAP*. Kada hizi ni zinachezea fedha za Serikali, na watu kama hawa muda mfupi utaona maisha yao yanabadilika.

Mimi nashauri, tumezungumza muda mrefu, na sasa hivi tunalipigia kelele, na Kada hii nayo iingizwe, siyo iwe viongozi peke yao na hao waingizwe kutokana na sehemu zao za kazi jinsi na kumiliki fedha nyingi za Serikali. Nasisitiza tathmini ifanywe kwa watu wote wanaochunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuja kwenye TAKUKURU. Kwanza napenda kupongeza kitengo hiki kwa kazi zao nzuri wanazofanya, lakini nataka niulize: wanashirikiana na Halmashauri zetu? Kwa sababu Halmashauri zinapigiwa kelele usiku na mchana kwamba fedha zinatafunwa. Kama kweli TAKUKURU inafanya kazi ndani ya Halmashauri na kuziangalia Halmashauri, naona suala hili lingelikuwa jepesi kwao kuweza kumjua ni nani anayetafuna fedha na fedha zinatoka vipi na nani anayetakiwa awajibike. Kuliko kumkamata mtu mnayetaka kumwajibisha, wakati yeye hahusiki na suala lile.

Mheshimiwa Spika, naomba hili waliangalie na wasiliogope, kwa sababu wajanja wapo na mtu akitaka kuchukua fedha lazima anakuwa mjanja na mbinu tofauti. TAKUKURU mzidi kuwa na mbinu tofauti za kuweza kuwamiliki hawa wajanja kidogo waliopo wanaoitia hasara Serikali. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. K. SHOMAR]

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU wanaweza kusema sheria inawabana au sheria haiwapi nguvu. Tunapiga kekele na tunazungumza mara kwa mara. Kama ni sheria inawabana, wailete tena Bungeni, wazungumze na Wizara yao mama, wazungumze na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, watuletee Sheria Bungeni ambayo itawasaidia kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuweza kufanikiwa pasipo kukaa pembeni wakanung'unika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la Ofisi ya Muungano. Ofisi ya Muungano inafanya kazi vizuri, ambapo iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Hivi karibuni ilikwenda Zanzibar ikafanya kongamano ya shughuli za Muungano ili kuboresha shughuli za Muungano. Lakini namwomba Waziri anayeshughulika na shughuli za Muungano, anapofanya vitu kama kutoa elimu, maboresho na hii Kamati yetu awe anaialika ili iweze kupokea hiyo elimu na iweze kusaidia katika majadiliano ya kuboresha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Ofisi ya Bunge. Wakati wa Bajeti tulizungumza kwamba mabasi tunayotumia hayaridhishi. Tukaambiwa kwamba katika mwaka huu tunafanya mpango wa kutafuta mabasi mapya. Lakini hadi hii leo sijauona mwelekeo huo kwamba kweli tuko katika utekelezaji. Sasa naomba niikumbushe Ofisi yangu kwamba bado tunahitaji mabasi mapya ya kuweza kutusaidia katika majumumu yetu ya kufanyia ziara katika Mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nakubali yaliyozungumzwa na Kamati zote mbili. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Felix Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Kamati ya Katiba na Sheria ambayo na mimi ni Mjumbe na Kamati ya TAMISEMI. Mimi nitajikita zaidi kwenye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. F. MKOSAMALI]

Kamati ambayo nashughulika nayo mara kwa mara ya Katiba na Sheria. Nitaanza kuzungumza juu ya Taasisi ambazo ziko chini ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, huwa kuna sababu kwamba kwa nini Tasisi kama vile *PCCB*, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Taasisi nyingine, kuna sababu ya kuziweka Taasisi hizo ziwe Ofisi ya Rais au ziwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Huwa kuna sababu. Moja ya sababu inawezekana ni kwa sababu mambo haya ni *cross cutting*; kwa mfano, rushwa iko katika kila Wizara. Sasa *PCCB* isipo-*perform* vizuri tutakuwa tunadhaliisha hizi ofisi ambazo ziko kwenye ofisi hii muhimu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, *PCCB* imekuwa inatuhumu kesi nyingi sana. Kwenye ripoti yetu ya Kamati ya mwaka 2012 tulisema zaidi ya Kesi 4,448 ambazo *PCCB* walituhumu, kesi ambazo walifaulu ni 48. Kwa hiyo, tuhuma ni nyingi lakini kesi ambazo wanafaulu Mahakamani ni chache, na tunapitisha fedha nyingi kwa ajili ya Taasisi hii. Ukizunguza na *PCCB* anasema mimi si-*prosecute* hizi kesi, anayehusika nazo ni *DPP*. Ukimwuliza *DPP* anakwambia kesi hizi zinakuwa hazina ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inapaswa kutupa majibu, msimamo wa Serikali ni upi? Nani anayesababisha kesi nyingi za *PCCB* zishindwe? Ni *DPP* au *PCCB* ambayo inatuhumu hizi kesi? Nani? *Solution* ni nini? Kwa sababu hatuwezi kuwa na chombo kinatuhumu *then* ni Mahakama? Mahakama ndiyo inaamua vibaya? Tupewe majibu, *what is the problem?* Hiy moja.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA, nilikuwa nasoma hapa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. *TASAF* kazi inayofanya ni kuwezesha watu masikini katika kuwapatia fedha na kadhalika. Lakini nimeshaomba hapa Bungeni mara nyingi kwamba tupate *framework*. *Framework* ya MKURABITA itamaliza kurasimisha hiyo ardhi na raslimali za wanyonge, mwaka gani? Itaendelea kudokoa dokoa hivyo hivyo? Leo utasikia wako wapi, leo wako wapi; tumeshaomba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. F. MKOSAMALI]

waje na *framework* tujue lini wanapima hii ardhi na kumaliza?

Mheshimiwa Spika, Kamati tukienda kuwatembelea tunaambiwa kwamba hawana fedha na kadhalika, wanapewa Shilingi bilioni moja au mbili, hawawezi kufanya hii kazi. Lakini ukiangalia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, *land* ni moja ya *issue*, lakini MKURABITA imekuwa ikifanya kazi kwa kudonoadonoa.

Sasa sisi tunataka Serikali ambayo inakuwa *serious*. Kama ni Taasisi kweli inashughulika na upimaji wa *land* ili watu waweze kupata mikopo, basi *land* ipimwe, tujue inaanza leo, inamaliza mwaka fulani. Kama hizo hati zinazotolewa na MKURABITA haziwasaidii kupata mikopo, leteni sheria, tutunge sheria hati hizo ziwe kama hati nyingine. Tutaweka MKURABITA, Ofisi ya Rais kazi inayofanya ni kudonoadonoa; Ngara, kesho Kibondo, keshokutwa sijui Njombe; kazi inaisha lini? Inaanza lini na mwisho wake ni lini?

Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma. Kama alivyoeleza vizuri Mheshimiwa Ntukamazina, nchi yoyote ili iendelee lazima watu wafanye kazi kwa muda uliopangwa kisheria na kazi zao zifahamike wanafanya kazi zipi. Ndiyo maana tumeshauri Watumishi wa Umma waingie mikataba ili tuweze kupima ufanyaji kazi wao.

Tumeanzisha *Big Results Now* hapa; sisi tulivyoambiwa na Tume ya Mipango ni kwamba Mawaziri watakuwa na wenyewe wanaingia mikataba ya kazi wanazofanya. Lakini kama Bunge lako litakuwa haioni hii mikataba, Katibu Mkuu wa Wizara fulani, Waziri amepangiwa kufanya hivi; hii *Big Results Now* itakuwa haina maana. Kwa sababu tumesema hii *Big Results Now* ambayo tunaipitishia Shilingi bilioni 29, kazi yake itakuwa ni kufuatilia utendaji kazi wa watu. Sasa hii mikataba iko wapi? Kwa nini Bunge lisioneshwe hii mikataba? Waziri fulani amepewa kazi hii aikamilishe ndani ya muda huu, tuone.

Mheshimiwa Spika, kama hatuoneshwi mikataba hiyo, maana yake itakuwa ni kawaida, itakuwa ni kama zamani.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. F. MKOSAMALI]

Kwa hiyo, Bunge lianze kuona mikataba ya Mawaziri kwa kazi ambazo wanazifanya. Makatibu Wakuu wapewe mikataba ya kazi zao tuione. Ilitakiwa wakati tunawasilisha taarifa kama hii na vitu kama hivi tunapima, wamefanya vile? Mawaziri na Makatibu Wakuu lakini mpaka wafanyakazi wa chini. Tanzania hii unaweza kwenda kwenye ofisi za TAMISEMI; mimi nimeshawahi kwenda kwenye ofisi ya Mkurugenzi mmoja, kila nikienda naambiwa amesafiri.

Hawa Wakurugenzi wa Halmashauri, kila nikifika Kibondo, naambiwa Mkurugenzi amesafiri, au yuko kwenye vikao. Sasa utumishi wa Umma ndiyo kusafiri, kusafiri, kusafiri! Sasa Mkurugenzi Mtendaji huo utendaji anaufanyaje kwa kusafiri kila siku? Utumishi wa Umma ni kazi za kutenda, sasa tusipowapa mikataba Wawakilishi wa wananchi tukawa tunaiona, kwa kweli ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma tumezungumza mwaka 2012 na mwaka huu 2013 kwamba kazi ya Sekretarieti ni nini? Ni kujazisha fomu watu? Watu wanajaza fomu, kila mwaka tunajaza, lakini hatusikii nani ambaye amekamatwa amevunja maadili haya? Nani ameonekana hata ambaye amepata mali ambazo siyo halali? Yupi? Au hayupo? Tunajaza fomu zaidi ya viongozi 10,000; fomu ambazo zinapitiwa hazifiki hata fomu 500 ndiyo taarifa ambazo tumekuwa tunapewa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa kazi ya hii Sekretarieti ni nini? Haikamati mtu, hakuna watu ambao wamekutwa na makosa, hatujasikia kwamba Waziri fulani wakati ni Waziri alipata mali ambazo siyo halali. Hatujawahi kuona! Rais fulani, na kadhalika. Hizi fomu ni kujaza tu au kuna kitu kingine za cha ziada? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hii iko chini ya Ofisi ya Rais, sasa kuwa na chombo ambacho kazi zake zipo lakini hatuoni kitu kinachofanyika na tunapitisha bajeti kila mwaka hapa Bungeni, binafsi naona ni tatizo kubwa. Naomba Serikali wakati inajibu itueleze, Sekretarieti ina-*achieve* vipi?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. F. MKOSAMALI]

Inakamata watu wangapi? Akina nani? Au haikamati, Watanzania wote wana maadili? Kama wana maadili, hizi rushwa na vitu vingine vinatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Mheshimiwa Rais ndiye anayeteua Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mkoa. Kuna Mkuu wa Wilaya ya Uvinza aliagiza watu waende kuchoma nyumba za wananchi, zikachomwa nyumba 68. Waziri Mkuu akaagiza kwenye kikao cha Kanda kwamba Mkuu wa Mkoa afuatilie nyumba zilizochomwa. Hakuna ambacho kimefanyika mpaka leo. Kuna Mkuu wa Wilaya mwingine mlimleta kule kwangu Kibondo na yeye akaagiza kwamba kijiji fulani kifutwe, kifungwe. Sasa hao Wakuu wa Wilaya huwa mnawatoa wapi? Watu ambao wanaagiza nyumba zichomwe, kufunga vijiji, watu wahame (*deportations*) na kadhalika huwa mnawaokota wapi? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba tujibiwe, hatuwezi kuwa na Wakuu wa Wilaya ambao ni *sub-standard*, watu ambao hawana uwezo wa kufanya kazi, watu ambao wanashinda wanaibua migogoro ya wananchi. Waziri Mkuu anaagiza lakini hakuna kitu kinachofanyika halafu wanaendelea kuwa ma-DC. Tuambiwe kazi za Wakuu wa Wilaya ni zipi wanazozifanya na ingekuwa ni muhimu sana Kamati ya TAMISEMI iwe inatuletea ripoti ya kila Mkuu wa Wilaya. Maana sisi kabla Kamati hii kugawanywa tulikuwa tunapitia na bajeti za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mkoa.

Tuambieni kwamba huyu Mkuu wa Wilaya amefanya kazi moja, mbili na tatu; huyu naye amefanya kazi moja, mbili na tatu. Hakuna kitu wanachofanya! Ndiyo maana wanaishia kuagiza watu wakachome nyumba za watu, kufunga vijiji na kufanya vitu vya ajabu ajabu kwa sababu hawana kazi za kufanya, na sisi hatujui mnawapataje, mnawaokotaje, kwa sifa zipi na kadhalika, hatufahamu! Tujibiwe na Waziri anayehusika na TAMISEMI. Nalisema hili kwa sababu na fungu la Waziri Mkuu lipo hapa na hawa watu wako chini yake, kwa hiyo, tujibiwe.

Suala la Uvinza limeishia wapi na kwa nini Mkuu wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. F. MKOSAMALI]

Wilaya ya Kibondo anaweza kuvunja Katiba na kuvunja sheria, afute kijiji ambacho kimesajiliwa na ambacho kina hati? Hayo mamlaka ameyatoa wapi? Alifundishwa hiyo kazi na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Tuna dakika kumi, Waziri wa Sheria si unaweza kujibu kitu kimoja tu hicho alichokuuliza? Tafadhali!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala.

Kwanza, nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati hii kwa kazi nzuri sana ambayo imekuwa ikifanya. Kwangu mimi imekuwa ni Kamati ambayo imesaidia sana katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Kama siku zote ninavyowaambia, wao wamekuwa ni Bodi nzuri sana ya Wakurugenzi kwangu, mimi nikiwa kama *CEO* wa Sekta hii na tumefanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki utafahamu kwamba tumepitisha sheria moja lakini mara kadhaa sheria hiyo imekuwa ni sheria muhimu sana lakini ilikuwa na sehemu ambazo kama tusingekuwa na ushirikiano mzuri na Kamati hii, pengine tungepata taabu sana kuipitisha sheria ile. Lakini nachukua nafasi hii kuwashukuru sana Kamati kwa sababu wameonesha ushirikiano mzuri na tumepitisha sheria ile muhimu sana ambayo inatuongoza katika mchakato mzima wa kupata Katiba yetu mpya. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo kwa kweli kwa Kamati yenyewe sina zaidi la kusema, labda nichangie tu moja ambalo limeulizwa la mahusiano ama utendaji baina ya Mkurugenzi wa Mashitaka na Mkugenzi Mkuu wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa uendeshaji wa mashitaka uko hivi; zamani ilikuwa Polisi ndiye anayemtuhumu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

mtu kisha anamchunguza, anamkamata na kumshitaki. Serikali ikaona kwamba mfumo huu siyo mzuri kwa sababu unakipa chombo hiki cha Polisi madaraka makubwa sana ya kuanza kumshuku, kumtuhumu, kumkata na kumshitaki mtu mmoja. Tukasema basi kuanzia sasa tutagawanya madaraka haya. Kazi ya kushitaki na kuendesha mashitaka ndani ya Mahakama itafanywa na Ofisi ya *DPP* na wataalamu wake ambao ni wanasheria wa Serikali. Kazi ya kutuhumu na kutafuta ushahidi ili mtu aweze kushitakiwa itafanywa na Polisi. Kwa upande wa *PCCB* TAKUKURU nako ni hivyo hivyo. TAKUKURU watawashuku, watatafuta ushahidi halafu ushahidi ule utapelekwa kwa *DPP* ambaye ndiye atakuwa na majukumu ya kushitaki.

Vile vile *DPP* ana mamlaka na ameyatumia mamlaka haya mara kadhaa ya kuwapa watu madaraka ya kushitaki kwa niaba yake. Watu hawa wapo *PCCB*, amewapa nafikiri siyo chini ya Maafisa 200 wanaweza wakaendesha mashitaka kwa niaba yake. Amewapa Maafisa katika Wizara ya Maliasili na Utalii ambao nao pia wanaweza wakaendesha mashitaka, amewapa madaraka Maafisa katika Wizara ya Kazi ambao nao pia wanaweza wakaendesha mashitaka kwa niaba yake.

Kwa hiyo, mwenye jukumu la kuendesha mashitaka nchini hapa ni *DPP*. Sasa kwa nini kesi zinashindwa, na kushinda? Tunapokwenda Mahakamani tunakwenda kutafuta haki. Kushinda ama kushindwa ni matokeo ya ushahidi uliopelekwa mbele ya Mahakama, Mahakama inatazama ushahidi uliopo, inaangalia na sheria inavyosema, basi inatoa uamuzi huo. Tunapokwenda kushitaki, hatuna nia ya kusema ni lazima tu tushinde, hapana. Tunachotaka ni kwamba haki itendeke. Sasa kutendeka kwa haki ni pamoja na kushindwa yule aliyekwenda kupeleka kesi vilevile.

Kwa hiyo, siyo vyema kusema kwamba labda kesi za rushwa zinashindwa kwa sababu kuna mahusiano mabaya baina ya vyombo viwili vya *DPP* na TAKUKURU, hapana. Mahusiano ni mazuri, na mpaka sasa mahusiano ni mazuri sana. Yalitokea maneno kwenye magazeti lakini tulikaa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu tukayamaliza yale, sasa mahusiano ya vyombo hivi ni mazuri kama yalivyo mahusiano baina ya Ofisi ya *DPP* na yale ya Polisi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilitaka nilisemee hilo kidogo tu ili hii picha inayotokea huku inayotaribu kuwekwa kwamba pengine watu hawa hawahusiani vizuri ndiyo maana kesi zinashindwa, lakini Serikali yenyewe kupitia Ofisi ya *DPP* baada ya kupewa ushahidi na Polisi imepeleka kesi na nyingine tumeshinda. Tumeshinda kesi nyingi na zipo chache tumeshindwa. Hiyo ndiyo hali ya utoaji haki ilivyo. Tunakwenda Mahakamani kutafuta haki tu; sasa haki inaweza kuwa aidha upande wa kushinda au upande wa kushindwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu kwa kweli nimeambiwa Wizara yangu haina bajeti ya kutosha na mimi nakubali. Ni kweli bajeti haipo ya kutosha lakini imekuwa kipanda mwaka hadi mwaka.

Tunashukuru tunao Mfuko wa Mahakama ambao umezidi kuimarika kwa sasa na kama utoaji wa fedha ungekwenda kama inavyotakiwa, basi shughuli za uendeshaji wa kesi Mahakamani zingekwenda vizuri kwa sababu zote zilipata bajeti kamili, ila sasa bahati mbaya imekuwa upatikanaji wa fedha zenyewe hatupati *OC* kama tulivyotegemea kupata, kwa hiyo, nako pia tunazorota kidogo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi bajeti ya sekta yangu imekuwa ikikua mwaka hadi mwaka na naishukuru Kamati imetusaidia sana katika jambo hili, Kila ilipopita katika Mahakama au katika vyombo vyetu, walivyotembelea *RITA* wanarudi wanatupa ushauri na sisi kama watekelezaji, tunatekeleza na mara nyingi sana tumekuwa tukitekeleza ushauri wa Kamati hii.

Kwa hiyo, naishukuru Kamati, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, hata wakichangia hoja zangu huwa nafurahi sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

Mara ya mwisho nilisimama hapa mbele nikaleta hoja ya mabadiliko ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na pale mwisho alianza Mheshimiwa Mnyaa akaunga mkono hoja ile, akaja Mheshimiwa Mbatia naye akaunga mkono na Mheshimiwa Mbowe kwa mara ya kwanza nikasikia anasema naunga mkono hoja.

Kwa hiyo, ilikuwa ni hoja ambayo kwa kweli ilikubalika na Bunge zima na mimi nafikiri basi *PR* hiyo tuendeleze katika Bunge la Katiba ili tupitithe mambo yetu vizuri. Tunatengeneza Katiba siyo ya leo tu bali ni ya miaka mingi ijayo na tunategemea ushirikiano kama huu ulioanza katika kipindi cha Bunge lililopita utaendelea hadi hapo tutakapopitisha Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Nakushukuru sana kuwa kunisaidia kutumia muda vizuri, ilikuwa imebakia dakika chini ya 15.

Nina tangazo ambalo nimeombwa nitangaze na Mheshimiwa Engineer Mnyaa na Mheshimiwa Ally Juma; majina mengine mbona sinawahi kuyasikia? Lakini anaomba Wabunge wote wanaotoka Zanzibar wakutane mara baada ya kuahirishwa kwa kikao hiki, watakutana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, Wabunge wote wanaotoka Zanzibar watakutana huko baada ya kuahirishwa kikao.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea saa kumi na moja na sasa nasitisha shughuli mpaka saa kumi na moja.

(Saa 6.57 mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kama tulivyoyaanza leo asubuhi ambapo mbele yetu kuna hoja za Kamati mbili, Hoja ya Kamati ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Hoja ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Said Mtanda simwoni, Mheshimiwa Genzabuke, naendana na orodha yangu, sasa ngoja niangalie aliyepo badala ya kuwataja ambao sidhani kama wako hapa. Namwona Mheshimiwa Pauline Gekul, aanze atakeyefuata nitamtaja baadaye.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie machache tu katika hotuba za Kamati zote mbili. Kwanza, ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI na nianzie kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wenyeviti wote ambao wameweza kuwasilisha taarifa za Kamati zote mbili pamoja na mapendekezo mbalimbali ambayo yameweza kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itazingatia mapendekezo ambayo Kamati hizi mbili wameyaandika ni imani yangu kwamba mabadiliko mengi yatafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati ya TAMISEMI, tulizungumzia suala la fedha za maendeleo kupelekwa katika ngazi za Kata na tukasemea hili tatizo ambalo lilipatikana katika Manispaa ya Kinondoni, kwamba fedha zinapelekwa katika ngazi za Kata na tukaishauri sana Serikali na naamini kwamba Mheshimiwa Waziri Ghasia ni msikivu katika hili kwamba fedha hizi zinapopelekwa katika ngazi za Kata ni nani anazisimamia. Kwanza wale Watendaji tulichokiona katika Manispaa ile wanakaa na fedha nyingi sana. Mtendaji anaweza akakaa na zaidi ya Shilingi milioni 200, ni Mtendaji wa Kata.

Vile vile katika Ngazi ya Manispaa pale, wao wanatekekeza miradi. Mfano, katika Hospitali ile ya Mwananyamala, wanakarabati ile Hospitali pale zaidi ya Shilingi milioni 100, lakini inaonekana kwamba Hospitali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

ukarabati umefanyika na wanasema kwamba hizi fedha zimetumika ni zile za Kata, unakwenda kwa Mtendaji anakwambia nina hizo fedha bado hazijatumika. Hapo tunaona mkanganyiko mkubwa sana. Inawezekana Bunge linapitisha fedha, lakini kumbe kuna kuwa na masalia mengine, kuna fedha nyingine zinakuwa zimebaki zinaelelea, wale Watendaji wanatumia zile fedha baadaye mahesabu haya yanakanganya sasa, zipi zimetumika, wakati Mtendaji anasema kwamba kuna fedha hizi bado hazijatokwa kwa ajili ya Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linaweza likawa limejitokeza katika Hospitali ile au katika Manispaa ile lakini kukawa na huu mchezo wa kupeleka fedha kwenye ngazi za Kata. Mimi katika Halmashauri yangu sijawahi kuona kwamba fedha kiasi hicho mamilioni ya pesa yanakwenda huko, lakini ni vizuri Mheshimiwa Waziri wakati wa kujumuisha akalieleza hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kiasi gani ambacho kinatakiwa kipelekwe katika ngazi ya Kata na zikasimamiwa kwa sababu hizi ni fedha za wananchi, ni vizuri tukafahamu; maana Kamati pia tulishangazwa sana, inawezekanaje kiasi kikubwa kiasi hiki kinapelekwa halafu Mtendaji anakaa tu na zile pesa, Halmashauri wao wanatekeleza kivyao, lakini huku yule aliyepewa pesa, zile pesa hazijatumika?

Kwa hiyo, ni mkanganyiko mkubwa sana. Lakini Halmashauri nyingine hawafanyi hivyo. Hebu tuambiwe kama ni *channel* ya ufisadi au ni watu wachache wanafanya tu hivyo kwa kukiuka utaratibu na hili lirekebishwe haraka sana kwa sababu vinginevyo mamilioni ya pesa yatatumika bila kuwa na rekodi sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo niendeleo kuishauri Serikali au Wizara mbalimbali kuhusu tatizo la msongamano Dar es Salaam, Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya TAMISEMI ameweza kulisemea hili na mimi nilirudie. Tulifika katika ziara yetu pale Uingereza. Ukienda pale London utaona magari yanayoingia pale Mjini kwenye *City Centre* yanatozwa na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

hakuna foleni hata kidogo. Pamoja na kwamba tuna hili zoezi la dhati la magari yanayokwenda kasi, tunaweza tukachukua hili na tukapunguza msongamano ambao unaisababishia Taifa hasara ya zaidi ya bilion tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali ikachukua hili wazo wakaangalia wale ambao siyo lazima kwenda na gari katika *City Centre* wakapaki magari yao pembeni. Hili ukiangalia tuseme tu ukweli, utakuta msongamano wa magari ni mengi sana, lakini chungulia kwenye yale magari, amekaa mtu mmoja. Uangalie yale magari ukiwa katika msafara Dar es Salaam katika pilikapilika za pale, wengi hawazidi wawili au watatu.

Kama tutaanzisha *public transport* itasaidia sana hata wale wafanyakazi kuwahi kazini, lakini pia itapunguza msongamano mkubwa sana badala ya mtu tu kwenda na gari lake *City Centre* ni vizuri akalipaki pembeni na tukaanzisha tozo maalum, inaweza ikawa Sh. 10,000/= kwa siku maana wenzetu wanachaji zaidi ya *pound 30*. Kwa nini sisi tusilichukue hili kwa sababu foleni ya Dar es Salaam ni kubwa sana na hata tukijenga hizi barabara za kupita huku na kule haitasaidia kama hatutadhibiti magari haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie suala la Mameya wa Halmashauri mbalimbali kuwa na *qualition* na Wakurugenzi. Nami nimpongeze Mheshimiwa Ghasia kwa suala la Manispaa ya Ilala, aliweza kusimamia kwamba yule Mkurugenzi aendelee kubaki pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Mameya wanatokana na Vyama na itasikitisha sana pale ambapo kama Meya labda ni Mjumbe wa Kamati kuu ya CCM, basi tukamwogopa hata kama anavuruga Manispaa au Halmashauri. Lakini nilisemee hili, ni vizuri pia tuwe na vikao vyetu vya Vyama, naamini kila Chama kina *caucus* ya Baraza la Madiwani kabla hawajaingia lakini pia hata Wabunge wana *caucus* za Vyama. Hivi inawezekanaje unamwona kabisa Meya wa Chama chako anasitisha shughuli za Utendaji kwa ngazi ya Manispaa Watendaji wote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

wanavurugwa kwa sababu tu Meya hamtaki Mkurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtaka tu Mheshimiwa Waziri kwa hili asione aibu na asiseme kwamba huyu ni Mjumbe wa Kamati kuu ya Chama cha Mapinduzi, amepewa rungu sidhani kama atashindwa kulitumia. Nami naomba tu awe mkali sana katika hili kwa sababu haiwezekani ameteuliwa Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Halmashauri au Meya anasema mimi sikuelewi, umefikafikaje mahali hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikalini kuna udhaifu pia. Kuna suala la kuwapeleka hawa Wakurugenzi pasipo utambulisho hata kwa hao Mameya au Wenyeviti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kuna tatizo gani kama mtu ameteuliwa kuwa Mkurugenzi kwenda na barua au barua ikafuata mlolongo unaoeleweka kwamba hata wale wenyeji wakapata taarifa kwamba wewe kuanzia leo umechaguliwa kuwa Mkurugenzi wetu, umeletwa mahali hapa tufanye kazi. Hili lilisababisha pale ilala watu wakashindwa hata kufanya *transactions* za benki kwa sababu Mkurugenzi hafahamiki kwa sababu tu Meya naye hajaelewa kwamba amefikaje huyu Mkurugenzi mahali pale, utakuta ni kutunishiana misuli wakati huo miradi ya maendeleo inashindwa. Katika miradi ya maendeleo fedha za wananchi haziendi kwa sababu tu sisi tunatunishiana misuli kwamba wewe umekuja lini na umekuja kwa mamlaka ya nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii inayohusika watoe mwongozo kwa Mameya wote na watoe mwongozo kwa Wenyeviti wote wa Halmashauri. Kama kuna taratibu zinakiukwa na Serikali iangalie, wanapelekwa utambulisho kwa ngazi ipi? Kama ni Mkurugenzi, anaenda na barua yake Mkononi aende nayo; kama inatoka kwa RAS, Ofisi ya Mkoa ipelekwe mapema badala ya kuanza kutibu matatizo wakati tatizo lilishajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa sana na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisemea ni fedha za miradi ya maendeleo kutokwenda kwa wakati. Hili pia tumeliona pale ambapo Serikali inaliomba Bunge tuwatengee fedha za ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Serikali imesema kwamba inaanzisha Hospitali mbalimbali na imetenga fedha kwa *phase* mbalimbali. Lakini angalia sasa kwenye uhalisia, Bunge linatenga bajeti, tukishaidhinisha bajeti Serikali hampeleki fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha nyingine zinakwenda mwishoni mwa mwaka wa bajeti zinakuwa hazitekelezeki tena. Lakini fedha nyingine zinakuwa hazipelekwi kabisa na tuliona tatizo hili katika Hospitali ya Mkoa wa Singida, tuliona katika jengo la Mkuu wa Mkoa wa Dodoma fedha haziendi. Hata zile ambazo zimetengwa, haziendi.

Nami niliuliza katika Bunge hili mwezi tu uliopita kuhusu fedha ambazo zimetengwa Shilingi bilioni 1.4 kwa Hospitali yangu ya Mkoa wa Manyara; ni mwaka wa bajeti unakwisha sasa fedha haziendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni vizuri Serikali mkaangalia vipaumbele na tukashauri wakati mnaleta mpango ule wa maendeleo tukasema vipaumbele vyenu ni vingi sana. Ni sawa mtu unataka kushika huku na huku na kule huwezi. Hebu tengeni mwaka huu wa bajeti Serikali ituambie mwaka huu tunamalizia Hospitali ya Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Singida na Mikoa mingine mitatu minne badala ya kuahidi Mikoa yote kwamba tunawajengea Hospitali wakati ni changa la macho fedha haziendi, ni jambo ambalo kwa kweli linasikitisha. Serikali na Kamati ya bajeti naamini katika hili mtafanya kazi na mtaona ni jinsi gani ambayo tunakuwa tunatunga au tunaidhinisha bajeti ambayo ni hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miradi ya maendeleo siyo katika ngazi tu ya Hospitali, lakini tumeona hata katika barabara, tumeangalia Mfuko wa Barabara

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

katika Serikali zetu za Mitaa ni fedha kiasi gani zinaenda. Utakuta kwamba fedha nyingi zinaishia kwenye *TRUNK ROADS* (barabara za lami) lakini kile kidogo ambacho kinaenda kwenye barabara katika Serikali za Mitaa hata usimamizi wake ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naendelea kushauri Wizara ya TAMISEMI kwamba ni vizuri katika ule mpango mzima wa kuanzisha benki sasa kwa ajili ya TAMISEMI ili Halmashauri hizi zikope ni vizuri mkaacha kukopesha fedha katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu kopesheni vifaa vya upimaji ardhi; hebu kopesheni vifaa vya ujenzi wa barabara, *let's say* Mkoa wangu wa Manyara; tupatieni vifaa vya ujenzi wa barabara pale Halmashauri ya Mji wa Babati ili na sisi sasa tukodishe kwenye Halmashauri nyingine ili tupate fedha za kulipa ule mkopo, badala ya nyinyi kukopesha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeona Mheshimiwa Waziri Halmashauri nyingi hata kwenye ile Bodi ya Mikopo katika Serikali za Mitaa hawalipi zile fedha. Halmashauri nyingi zinadaiwa, hebu katika kuhakikisha maendeleo nchi hii inapatikana Mheshimiwa Naibu Spika kwa sababu hivi tunavyoongea kwa upande wa barabara, barabara nyingi za Serikali za Mitaa ni mapario ya ng'ombe kwa Mkoa ya Wafugaji. Hakuna barabara zilizochimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupeni vifaa tukapasue barabara mpya ili zile barabara zikarabatiwe tukiwa na vifaa katika ngazi ya Mkoa badala ya kuzipatia Halmashauri fedha lakini hizo fedha zikatumika vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sasa Serikali ikajitizama ikakopesha vifaa vya upimaji ardhi kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

Halmashauri, ikakopesha vifaa vya kutengeneza barabara, utaona kazi inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila nia ya dhati ya usimamizi wa fedha hizi, bila Wakurugenzi kuwa na nia ya dhati na wakasimamia fedha hizi, bila Madiwani kuvaa viatu vyao na kusema hizi ni kodi zetu tuzisimamie. Hakuna kazi itakayoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sababu ya kujitazama kama Viongozi ambao tumepewa jukumu hili na Watanzania. Tuna sababu tunaposimama mbele zao kwa miaka 52 ya uhuru tuwaambie tumeacha *land mark* gani? Tumeacha kitu gani ambacho wananchi watatukumbuka? Leo tunamlilia Mandela kwamba ameacha haya na haya na haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM mtakapoondoka madarakani Watanzania watawakumbuka kwa hali gani, kama hata sasa barabara kwa miaka 52 ya uhuru ni mapario ya ng'ombe kwenye Mikoa yetu.

Zaidi ya barabara za Wilaya na za Mikoa, tuwe tu wakweli. Majimbo mengine hayapitiki, mnafahamu! Hata tukipinga au tukibeza, kuna Majimbo hayapitiki! Huwezi kwenda kijiji kimoja kwenda kingine. Mimi natoa ushauri huu kwa Serikali leo kwamba ni vizuri tukajitizama badala ya kupeleka fedha tukapeleka vifaa kwa ajili ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Baada ya Mheshimiwa Pauline Gekul, namwita Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii, na nianze na suala la Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia suala la Mahakama katika nchi yetu, katika kila Wizara nadhani kuna Wizara ambazo hazipewi vipaumbele au zinasahauliwa kabisa. Suala la Mahakama ni tatizo katika maeneo mengine.

Mimi nimekaa hapa Bungeni kwa muda mrefu na kila wakati nilikuwa nalalamika kwamba hatuna Mahakama ya Mwanzo wala hatuna Mahakama ya Wilaya. Kila Waziri aliyepitia katika Wizara hii anajua ombi langu na huyu aliyeko sasa nadhani ni mara ya pili kuingia na namwambia kila wakati. Lakini tatizo ni fedha, hawapewi fedha kabisa Wizara hii. Sasa nashindwa kujua kwamba watu wa Longido watapata haki namna gani kama hakuna Mahakama ya Mwanzo wala Mahakama ya Wilaya!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakaimu walioko hata usafiri hawana, hawana Mahakama, kwa hiyo, kila anayepangiwa Longido, kwa kweli anataka tu abadilishe kituo. Naomba suala hili lipewe tena kipaumbele ili tuangalie kama wananchi wataweza kutendewa haki. *(Makofi)*

Suala lingine ni wazee wale wa Mahakama. Ukisikia kitu wanachopewa ni kidogo sana. Wazee wanakuja kukaa hapo, lakini baadaye wanachopewa ni kidogo, jamani tuwaangalie na hawa wazee wetu kwa sababu wanafanya kazi. Mbona basi imeshindikana kuendesha Mahakama bila ya hawa wazee? Kwa hiyo, naomba suala hili la Wazee kile kidogo wanachopewa waongezewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kanuni. Tuna sheria nyingi sana tunapitisha hapa; inahitajika Wizara watunge kanuni, lakini hakuna kinachofanyika. Kuna kanuni nyingi sana zinahitajika mpaka sasa sheria wakati mwingine zinashindwa kutumika kwa ajili ya kanuni zinazosubiriwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MICHAEL L. LAIZER]

Kwa mfano, tulisema hapa Halmashauri waruhusiwe kuajiri. Ule utaratibu mpaka sasa bado Halmashauri haziwezi kuajiri Watumishi ambao inapaswa kuwaajiri. Hivi nini kinashindikana? Naomba Serikali wakati mwingine wafanye juhudi kuharakisha baadhi ya mambo ili Wananchi wapate huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni la Muungano. Suala la Muungano ni gumu na ni zuri kwa sababu limejengwa. Muungano umejengwa kwa muda mrefu. Miaka 50 sasa tuko kwenye Muungano, tunarekebisha kila wakati matatizo yaliyoko katika Muungano. Kwa sasa watu wengine wanasema hili ni jambo jepesi tu kuweza kuvunja Muungano. Wanafanya ni kitu rahisi tu kuvunja Muungano. Sijui ni kwa sababu watu wengi walizaliwa baada ya Muungano ndiyo wanafikiri ni kitu chepesi tu. *(Makofi)*

Jamani hili ni jambo zito, ni suala la muhimu sana kuangalia na kufikiria kuimarisha zaidi Muungano, siyo kuvunja Muungano. Hivi nani amejiandaa kuvunja Muungano, ajue kwamba tunavunja kwa njia gani, taratibu ni zipi? Ni kusema tu kuvunja Muungano basi, tumejiandaa. Kwa hiyo, hili suala tuliangalie sana. Naomba Wabunge wenzangu, tuangalie tena michango yetu tunapochangia hapa Bungeni. *(Makofi)*

Nadhani baadaye tukiingia kwenye Bunge la Katiba, Wajumbe wengine wanaoingia ni wachache kidogo kuliko sisi Wabunge tulioko hapa na wa Baraza la Wawakilishi. Naomba tuache vijembe, tuache siasa, kwa sababu Katiba tunayounda siyo ya Chama cha Mapinduzi wala Katiba ya Chama chochote, ni katiba ambayo Chama chochote kitakachoshinda miaka ijayo ndiyo kitatumia. Kwa hiyo, msije mkasema hapa ni ajenda ya CCM; hakuna ajenda ya CCM, tuangalie tutaiendeshaje nchi yetu.

Tuangalie miaka ijayo, siyo lazima wewe uwepo miaka ijayo, lakini utakuwa umeiundia nchi yako jambo zuri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MICHAEL L. LAIZER]

sana. Tutakumbukwa kwa jambo hili muhimu ambalo tumewatengenezea Watanzania. Hatukuwatengenezea Wanachama wa Chama cha Mapinduzi wala wa CHADEMA. Naomba tuache vijembe kwa suala hili na tuweke siasa pembeni. Naomba hili jambo tuliombe Mungu na sisi wenyewe tuwe makini katika mchango huu wa Katiba. Pamoja na Muungano, tusibeze Muungano ndugu zangu. Tuimarisha Muungano udumu na uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tulikuwa tunasikia tu Waziri Mkuu alikuwa anatumia sana kwa ajili ya matatizo ya Watendaji wa Halmashauri. Nadhani kwenye Halmashauri, mtu ambaye ameteuliwa na Uongozi wa Juu, Waziri Mkuu ni Mkurugenzi. Bado Baraza la Madiwani linaweza likamjadili Mkurugenzi hata kama hawawezi kumfukuza kazi, lakini wale wengine wote wapo chini ya Halmashauri.

Baraza la Madiwani lina mamlaka kisheria, kama ni wezi, hatujazuliwa kuwafukuza. Ninachooomba ni utaratibu wa kuwaondoa hawa wezi na Serikali isiwang'ang'anie wakati wamebainika kwamba ni wezi. Siyo jambo la kumtuhumu Waziri au Waziri Mkuu kwa Viongozi walioko chini ya Halmashauri. Hilo naomba tukirudi tuwe wakali kwa wale wezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la *TASAF*. *TASAF* imefanya kazi nzuri sana katika baadhi ya maeneo, lakini kuna maeneo mengine ambayo imekuwa ni kichaka cha wizi. Naomba ukaguzi wa hizi fedha za *TASAF* katika maeneo ambayo hayakufanya vizuri, kwa sababu ni fedha ambazo zinalenga Wananchi wa hali ya chini. Tusikubali hizo fedha ziliwe na wajanja. Tuzisaidie Halmashauri hizo ili hizo fedha zifanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Jambo lingine ni Viwanja vya Serikali pamoja na Majengo ya Serikali. Kuna viwanja vya Serikali ambavyo vimezagaa tu havikuendelezwa, ndiyo vinavamiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MICHAEL L. LAIZER]

baadaye na watu. Hivi ni kwamba Serikali imekosa fedha za kuendeleza maeneo hayo? Kuna viwanja vingine havina hata hati. Kuna majengo ya Serikali yaliyoko ndani ya miji, hata ukienda Dar es Salaam, yamechakaa hayafai.

Hivi jamani, ukiona Jengo la Serikali ambalo limechakaa lipo ndani ya mji; hivi ni kwa nini; Serikali imeshindwa kuendeleza? Kama imeshindwa, si iuze. Sitegemei kama Serikali inashindwa kuendeleza majengo yaliyoko ndani ya miji, ni kwamba haijapangilia. Naomba majengo kama hayo yaendelezwe na wakati mwingine viwanja ambavyo vipo lakini havina hati, vitafutiwe hati. Majengo ambayo yamechakaa, waruhusiwe *National Housing* wayaendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini bado nasisitiza kwa Wabunge wenzangu kwamba, suala la Muungano tulidumishe. Suala la Katiba tujadili vizuri na Wajumbe wengine wanaoingia katika Bunge hili, tusiwaambukize ugonjwa huu wa siasa. Ilishie katika Bunge hili na kama mnataka kuendeleza, endelezeni baada ya kumaliza hili suala la Katiba, lakini suala la Katiba tulimalize vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimpe nafasi Waziri Kivuli wa Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia na mimi hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uwasilishaji wa Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati alilieleza Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilipata fursa ya kutembelea nchi kadhaa za Kiafrika kwa lengo la kujifunza juu ya utaratibu mbalimbali wa Kikatiba katika nchi hizo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema kwamba, Kamati ilikwenda Zimbabwe, Kenya na Ghana na tulijifunza mambo mengi sana. Naomba nichangie katika hayo mafunzo ambayo Kamati yako ya Katiba, Sheria na Utawala iliyapata katika hizo nchi tatu na tuyatafakari tuone ni kiasi gani tunaweza tukayatumia katika utaratibu wetu wa namna ya kupata Katiba mpya na kitu gani kinaweza kikatokea baada ya kupata Katiba mpya kama ambavyo tumedhamiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya na Ghana zina mafunzo makubwa sana kwetu, hata Zimbabwe kama nitakavyoonesha *shortly*. Zina mafunzo makubwa sana kwetu katika utaratibu wa kuweka utaratibu mpya wa Kikatiba kwa njia hii ambayo ni tofauti na njia za zamani za kutengeneza Katiba mpya.

Moja ya vitu muhimu ambavyo tulijifunza ni kwamba, kupata Katiba mpya siyo mwisho wa safari. Kupata Katiba mpya ni mwanzo tu wa safari ya kujenga nchi upya kulingana na matakwa ya Katiba mpya. Kwa hiyo, ni muhimu tunapofikiria utaratibu mpya wa Kikatiba, tusifikirie tu namna ya kuipata hiyo Katiba mpya, lakini vilevile tufikirie maisha ya siku baada ya Katiba hiyo mpya kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri wa hizi nchi tatu; Katiba mpya ya Ghana ilitungwa mwaka 1992, ina miaka 21 leo. Mara baada ya Katiba mpya ya Ghana kutungwa, Serikali ya Ghana ilipewa na Katiba mpya hiyo muda wa mwaka mmoja ili kuweka utaratibu mpya wa Kisheria na utaratibu mpya wa Kitaasisi, kulingana na matakwa ya Katiba mpya.

Kwa hiyo, katika hicho kipindi cha mwaka mmoja, Sheria zote ambazo zilikuwa haziendani tena na utaratibu mpya wa Kikatiba, zilifutwa au kufanyiwa marekebisho. Taasisi mpya zilizokuwa zimeundwa na Katiba mpya ziliundwa katika kipindi hicho, Taasisi za zamani ambazo zilikuwa zimeundwa zamani lakini zinaendelea kwa mujibu wa Katiba mpya katika mazingira mapya vilevile zilifanyiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

marekebisho, Maafisa wapya kuteuliwa na vitu kama hivyo. Kulikuwa na muda wa mwaka mmoja baada ya Katiba mpya kupatikana, kwa ajili ya kuiweka nchi katika mazingira ya kwenda sambamba na matakwa ya hiyo Katiba mpya. Mheshikiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kenya, Kenya walijipa miaka miwili na nusu. Katiba ya Kenya ilipatikana Agosti, 2010. Kuanzia Agosti, 2010, ndani ya Katiba mpya yenyewe kulikuwa na vifungu vilivyoelekeza utaratibu wa namna ya kufanya marekebisho mbalimbali ya Sheria ya Taasisi, namna ya kupata Viongozi wapya wa Taasisi na vitu kama hivyo. Ndani ya miaka miwili na nusu, kazi ilifanyika ya kuhakikisha nchi inakuwa na utaratibu unaolingana na utaratibu ulioko katika Katiba mpya. Ndiyo maana baada ya hicho kipindi cha miaka miwili, uchaguzi umefanyika katika mazingira mapya kabisa na nchi inasonga mbele.

Katika hizi nchi mbili, kuna kitu muhimu sana ambacho tumejifunza; umuhimu wa Bunge. Katika Nchi ya Kenya, baada ya Katiba mpya kupatikana, Kamati kubwa kuliko zote katika Bunge la Kenya, Kamati yenye nguvu kuliko Kamati nyingine yoyote ndani ya Bunge, inaitwa Kamati ya Utekelezaji wa Katiba mpya (*Constitution Implementation Oversight Committee*). Hiyo Kamati ina Wajumbe 52 pamoja na Mawaziri. Mawaziri karibu 14 au 15 hivi ni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Katiba mpya. Ni Kamati yenye nguvu kuliko Kamati nyingine zozote.

Vilevile Vyombo vya Kikatiba vipya, kuna Tume ya Utekelezaji wa Katiba, kuna Tume ya Urekebishaji wa Sheria kama *Law Reform Commission* ya kwetu, lakini ya Kenya imepewa meno mapya ili kusimamia utekelezaji wa Kamati. Bunge lenyewe, hii Kamati tunayoisema *Constitution Implementation Oversight Committee (CIOOC)* ni Kamati ya Bunge. Utaratibu wa namna ya kutunga sheria ndani ya Bunge lenyewe umebadilika kabisa.

Kwa hiyo, kwa mfano, Kenya, hii Miswada ya Sheria ili uwe Muswada wa Sheria lazima uende kwanza kwa Maspika wa Bunge, ina *Chamber* mbili za Bunge. Kwa hiyo, Muswada wa Sheria unaotoka Serikalini au unaotoka ndani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

ya Bunge, unaenda kwanza kwa Maspika wa Bunge wanauangalia, wakiridhika ndiyo unachapishwa katika Gazeti la Serikali unaletwa ndani ya Bunge. Ndani ya Bunge, Muswada unapita katika hatua zote unapitishwa na Viongozi wa Bunge. Kwa hiyo, kazi ya kutunga Sheria, imekuwa ni kazi ya Bunge na Bunge limekuwa linapatiwa nguvu sana.

Vivyo hivyo katika Nchi ya Ghana ambayo kwa mujibu wa Katiba yao, angalau nusu ya Mawaziri wanatoka Bungeni na nusu nyingine wanatoka nje ya Ubunge, siyo Wabunge. Kwa hiyo, ukiangalia Mabunge ya nchi hizo mbili, yamekuwa na nguvu kweli kweli. Yana uwezo wa kutekeleza wajibu wao Kikatiba, kwa sababu ya utaratibu wa Kikatiba ambao umewekwa katika hii *New Constitutional Order*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ambayo nayasema, nimesema ni mafunzo ambayo tunahitaji kujifunza. Siyo lazima na naomba nieleweke, siyo lazima kilichofanya kazi vizuri katika nchi jirani kifanye vizuri kwetu. Vilevile, huwezi ukapuuza kinachoendelea kwa jirani yako hasa kama mifumo yenu ya Kikatiba na Kiutawala inafanana. Tanzania, mfumo wetu wa Kikatiba na wa Kisheria, unafanana na hizi nchi ambazo tumezitembelea. Sisi wote mfumo wetu wa Kikatiba na wa Kisheria, ni mfumo wa *Common Law*. Kwa hiyo, ni vizuri kujifunza haya ambayo tumeyasoma. Tuangalie kipi kinawekwa na kipi hakiwekwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatingisha kichwa sijui anatingisha kwa sababu ya ninachokisema hiki au la. Naomba niseme tu kwamba, katika nchi yetu, mwaka 1984, miaka karibu 30 iliyopita, tulifanya mabadiliko makubwa sana ya Kikatiba. Mabadiliko yaliyoingiza Hati ya Haki za Binadamu katika mfumo wetu wa Kikatiba. Miaka yote kabla ya 1984, hatukuwa tunatambua haki za binadamu Kikatiba, lakini mwaka 1984, tulipofanya mabadiliko hayo makubwa, Serikali ilipewa muda, ukiangalia hiyo *Bill of Rights*, Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

ilijipa muda wa miaka mitatu wa kubadilisha Sheria zote ili ziendane na *Bill of Rights*.

Kwa sababu ya kutokuweka Taasisi za kuhakikisha kwamba hilo linafanyika, matakwa ya *Bill of Rights* ya kusafisha nyumba Kisheria miaka mitatu, hayakutekelezwa kabisa. Matokeo yake, tumeendelea kuwa na Sheria kama hii tuliyokataa kuifanyia marekebisho juzi; Sheria ya Magazeti. Sheria ambazo ni za Kikoloni zinaenda kinyume kabisa na *Bill of Rights*, kwa sababu hatukuweka utaratibu mzuri wa namna ya kuhakikisha matakwa ya Katiba mpya yanatekelezwa.

Baadaye wakati tunaingia katika Mfumo wa Vyama Vingi mwaka 1992, vilevile tulifanya mabadiliko makubwa sana ya Kikatiba. Mabadiliko ambayo yalitungiza katika Mfumo mpya wa Siasa za Ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Ripoti ya Tume ya Tume ya Rais ya Chama Kimoja au Vyama Vingi, Ripoti ya Tume ya Nyalali, iliweka utaratibu utaratibu na Ratiba ya kuhakikisha namna gani tutaingia katika Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi. Ripoti ilielezea hatua za kufanya na muda gani zifanyike. Ie Ripoti ilikuwa *detailed* sana, ilikuwa na mapendekezo mengi sana mazuri juu ya namna ya kwenda huo mwaka wa kwanza baada ya kuingia katika Mfumo wa Vyama Vingi. Pamoja na kuondoa Sheria zilizopitwa na wakati, kutunga Sheria mpya, Kuunda Taasisi upya, mapendekezo yalikuwa mazuri sana, lakini yalikataliwa kwa sababu hatukuweka utaratibu wa Kitaasisi wa kuhakikisha tunatekeleza matakwa ya Katiba mpya.

Sasa hili jambo ni muhimu sana. Kama tunatunga Katiba mpya ili tubadilishe kabisa mfumo wa namna tunavyojitawala, *it will never be business as usual*, kama Katiba mpya ni mpya kweli kweli haiwezi ikawa biashara kama ya jana na ya juzi. Lazima iwe biashara tofauti kabisa, kwa utaratibu tofauti kabisa na ili hiyo iwezekane, inabidi tuangalie utaratibu wa namna ya kutekeleza hiyo *New*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Constitutional Order itakayokuwa imezaliwa na Katiba mpya. Ni muhimu tukajifunza kwa sababu tumepita katika mkondo huo huo, tumeshindwa mwaka 1984, tukashindwa mwaka 1992/1993 tukirudia tena makosa kwenye Katiba hii sasa hivi, tutakuwa hatujajifunza lolote kutokana na historia yetu ndefu ya zaidi ya nusu karne katika kutengeneza Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizingumzie suala moja la mwisho kuhusiana na huu utaratibu wa namna ya Taifa kujizaa upya. Kwa vyovyote vile, kama nilivyosema, mambo hayatakuwa kama ambavyo yamekuwa siku zote. Kwa vyovyote vile, hatutaweza kuendelea kufanya mambo kama ambavyo tumekuwa tunayafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mjumbe mmoja amependekeza kwamba, tubadilishe utaratibu tusingize siasa, utaratibu wa Katiba. Kitu cha kwanza juu ya Katiba ni Waraka wa Kisiasa. *A Constitution is a fundamental political document*, ni Waraka wa Kisiasa *Number One*. Huwezi ukaepuka siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu muhimu ni kwamba, Waraka huu wa Kisiasa *Number One* lazima kama Taifa tuuridhie wote. Matatizo yanaanza pale ambapo Waraka wa Kisiasa mkubwa kama Katiba unakuwa ni Waraka wa upande wa mmoja. Tuangalie utaratibu wa kuhakikisha kwamba, huu Waraka wetu wa Kisiasa tunaoutengeneza kama Taifa, kweli unakuwa ni Waraka wa Taifa na siyo Waraka wa upande huu au wa upande ule katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu, ahsante sana. Anayefuata katika uchangiaji wetu ni Mheshimiwa Waziri George Mkuchika, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Wasira. Mheshimiwa Mkuchika!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Taarifa hizi mbili.

Moja, kulikuwa kuna hoja, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kazi ya Sekretarieti ya Maadili ni nini mbona hatuna mrejesho. Maelezo; Kazi ya Sekretarieti ya Maadili kwa Mujibu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara 132 ya Mwaka 1997 inasema: Moja, kupokea Hati na Tamko la Mali za Viongozi na kufanya uhakiki. Pili, kuchunguza tuhuma ya kuvunjwa kwa maadili na Viongozi wa Umma. Tatu, kupokea na kuchunguza malalamiko yoyote kuhusu Kiongozi yeyote wa Umma, kwa mdomo au kwa maandishi. Nne, kuwasilisha kwa Mheshimiwa Rais, mapendekezo ya Baraza Maadili kuhusu uchunguzi wa tuhuma zilizokiukwa.

Ninyi ni mashahidi mnalisikia katika Vyombo vya Habari, Baraza la Maadili hivi karibuni lilifanya kikao kule Tabora, yale waliyoyaona kule yanawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, swali lingine liliulizwa kwamba kwa nini hakuna mrejesho wa kazi za Sekretarieti ya Maadili ya kila mwaka. Maelezo ni kwamba, mrejesho, matakwa ya Sheria inataka kila mwaka shughuli zao zipelekwe taarifa kwa Mheshimiwa Rais na nakala kwa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fomu ya tamko la mali na madeni kwanza uhakiki unafanyika na wale wenye hitilafu hupelekwa kwenye Baraza la Maadili. Ukiona kimya, umejaza fomu umepeleka fomu hujaitwa, maana yake ni kwamba hatujaona hitilafu. Kwa hiyo, kama ndugu yangu aliyekuwa anauliza Mheshimiwa Felix Mkosamali hujaitwa,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)]

maana yake mpaka sasa mambo yako mazuri, nakuombea yaendelee kuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulitolewa hoja kuhusu kada za Uhasibu, alishauri ndugu yangu pale Mkosamali kwamba, Watumishi wa Uhasibu na Manunuzi waongezwe katika orodha ya Viongozi wa kutoa tamko la mali. Maelezo ni kwamba, Sheria ya Maadili chini ya Kifungu cha (7), Mheshimiwa Rais amepewa uwezo wa kuongeza Viongozi wa kutangaza mali.

Mheshimiwa Rais, kwa kutumia kifungu hicho, mwezi Septemba, 2013 kupitia Tangazo la Serikali Namba 260 la tarehe 6 Septemba, 2013, Mheshimiwa Rais alifanya hivyo na Wahasibu na Maafisa Ugavi ni miongoni mwa watu walioongezwa katika orodha kama Mheshimiwa alivyoshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ilikuwa kwamba, Mheshimiwa Felix Mkosamali alitoa ushauri pia kuwa TAKUKURU wawe wanashauri na kufanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ushauri tumeupokea ni mzuri. Hata hivyo, napenda kutoa taarifa kwamba, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), imeandaa mafunzo kwa Wajumbe wote wa Kamati za Ushauri za Mikoa, ambapo wanapata mafunzo kuhusu Sheria ya Kupambana na Rushwa na baada ya hapo tutaendelea katika Mabaraza ya Madiwani. Kwa mfano, Siku ya Ijumaa, tarehe 6 Desemba, 2013 tuliendesha mafunzo hayo ya masuala ya rushwa kwa Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Kigoma, ilikuwa nzuri sana, walihamasika sana na baada ya pale wameazimia kila Baraza la Madiwani lipewe mafunzo kama waliyopata katika Baraza la Ushauri la Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kusema kwamba, pamoja na kupokea na kuchunguza malalamiko dhidi ya vitendo vya rushwa, kazi nyingine ya TAKUKURU ni kuelimisha. Kwa hiyo, natoa wito kwa Ofisi mbalimbali za Serikali, Madhehebu ya Dini, Vyama vya Hiari kadhalika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)]

hata Vyama vya Michezo na Jumuiya za Chama, naomba mnapofanya semina zenu, waalikeni na Viongozi wa TAKUKURU watoe mafunzo kuhusu vita dhidi ya rushwa, kwa sababu kazi ya kuelimisha ni mojawapo katika kazi walizopewa TAKUKURU kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono Hotuba zote mbili za Kamati hizi. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Stephen Wasira, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nitumie nafasi hii kuishukuru Kamati na kuunga mkono hoja zilizotolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Vilevile nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi wa mambo machache ambayo yametokana na mjadala wa Hotuba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mchache yaliyotokana na mjadala huo, yametokana na kauli ya Mheshimiwa Felix Mkosamali, ambaye yeye ameuliza MKURABITA itamaliza lini kazi ya kupima ardhi. Mimi nataka kusema, ardhi yote ya Tanzania haiwezi kupimwa na MKURABITA, inaweza ikapimwa kwa utaratibu maalum. Kazi ya MKURABITA ni kuwezesha Halmashauri za Wilaya, kuzijengea uwezo kwa kufundisha na kuzipatia vifaa ili wale vijana wanaofunzwa kule waweze kufanya kazi ya kupima ardhi na kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, ramani zote zitakazotokana na upimaji ule ziweze kupata kibali cha Wizara ya Ardhi. Baada ya hapo, tunatoa hati kwa wahusika ambao wamepimiwa ardhi na ardhi ile ikarasimishwa. Kwa hiyo, tukitegemea MKURABITA ipime vijiji 10,000 vya Tanzania, haitawezekana.

Halmashauri za Wilaya zikiwezesha nazo zikatoa suala la upimaji wa ardhi kama kipaumbele katika bajeti

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

zao, tutaweza kupima ardhi yote ya Tanzania katika muda mfupi unaowezekana. Nimetembelea Mkoa wa Kagera na nimeshuhudia baadhi ya Halmashauri ambazo zimejiandaa na kuweka taratibu nzuri za kupima baada ya kuwa MKURABITA imeonesha mfano.

Kwa hiyo, mimi nadhani huo ndiyo mfumo tutakaotumika na wala ambao hawajafikiwa, wakiweza kufikiwa wajiandae vizuri ili Halmashauri iwe mdau katika kazi hii. Hata Wizara ya Ardhi yenyewe kupima ardhi yote ya Tanzania imekuwa ngumu, sembuse *Unit* ndogo inaitwa MKURABITA ambayo watu wake ni wachache sana. Hata hivyo, imejitahidi, imeshafikia zaidi ya Wizara 50 nchini na bado kazi inaendelea.

Kwa hiyo, nilitaka kuweka hilo sawa ili tuisubiri MKURABITA ufanye kazi hii, lakini tuitake MKURABITA iziwezeshe Halmashauri zetu zifanye kazi na Halmashauri zile zifuatilie baada ya hapo ili tuweze kupima ardhi yetu na kurasimisha kwa manufaa ya watumiaji.

Vilevile alisema kwamba, zile hati zinazotolewa na MKURABITA hazikubaliki kwa vyombo vya fedha. Ukweli ni kwamba, vipo vyombo vya fedha ambavyo vinazikubali. Kwa mfano, Benki ya *CRDB* imewahi kutoa mikopo kwa hati hizi hizi katika Wilaya ya Mbozi na imefanya vizuri. Wakulima wa Chai kule Njombe wanapata mikopo kutokana na hati hizi. Vilevile katika Wilaya ya Misungwi kuna mtu alipata hati hii na akatafuta mkopo wa treka na akakubaliwa. Benki ya *NMB* sasa hivi inakwenda kufanya kazi hiyo katika Wilaya ya Tandahimba na katika Mikoa ya Kusini ambayo tumeamua wafanye iwe mahali pa majaribio na benki imekubali kufanya hivyo.

Sasa benki zipo nyingi Tanzania, kila moja inaweza kuwa na mtazamo tofauti. Kazi yetu ni kuzifanya Benki hizi ziamini kwamba, hati hizi ni za kisheria kama zilivyo hati zinazotolewa na Wizara ya Ardhi.

Nilitaka kuliweka hilo vizuri na sidhani kama tunahitaji

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

marekebisho ya Sheria kabla hati hizi hazijaanza kupokelewa. Kwa sababu zinapokelewa sasa hivi na zinatumika kutoa mikopo.

Mheshimiwa Felix Mkosamali, alizungumzia kitu kinachoitwa *Big Results Now* na hili lilisemwa tangu jana na akataka mikataba inayowekwa baina ya Wizara na Rais iletwe Bungeni. Nadhani ndugu yangu Mkosamali, tulishaelezana sana juu ya *Big Results Now*. Yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na ndiyo inayosimamia jambo hili. Tumeshasema kwamba, mkataba kati ya Waziri na Rais ni wa kumwezesha Rais kusimamia kazi ambayo ni ya Serikali, lakini mfumo mzima wa Serikali unawajibika Bungeni.

Kwa hiyo, ule mkataba kati ya Rais na Waziri ni wa kumwezesha Rais kuhakikisha kwamba, yale waliyokubaliana yanatekelezwa. Sasa tulete Bungeni Mkataba wa kusema nini? Sisi tunafikiri tunachotakiwa kuleta Bungeni ni masuala mazima, maana Bunge ndiyo linatoa fedha kwa Miradi hiyo ambayo inasimamiwa na *Big Results Now*. Kwa hiyo, kama Serikali tunakuja kuwajibika Bungeni kwa kueleza tulipewa fedha kiasi hiki utekelezaji umekwenda kiasi kile. Hilo ndilo la msingi zaidi na ndiyo uhusiano wa Serikali na Bunge katika uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwamba tunamwuliza Waziri wa Nishati lete mkataba wako na Rais. Sasa mkataba wake na Rais acha wajuane na Rais na Rais anataka yule afanye kazi waliyokubaliana halafu aje aripoti Bungeni. Kama haikufanyika vizuri, Bunge lina haki sasa ya kuhoji, kwa nini mlisema mtafanya hiki hamkufanya. Mimi nadhani hapo ndipo tunaweza tukagawana kazi hizi. Tukitaka kila kitu kifanywe na Bunge, sasa itakuwa Serikali haipo, Bunge litachukua kazi ya Serikali, halafu litawajibika kwa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo limezungumziwa linahusu *TASAF* na hili limezungumziwa na Mheshimiwa Lekule Laizer. Kwanza, nataka kukubaliana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

naye kwamba, *TASAF* imefanya kazi nzuri sana nchini hapa. Wote ambao wanatoka kila mahali wanajua kwamba kuna shule, kuna zahanati, kuna Miradi ya Maji na kuna barabara, zimejengwa na Wananchi wenyewe kwa kusaidiwa na *TASAF* na rekodi safi kabisa ya kazi hii.

Vilevile kila kuliko na mafanikio hapakosi matatizo. Mheshimiwa Lekule Laizer amesema, baadhi ya Miradi ya *TASAF* haikutumika vizuri. Nami ninakubaliana naye na popote ambapo Waheshimiwa Wabunge mnajua kwamba, ubadhirifu umefanyika wa fedha hizi za *TASAF*, tupeni taarifa na tutachukua hatua. Kwa sababu haiwezekani tukatoa kwa ajili ya matumizi ya Wananchi kupata maendeleo halafu watu wachache wakazivuruga. *TASAF* ilikuwa na mtu maalum wa *TASAF* kila Wilaya, ilipokuja *TASAF II* tuka-*compromise* na mfumo wa *Local Government* kwa sababu ya *D by D* kwamba, sasa Halmashauri zitachukua nafasi yake na Miradi hii itaenda kusimamiwa na Halmashauri.

TASAF II ndiyo imekuwa na fedha nyingi na ndiyo imekuwa na Miradi mingi. Kwa hiyo, inawezekana kuna mahali ambapo makosa yametendeka na tukipajua pale tutafanya *auditing* kama alivyopendekeza Mheshimiwa Laizer.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema *TASAF III* sasa imeanza na hii itakuwa tofauti na *TASAF I*. Bado tutaendelea kushughulika na Miradi kama ambayo tunaifanya, lakini mkazo mkubwa utawekwa katika kuinua familia maskini. Tanzania tunazo familia maskini sana, kati ya watu 12,000,000 ambao wapo katika mazingira maskini bado ndani yao wapo maskini wa maskini (*poorest of the poor*). Kwa hiyo, wale ndiyo tunataka kuinua kipato chao kwa kuwasaidia. Hawa hawawezi kupeleka watoto shule, hawa wanaogopa shule kwa sababu hawawezi kununua *uniform*, hawa hawaendi hospitali kwa sababu wanaogopa kumlipa Daktari lakini ni Watanzania wenzetu.

Kwa hiyo, tunataka kufanya kazi ya kuhakikisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

hawa maisha yao yanainuka. Tutakapopata nafasi tutawapa semina Wabunge wote ili waelewe vizuri *TASAF III* inakusudia kufanya nini kwa familia 12,000,000 katika muda wa miaka miwili iliyobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nadhani ufafanuzi huo utasaidia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wasira, ahsante sana. Sasa naomba nimpe nafasi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Werema, atafuatiwa na Mheshimiwa Lukuvi.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nizungumze maneno mawili, matatu. Nianze ambalo ni rahisi zaidi na ni ushauri tu. Namshauri Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwenye ukurasa wa 30 na 31, pale maoni ya jumla ni haya aliyosema Mheshimiwa Wasira, maneno yanayotumika kuagiza, badala ya maneno ya kusema Kamati inaagiza wangeweza tu kusema Kamati inashauri, kama maneno yaliyotumika kwenye Katiba. Ukurasa wa 31 pale panaposema katikati ya sentensi ya mwisho ile; “hakika Kamati haitasita kuzichukulia hatua Halmashauri zilizokiuka Msingi wa Utawala Bora katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.” Nadhani hiyo siyo kazi ya Kamati, wangeweza kutafuta maneno mengine badala ya hayo. Ni ushauri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni hili ambalo leo asubuhi Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, amesema kwamba, Serikali haina dhamira ya kulishughulikia suala ambalo sasa linaitwa Mabilioni ya Uswisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikutaka kusimama, lakini kwa sababu maneno haya ni mazito, ninaomba na mimi kusema kidogo. Maneno haya aliyosema Mheshimiwa Zitto

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Kabwe na bahati mbaya simwoni, hayafanani kabisa na tabia yake, mwenendo wake na kauli zake mbele ya Kamati. Leo Mheshimiwa Zitto Kabwe, anataka tuangalie mfumo badala ya majina. *(Makofi)*

Nakumbuka kwenye Bunge la Tisa, tulibishana hapa na mimi nilikuwa nasema tuangalie mfumo, lakini Mheshimiwa Zitto akasema, umefika wakati wa kwake yeye kutoa dukuduku lake, atoe Taarifa alizonazo na nyaraka alizonazo ili watu hao washughulikiwe. Sasa leo tofauti, kutokana na kauli ya Mheshimiwa Zitto Kabwe, Bunge lilitoa hadidu rejea. Moja ya hadidu rejea ni kuchunguza na kubaini majina ya Watanzania wanaodaiwa kuwa na fedha nje ya nchi kinyume na Sheria. Pili, ilikuwa kuchunguza kama fedha hizo ni haramu. Tatu, kutambua Benki ambako fedha hizo zipo. Nne, kuandaa mashitaka. Tano, kuishauri Serikali. Sasa ukisema mfumo leo ukigeuza ukasema mfumo, sisi *chapter* ya mfumo hii hapa. Ninayo *chapter* ya mfumo na ninayo *chapter* ya ushauri, ninachokosa yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie, tarehe 25 Februari, 2013, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Zitto Kabwe hapa Dodoma Ofisini kwangu pale Ofisi za Bunge, akasema ana taarifa na ana nyaraka. Akatoa masharti mawili kwamba, ahakikishiwe na Bunge kwamba, hakuna mtu atakayemsonga baada ya kutoa hizo taarifa. Pili, kwamba kuwe na kiapo, yaani mimi nitoe kiapo kwamba, ikigundulika ni uongo basi yupo *free*.

Tarehe 23 alitukwepa hapa Mheshimiwa Zitto Kabwe akaenda Kambi ya JKT Tanga. Tarehe 22 Machi, tulikwenda Tanga kwenye Kambi, baada ya kushauriana pale tukaona kweli ngoja kwanza amalize mafunzo yale halafu tutamwona Dar es Salaam naye akasema atakuja hakuja.

Tarehe 12 Aprili, tukakutana tena Dodoma akasema alikuwa anajiandaa kwenda South Africa anahitaji muda, hakuhojiwa. Tarehe 4 Mei, tukakutana nae kwenye Viwanja vya Bunge hapa, katikati ya mahojiano

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Bunge lilikuwa linaendelea, akasema ana hoja yenye masilahi ya Taifa. Kamati ikasema nenda basi utarudi hakurudi. Alipotafutwa akasema yupo Dar es Salaam ameshaondoka Dodoma na kwamba, alikuwa anajiandaa na Kongamano la Kigoda cha Mwalimu. *(Kicheko)*

Kamati ilikwenda Dar es Salaam, Mheshimiwa Zitto Kabwe akasema, hakuwa na nafasi kwa sababu alikuwa anajiandaa kusaidia Timu ya Taifa ya Mchezo wa Mpira. Tarehe 18 Juni, sasa Sheria ichukue mkondo wake, tukachukua maelezo ya Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa kiapo chini ya Kifungu cha 7 (1) na Kifungu cha 9 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Ndipo Mheshimiwa Zitto Kabwe akasema, hakuwa na jina au akaunti ya Mtanzania yeyote aliyeficha fedha nje ya nchi. Chini ya kiapo, asubuhi ya leo Mheshimiwa Zitto Kabwe amesimama hapa anasema Serikali haina dhamira na sasa ameondoka na ukimtafuta sasa hivi hayupo tena hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mheshimiwa Zitto Kabwe ni mzito. Ninakubaliana na Mheshimiwa Lema, maneno aliyosema asubuhi kwamba, alete taarifa lakini sasa sisi tunafanya kazi hii kama vile haitokani na Azimio lililotokana na maneno ya Mheshimiwa Zitto Kabwe. Tumeingia kuifanya kazi hii kama Serikali na tunachoomba, sikutaka kulisema hili kwa sababu sidhani kama ni utaratibu mzuri, ni muda wa kuendelea kutafuta taarifa za watu bila kumwonea mtu yeyote. Ninarudia, bila kumwonea mtu yeyote. Afadhali watu wahalifu mia moja waende huru kuliko kumwonea mtu mmoja asiyekuwa na hatia. Mimi kama Kiongozi wa Kamati hii, nitasimamia hilo. Kama nitaonekana sifai kwenye kazi hii, sawa bado ninao ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge 87 waliofika kwenye Kamati. Ninawashukuru pia Watanzania waliofika kwenye Kamati na taarifa zao nyingine zimetusaidia kupiga hatua. Ninayashukuru pia Mashirika ya Mataifa na nchi rafiki zinazoendelea kutusaidia ili tuweze kupata taarifa hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Tulipofikia siyo kubaya. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuomba muda, uiruhusu Serikali ifanye kazi hii na hili la Mheshimiwa Zitto tutashughulika nalo kisheria. Kwa sababu huwezi kusema uongo Bungeni na ukasema uongo kwenye Kamati ukaenda hivyo hivyo, haitawezekana. Kwa hiyo, naomba muda, tunadhani kwa kazi hizi tulizofanya, mianya tumeshaiona na mambo mengine tumeshaiambia Serikali, yanaihusu Serikali, tunadhani ukituongeza muda wa miezi sita, tutakuwa tumemaliza hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kutusikiliza. Mwisho, naishukuru sana Kamati ya Uchunguzi na Vyombo vya Uchunguzi, ambavyo vinafanya kazi usiku na mchana na nina hakika tutafika mahala ambapo Watanzania watakuja kutuelewa na tutakuwa tumeitendea haki nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lukuvi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, nafikiri Mheshimiwa Zitto sasa ameelewa kwa nini jana nilisema naomba muda, maana alianzia kwenye kauli yangu sasa ameelewa.

Mimi naomba nitoe ufafanuzi kidogo juu ya jambo lingine ambalo Mheshimiwa Zitto amelisema linalohusu matumizi ya *biometric kits*, ambayo yamekusudiwa kuagizwa na kutumika nchini kwa ajili ya uandikishaji, siyo upigaji wa kura kama alivyosema yeye, uandikishaji wa wapiga kura.

Kwanza, naomba nizishukuru sana Kamati zote mbili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

zilizowasilisha Taarifa, lakini zaidi Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo ndiyo inasimamia shughuli za Waziri Mkuu. Tumeshirikiana sana, tunajua tuna shughuli nyingi nao, lakini tumeenda vizuri sana; tunawashukuru sana kwa kazi kubwa mliyoifanya.

Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Jaji Lubuva, naunga mkono maneno yake aliyosema juzi kwenye Vyombo vya Habari. Amesema wazi kwamba, Tume ya Uchaguzi ni Tume Huru, haingiliwi na chombo chochote wala Taasisi yoyote. Hili nilitaka Mheshimiwa Zitto ajue kwamba, yale aliyosema yanahusu Tume Huru ya Uchaguzi hayamhusu Waziri wa Nchi aliyekuwa anamsema yeye. Kwa sababu Waziri wa Nchi siyo Waziri wa Tume ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi ni chombo huru na mlipopitisha Bajeti hapa mlipitisha Bajeti ya *Vote* ya Tume ya Uchaguzi.

Kwa hiyo, naunga mkono sana maelezo ya Mheshimiwa Jaji Lubuva na ni kweli tumekuwa tunafanya kazi namna hiyo, tukijua kwamba, Tume ya Uchaguzi ni Tume huru. Hata haya anayosema yameharibika walifanya wenyewe na walijua wanachokifanya na watarekebisha wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba, uandikishaji wa wapiga kura wa *biometric* unaokusudiwa na Tume, umelenga kuchukua taarifa zile zile zilizochukuliwa na Tume awali, kwa teknolojia ambayo itawezesha kupata daftari sahihi zaidi. Zipo nchi mbalimbali zilizotumia teknolojia ya *biometric* katika uandikishaji wa wapiga kura.

Nasema uandikishaji, Mheshimiwa Zitto, yeye alisema upigaji wa kura. Tume ya Uchaguzi hainunui teknolojia hii kwa ajili ya kupiga kura, yenyewe inachukua kwa ajili ya waandikishaji wa daftari la wapiga kura basi. Hizi *kits* ni za waandikishaji na wala havitahusiana na mambo ya upigaji wa kura.

Nchi mbalimbali zilizofanya utaratibu huu ni Nigeria mwaka 2007, Guinea Mali 2005, Uganda 2008, Zambia 2008,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Afrika ya Kusini na Zanzibar. Nigeria ilifanikiwa kuandikisha wapiga kura 70 milioni kwa kutumia *kits* hizi za *biometric* kwa siku 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kwamba, *biometric registration* ni mfumo unaolenga kuwaandikisha wapiga kura kwa haraka na kuwa na daftari lililo sahihi zaidi, kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, utawezesha wapiga kura kuwa na wapiga kura wote waliojiandikisha. Pili, taarifa zitakazochukuliwa hasa alama za vidole kwa kutumia *kits* hizi kupitia mfumo wa *Automatic Fingerprint Identification System (AFIS)*, itawezekana kuondoa watu wote waliojiandikisha zaidi ya mara moja. Tatu, utarahisisha uhamishaji wa Wapigakura waliohama kutoka sehemu moja na kuhamia sehemu nyingine. Kwa hiyo, hii ni teknolojia mpya kwetu, lakini itarahisisha sana kwa muda tulionao kuweza kuandikisha Watanzania wote wanaostahili na kutunza kumbukumbu zao vizuri.

Sasa ametoa mifano kwamba, Malawi shughuli hii imeharibika. Sasa nataka kumwambia kilichosababisha Malawi ikaharibika. Nchi ya Malawi haiwajahi kutumia mfumo wa *biometric* kama alivyosema Mheshimiwa Zitto Kabwe katika uandikishaji. Nchi hii hata sasa inatumia mfumo wa *Optical Mark Registration (OMR)*. Tatizo lililotokeza Malawi halihusiani na *biometric* ila lilihusiana na kukiuka Sheria katika utaratibu wa uchaguzi, mchakato wa uchaguzi. Matatizo mengine ameunganisha na Kenya. Sasa matatizo yaliyojitokeza Kenya siyo katika uandikishaji kama tunaofanya sisi, bali katika mfumo wa uhakiki wa Wapigakura (*Voter Verification System*) na katika mfumo wa kutuma matokeo (*Results Transmission System*).

Sasa katika mfumo wa uhakiki pia matatizo yalitokea katika mfumo wa uhakiki kwa kutumia *poll book* kwa upande wa Kenya. Baadhi ya Watendaji walisahau *user names* na *passwords* ya *poll books* zile walizopewa na kuamua kufanya kwa mkono, yaani kufanya *verification*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

kwa mkono. Pia baadhi ya *poll books* hazikuingizwa taarifa zote za wapigakura za kituo; hivyo, baadhi ya wapigakura hawakuweza kuthibitishwa kwa kutumia *poll books* kama katika vituo vyao.

Tatizo la tatu lilikuwa linatokana na kuchelewa kununuliwa vifaa hivyo, hizo *poll books* huko Kenya na kazi ya kuingiza taarifa ya wapigakura ilifanyika kwa haraka sana; hivyo, kusababisha baadhi ya *poll books* kutoingizwa taarifa kabisa.

Lingine lililosababisha mgogoro Kenya ni kuisha kwa umeme, umeme ulisha katika hizo *poll books* kwa haraka sana. Mwisho kabisa, kila *poll book* ilikuwa na betri ya pili, haikuwa imechajiwa kwa sababu imefika dakika ya mwisho. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo walitegemea yangefanywa kwa teknolojia, lakini wakaingiza sasa na mkono hayakufanya kazi, kwa sababu walifikiri kwamba, mfumo huu ungeweza kutoa mpaka matokeo kwa teknolojia hii. Baadaye walivyoona inachelewa na ucheleweshwaji huu ulitokana na Wafanyakazi hao hawakupata *training* ya kutosha na vifaa vimefika mwisho na vilikuwa vimefika vina hitilafu.

Sasa niseme tu kwamba, ni kweli *biometric* haijatumika hapa nchini. Tume ya Uchaguzi ilishaanza *process* ya kuagiza hizi *kits* kwa ajili ya uandikishaji. Watanzania wote wataandikishwa upya na madaftari yatatunzwa upya na tutazingatia hii Sheria ambayo vilevile tumeitunga juzi kwamba, Kura ya Maoni itapigwa baada ya uandikishaji huu kufanyika. Hapa mmeona siku 21, Nigeria wameandikisha watu milioni 70, kwa hiyo, tunahitaji muda mfupi sana wa kuandikisha Wapigakura wa Tanzania kwa kutumia teknolojia hii.

Sasa ni kweli walishatangaza, Tume ya Uchaguzi wenyewe walishatangaza kwa sababu wanayo *Tender Board* yao, wakapata mzabuni, lakini baadhi ya wazabuni walioshindwa kwenye ile *tender* walikata Rufaa *PPRA*. *PPRA* baada ya kuchunguza zile rufaa, wakagundua kweli kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

makosa makubwa yamefanyika, kwa hiyo, wamefuta matokeo ya ile *tender* na imetangazwa kwamba sasa waanze upya.

Kwa hiyo, kitakachoendelea sasa ni kuanza upya katika *process* ya kutafuta mzabuni wa kuagiza hizi *kits* za uandikishaji. Sasa hii ni *process* ya kawaida, mtu yeyote ambaye hajatendewa haki katika Mahakama fulani ya chini, lazima anakwenda Mahakama ya juu. Kwa hiyo, hata utaratibu wa manunuzi una utaratibu hizo hizo, kama hukutendewa haki mahali ndiyo maana tumeunda ile *PPRA* unakata rufaa. Wale wametoa haki siyo kwa wale waliokata rufaa lakini kwa Serikali kwa sababu pengine vingenumuliwa hivi vifaa visingekuwa na ubora au fedha zetu zingetumika vibaya. Kwa hiyo, huu ni utaratibu, mimi sijasema kwamba mpaka sasa kuna ufasidi, maana jambo hili limerekebishwa kwa kutumia utaratibu wa Sheria. Ila sasa ni jukumu la Tume yenyewe ya Uchaguzi kufanya uchunguzi ili kuona kama hitilifu hii ilisababishwa na baadhi ya Watendaji mle ndani ya Tume, Tume yenyewe itachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nieleze kwamba, *biometric kits* tunazoziagiza zitatumika tu kwa daftari la kupigia kura. Wenzetu majirani wamefanya. Daftari la kupigia kura, hizi hatukuagiza wala hatujaagiza vifaa vya kupigia kura, ila anachosema Tume yenyewe imepanga utaratibu wa kushirikisha wadau, kwa sababu hata *process* ya uagizaji itachukua zaidi ya miezi miwili.

Kwa hiyo, *process* ya ushirikishwaji wadau itafanyika, hata hapa Bungeni tumeshaandika barua ya kuomba semina kwa Waheshimiwa Wabunge. Tulifikiri tungeweza tukapata nafasi Jumamosi lakini ikipatikana sawa. Nafikiri muda umejaa, lakini bado tuna nia, Tume ina nia imeomba kuja kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge nini hasa teknolojia hii na kazi gani itafanya hapa Tanzania.

Tutakutana pia na Vyama vya Siasa ambao ndiyo Wadau Wakuu. Tume itakutana na Taaisi mbalimbali ili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

kuwaelimisha na kuwapa maoni yao kwa nini wameamua kutumia teknolojia hii na faida zake zote. Kwa hiyo, wadau wote watashirikishwa na wataambiwa matumizi sahihi ya vifaa hivi kwa ratiba na utaratibu kama utakavyoelekezwa na Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nitoe ufafanuzi huo ili Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wajue kwamba, walichokiagiza na wanachotekeleza Tume ya Uchaguzi, wala hawana nia ya kununua vifaa au teknolojia hii kwa ajili ya upigaji wa kura, isipokuwa kwa ajili ya uandikishaji wa Daftari la Wapiga Kura. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Sasa nirekebishe kidogo ratiba yangu, nampa Mheshimiwa Angellah Kairuki dakika tano, Mheshimiwa Celina Kombani dakika tano, halafu Mheshimiwa Hawa Ghasia atapewa dakika 15. Mheshimiwa Angellah Kairuki!

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia na mimi fursa niweze kuchangia hoja hii iliyoko Mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kutoa pongezi nyingi kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, pamoja na Kamati ya Tawala za Mikoa, kwa taarifa nzuri waliyoitoa, lakini pia kwa ushauri ambao wameutoa kwa Serikali katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutolea ufafanuzi hoja chache ambazo zimetolewa jioni hii. Kwanza kabisa, ningependa kutoa ufafanuzi kuhusiana na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kafulila, kuhusiana na tatizo la Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Nguruka. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Kafulila, yeye ndiyo aliyefuatilia tatizo la Hakimu huyu na mara tu alipotutaarifu, tulichukua hatua kwa kuwasiliana na Uongozi wa Mahakama kupitia Jaji Mkuu na Jaji Kiongozi. Pia kwa kushirikiana na Hakimu wa Wilaya hiyo huko Kigoma na tayari walishafanya uchunguzi na hatua mbalimbali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

zimeshachukuliwa, ya kwanza ni uhamisho na yeye amekuwa akiomba matokeo ya uchunguzi.

Niseme tu kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 40 cha *Judicial Service Act*, mtoa taarifa hana sababu ya kupewa taarifa ya uchunguzi. Niseme tu kwamba, tayari tumeshamhamisha na itakapothibitika kwamba tuhuma zile zimethibitika, basi hatua zitachukuliwa na Mahakama.

Eneo la pili ni kuhusiana na tatizo la Hakimu wa Wilaya huko Kigoma na amemtaja kwa jina kama Bwana David Ngonyale. Nalo pia hili tunalipokea kwa uzito mkubwa na kama ambavyo Kamati ya Maadili na Nidhamu za Mahakama zilivyo, kwa Hakimu wa Wilaya mamlaka ipo chini ya Mkuu wa Mkoa. Watafanya uchunguzi, Kamati ipo kabisa na wamekuwa wakifanya kazi nzuri na baadaye Mheshimiwa Jaji Mkuu, atapewa mapendekezo ya hatua gani za kuchukua.

Vilevile Mheshimiwa Kafulila, ameomba Jengo la Mahakama Kuu Kigoma. Niseme tu kwamba, nasi kwa kupitia Mahakama tunalionga tatizo hili, kwa muda mrefu wamekuwa wakienda umbali mrefu na wamekuwa wakipata huduma za Mahakama Kuu kutokea Mkoa wa Tabora. Napenda kumtaarifu kwamba, katika Mahakama Kuu ambazo tunarajia kujenga katika mwaka huu wa fedha, tunatarajia kujenga Mahakama Kigoma pia. Vilevile tunajenga na kukarabati takribani Mahakama zingine nane.

Eneo lingine ni kuhusiana na hoja za Mheshimiwa Lekule Laizer, ambaye kwa muda mrefu amekuwa akiongelea suala la ukosefu wa Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Wilaya ya Longido kwa uchungu mkubwa. Wiki iliyopita nilijibu swali kuhusiana na ukosefu wa Mahakama katika Wilaya ya Longido. Ningependa kumhakikishia kwa mara nyingine tena, katika mwaka huu wa fedha, tumeahidi na tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Longido.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

Nampongeza tena kwa sababu hivi sasa shughuli za Mahakama zinafanyikia katika Ofisi ya Mbunge. Tunalichukua kwa uzito mkubwa na Mahakama hii ya Mwanzo itajengwa na vilevile tutajitahidi kuangalia namna tutakavyopata fedha ili Mahakama ya Longido nayo iweze kujengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Laizer pia ameongelea suala la posho ya Wazee wa Mahakama kwamba ni ndogo na amependekeza iongezwe. Hata sisi pia kwa upande wa Serikali tunaliona hili. Tulianza huko nyuma kuwapa Sh. 2,500 kwa kila kesi. Kwa kweli sote tunajua ni kiwango kidogo, lakini Serikali imechukua hatua, imeongeza kiwango cha posho hadi Sh. 5,000 kwa kila kesi inayomalizika. Hivi sasa tumeenda mbali zaidi, tunataka tuangalie na vivutio vingine ikiwezekana hata Bima ya Afya ili tuweze kuwaenzi Wazee hawa wa Mahakama, ambao kimsingi wanafanya kazi kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Laizer ameongelea pia kuhusu Bunge la Katiba. Ametoa angalizo Bunge la Katiba liwe la kistaarabu na lisiwe na vijembe. Kwa kweli tumshukuru na ni angalizo kwetu sote kwani na sisi tutakuwa Wajumbe wa Bunge la Katiba. Naamini kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, kutakuwa na Kanuni zitakazoongoza Bunge hili na naamini tayari zimekwishaanza kuandaliwa. Itakapofikia wakati wa kuzipitia, wote tuzipitie kwa makini na kila mmoja azingatie majadiliano mema na yenye tija, tupate Katiba mpya itakayotutoa hapa tulipo kwenda katika miaka 50 ijayo na zaidi.

Eneo la mwisho, ningependa kujibu hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu kuhusiana na ziara ya mafunzo ambayo wameifanya Kenya, Zimbabwe na Ghana. Niipongeze sana, mmetueleza mazuri yote mliyoyapata. Kimsingi, kwa kuwa wote ni Wajumbe wa Bunge la Katiba na kwa kuwa na Mheshimiwa Tundu Lissu naye atakuwa Mjumbe wa Bunge hili la Katiba, basi itakapofikia wakati tukachangie hoja hizi ili zile Taasisi mbalimbali za ufuatiliaji wa Katiba na vyombo vingine vya ufuatiliaji wa Katiba,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

lakini pia marekebisho yatakatyotakiwa kufanyika na vyombo mbalimbali basi yaweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Celina Kombani, dakika tano!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami niwapongeze sana Kamati hizi mbili, kwa kutupa ushauri mbalimbali ambao utasaidia katika kutekeleza majukumu yetu. Nianze na hoja ya Mheshimiwa Ntukamazina na Mheshimiwa Machali kuhusu Watumishi wapimwe.

Watumishi kwa hivi sasa wanapimwa kwa Mfumo wa *Open Performance Appraisal (OPRAS)* na kwa upande wa Walimu, wao wameleta mfumo tofauti kulingana kazi zao, tunarekebisha. Kwa hiyo, *OPRAS* yao itakuwa tofauti na ya Watumishi wengine na Mtumishi ambaye hajazi fomu ya *OPRAS* kwa sasa hivi anasimamishiwa mshahara. Kwa hiyo, *OPRAS* tunaifanya kuwapima Watumishi uwezo wao. Ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge, tusiwe na tabia ya kulindana, mtu akiwa na tatizo mahali fulani achukuliwe hatua mahali husika badala ya kumlinda hasa kwa waajiri.

Suala la pili la Mheshimiwa Lekule Laizer na Waheshimiwa Wabunge wengine kuhusu zile nafasi ambazo tumesema zitaajiriwa na Halmashauri. Kweli Mheshimiwa Rais, aliipitisha ile *Miscellaneous Amendment* mwezi Juni tarehe 30 na sisi tulichofanya ni kuziambia Taasisi mbalimbali kwamba, watuletee zile kada za chini zote bila kujali ni za *Local Government* peke yake ili Taasisi zote ambazo zina Watumishi ambao ni *Operation Service*, waweze kuajiriwa na Taasisi zenyewe. Wameshatuletea, tumeshaziorodhesha na mwisho wa mwezi huu, yaani Ijumaa ya mwezi Desemba mwishoni, tutatoa kwenye Gazeti la Serikali ili Halmashauri na Taasisi nyingine ziweze kuajiri Watumishi wa kada ya chini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)]

Suala lingine ni kuhusu mishahara ya Wafanyakazi, ni ushauri mzuri kwamba, tuongeze mishahara ya Wafanyakazi na motisha mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe *formula* ya mishahara ya Wafanyakazi ni jinsi gani tunatafuta mishahara ya Wafanyakazi. Hii ni *formula* ya ILO. Ya kwanza ni gharama ya chini ya chakula kwa mwanakaya kwa mwezi. Ya pili, wastani wa wanakaya katika kaya. Ya tatu, uwiano wa gharama ya chakula dhidi ya matumizi yote ya kaya kwa mwezi. Ya nne, idadi ya wanakaya wanaofanya kazi katika kaya husika. Ya tano ni akiba ya kaya kwa asilimia kumi. Tunategemea kila kaya iweze kuwa na asilimia kumi ya akiba. Hivyo ndiyo vigezo vya ILO vya kutafuta kima cha chini au *living wage* kwa mfanyakazi.

Sasa kulingana na ILO, gharama za maisha kwa kaya ni shilingi 284,580. Sisi kima chetu cha chini ni shilingi 240,000. Kwa hiyo, utaona tofauti ni ndogo sana. Pia tunapoangalia mishahara tunakuwa na takwimu za *living wage* kulingana na miezi, kwa sababu miezi yote haiwezi ikalingana. Miezi ambayo chakula kinakuwa kingi na gharama za maisha zinakuwa chini.

Naomba nitoe tu taarifa kwamba, Kitaifa gharama za maisha ni shilingi 284,000, lakini kwa Dar es Salaam *living wage* ni shilingi 364,000 kwa miji mingine ya mijini ni shilingi 302,000 na kwa miji mingine midogo ni shilingi 266,000. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *formula* ambayo tuna-*calculate*, tunaangalia sasa kima cha chini tucheze namna gani. Kuangalia maisha ya Dar es Salaam, *urban areas* na *rural areas*, unatafuta *average* ndiyo mnapata kima cha chini cha mishahara. Kwa hiyo, hatuongezi tu kiholela bali tunatumia *statistics* kutoka *National Bureau Statistics* na pia tunatafuta vigezo vya *living wage* katika miezi husika.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo *formula* ambayo tunaitumia na upande wa motisha, motisha siyo lazima ziwe za kifedha tu, sasa hivi motisha zipo nyingi tunazozitoa kwa Wafanyakazi. Kwa mfano, mikopo, kuna mikopo isiyokuwa na riba ambayo inatolewa na Serikali kwa ajili ya nyumba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)]

na samani. Hiyo pia nayo ni motisha. Kwa hiyo, tunaangalia motisha kwa ujumla wake na ndiyo maana Bodi ya Mishahara na Motisha imeanzishwa na inafanya kazi nzuri na itatuletea mapendekezo mazuri kwa ajili ya kumotisha Wafanyakazi.

Kuhusu ajira za Watumishi, kwa kweli kwa miaka mitano iliyopita vipaumbele ilikuwa Afya, Elimu, Kilimo pamoja na Mifugo. Tumeona kwamba, tutakuwa na tatizo huko mbele ya safari la *succession plan* katika kada nyingine. Kwa hiyo, kuanzia sasa tutaajiri kada zote ambazo zina *shortage* ya *staff*, pamoja na Watumishi wa Ardhi, Mipango na Wahasibu. Pia kwa kujiandaa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kwa kuwa Watendaji wa Kata ni *Returning Officer*, kwa mwaka ujao wa fedha tutatoa nafasi nyingi sana kwa Watendaji wa Kata ili waweze kuziba mapengo yote ya kwenye Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla nakushukuru sana na nawashukuru sana wachangiaji wote ambao wametupa ushauri na sisi tunauchukua ili tuweze kuufanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Celina Kombani. Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mheshimiwa Hawa Ghasia, robo saa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami napenda niungane na wenzangu, kuzipongeza Kamati zote ambazo zimewasilisha Taarifa zao. Kwa namna ya pekee, nachukua fursa hii, kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ni mpya, lakini kwa muda mfupi ambao tumefanya nayo Kazi, imekuwa ni ya msaada sana katika Ofisi yetu. Imani yetu ni kwamba, kama tutaendelea kwa utaratibu ambao wanaufanya,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

basi baada ya muda mfupi TAMISEMI itakuwa imeondokana na kero nyingi ambazo inalalamikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara tu ilipoanzishwa Kamati hii, tumekaa nayo, tumefanya nayo mikutano mbalimbali, tumefanya nayo semina. Kwanza, kwa madhumuni ya kuwawezesha Wajumbe kufahamu majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Taasisi zilizopo chini yake. Baada ya hapo wameweza kuzitembelea Taasisi mbalimbali, kujua majukumu yao, changamoto na jinsi ya kufanya nazo kazi.

Ndiyo maana nasema kwamba, Kamati hii ni ya msaada mkubwa sana kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ninapenda kuchukua fursa hii pia, kumpongeza Spika pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuamua kuianzisha Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imetoa ushauri mbalimbali ambao na mimi ningependa nichangie. Kimsingi, ningesema tu ushauri tumeupokea na tunaenda kuufanyia kazi. Napenda nichangie na mimi katika baadhi ya vipengele ambavyo Kamati imevzungumzia. Eneo la kwanza, Kamati imetushauri tutenge pesa za kutosha kwa ajili ya kujenga miundombinu katika maeneo mapya ya utawala hasa mikoa na wilaya ambazo tumezianzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Ofisi yangu na kwa maana ya Serikali, imetenga pesa kwa ajili ya kujenga miundombinu katika maeneo hayo na tayari tumeainisha maeneo ambayo yatajenga makazi ya nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na majengo ya maeneo mapya. Tathmini imeshafanyika na pesa za fidia tayari tumeshapeleka. Michoro nayo tayari imeshaandaliwa na tayari tumeshafanya makubaliano na Wizara ya Ujenzi kupitia TBA na wameshatupa gharama zao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

Hivi sasa tulikuwa tunaainisha maeneo ambayo tunataka ni Wilaya zipi na Mikoa ipi waende wakaanze kujenga. Wiki hii tutawakabidhi TBA ili kazi hiyo ianze. Kwa hiyo, agizo hili tumelizingatia na tutaendelea kutekeleza kuhakikisha kwamba, kazi katika maeneo haya ya kuanzisha maeneo mapya inakwenda kwa wakati kama ambavyo tumejipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilizungumzwa na Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wachangiaji wengine ni kwamba, uwiano wa mgawanyo wa fedha za matengenezo ya barabara baina ya TANROAD na Ofisi ya Serikali za Mitaa, uangaliwe upya. Kwa hivi sasa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapata asilimia 30 na zinazobaki asilimia 70 ndizo zinazokwenda Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari ametafutwa Mshauri Mwelekezi ambaye anafanya utafiti na kuangalia uwiano huu ili tuone kama kutakuwa na uwezekano wa kuuangalia upya. Mategemeo yetu ni kwamba, Mtaalam atakapomaliza kazi yake ni dhahiri kwa vyovyote uwiano huu utaangaliwa. Kwa sababu sasa hivi mtandao wa barabara katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa umeongezeka kutoka kilometa 56,000 hadi kilometa 99,000. Kwa hiyo, tuna uhakika kabisa kwamba, uwiano utaangaliwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilitolewa na Kamati ambayo imezungumzwa ni suala la eneo Jengo la *Machinga Complex* kwamba liangaliwe na miundombinu iboreshwe. Kwa kuwa Kamati ilishatupatia maelekezo haya kabla ya leo, tayari NSSF na Jiji la Dar es Salaam kwa usimamizi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, wanaendelea na mazungumzo ili kuhakikisha kwamba, maeneo yenye changamoto yote yanafanyiwa kazi na kurekebishwa.

Pia Kamati imependekeza kwamba, tuangalie uwezekano wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Ilala

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

kukaa pamoja na kuona uwezekano wa soko lingine la Manispaa ya Ilala liondoshwe eneo lile ili Wafanyabiashara wote waende katika Jengo la *Machinga Complex*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukuhakikishia kwamba, suala hili linafanyiwa kazi na nina imani kabisa kwamba, watafikia mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imezungumzwa hapa ni suala la msongamano wa magari ya Dar es Salaam kwamba, pamoja na kwamba tunajenga mtandao wa mabasi yaendayo haraka, basi tuhakikishe tunaweka na utaratibu mwingine wa tozo ili kupunguza msongamano na ili kupunguza magari ambayo yanatembea viti vikiwa vitupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo ni zuri na sisi tunaliunga mkono, kwa sababu nchi nyingi ukienda utaratibu huo upo. Kwamba, katika muda fulani, uelekeo fulani huwa una tozo na lile tozo huwa linaongezeka kadiri muda wa msogamano unavyokuwa. Barabara hizi pekee haziwezi zikawa mwarubaini, kwa hiyo, lazima kuwe na mbinu nyingi ambazo zitaweza kutusaidia kuhakikisha msongamano katika Jiji la Dar es Salaam unaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa pia suala la migogoro baina ya Mamea na Wakurugenzi na mfano ukatolewa katika Jiji la Arusha na Manispaa ya Ilala.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikuhakikishie kwamba, Kamati ilienda Arusha na mimi mwenyewe nilienda Arusha, nilikaa na Mheshimiwa Meya wa Jiji la Arusha na Mkurugenzi wa Jiji la Arusha. Napenda nikuhakikishie kwamba, sasa hivi Mkurugenzi wa Jiji la Arusha na Meya, hawana mgogoro tena, wanafanya kazi kwa pamoja na wanashirikiana. Vilevile suala la Manispaa ya Ilala pia tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limezungumzwa sana kwamba, tuangalie uwezekano wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

Halmashauri zetu kuongeza makusanyo yao badala ya kutegemea ruzuku tu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumefanya utafiti katika Manispaa za mfano thelathini na tumeangalia maeneo mapya ambayo yanaweza yakapanua wigo wa makusayo au kuongeza vyanzo katika Halmashauri zetu. Hivi sasa tunaendelea kuandaa miongozo ambayo tutapeleka katika Halmashauri ili nayo pia iweze kufanyia kazi katika maeneo hayo. Lengo ni kuhakikisha kwamba, makusanyo katika Halmashauri yanaongezeka. Vilevile tumeanzisha mfumo katika Miji saba na katika baadhi ya Halmashauri, lengo ni kuhakikisha Miji yote sasa hivi inakuwa na mfumo wa kukusanya mapato kwa njia za kielektroniki.

Mfumo huo umefanya vizuri katika Manispaa ya Temeke na sasa hivi unafanya vizuri sana katika Jiji la Arusha. Tayari kwa kupitia wafadhili mbalimbali mfano *JIZ*, wametusaidia mtandao huu katika Manispaa, kuweka mifumo ya ukusanyaji wa mapato (*e-Tax*) katika Manispaa ya Mtwara Mikindani, Jiji la Tanga na katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi nikajibu hoja zote lakini kimsingi niseme tu kwamba, naunga mkono hoja na naliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, tutaendelea kuzifanyia kazi hoja zote na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati na wachangiaji mbalimbali. Niendeleee tena kwa mara nyingine kuishukuru Kamati kwa ushirikiano mkubwa sana ambao inatupatia katika utendaji wetu wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho katika hoja ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Nianze kwa kuwashukuru wote waliochangia kwa kusema na waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, naomba radhi, asubuhi ilikuwa tulete Kitabu cha Kamati yetu, hakikutoka kutokana na matatizo ya uchapaji kwenye *Hansard*. Naomba radhi sana, tutajitahidi ikiwezekana kesho kitabu kitoke Waheshimiwa Wabunge wakipate.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Katika hotuba yangu asubuhi hapa nilijitahidi kuwa *very brief* kwa sababu mambo yalikuwa mengi. Nawashukuru sana wachangiaji na hasa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, wao wamejitahidi sana kwenda ndani, wametoa *details*. Nawashukuru mno akina Mheshimiwa Tundu lissu, Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Ntukamazina na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji walizungumza mambo mengi, nitajitahidi kwa muda huu kujaribu kugusia machache, sijui nitapewa dakika kumi na tano au thelathini? Thelathini, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mchango wa Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini. Yeye ametoa mchango wake kwa njia ya maandishi, ametoa mengi na mengine yamejibiwa na Mheshimwa Waziri. Yeye binafsi alikuwa analalamikia Mahakimu kukaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi na ameeleza vizuri sana kwamba, hii inapunguza ufanisi na anapendekeza uhamisho wa mara kwa mara wa Mahakimu kwamba, wawe wanahamishwa ili wasijenge mazoea na wasizoeane na watu wanaoishi maeneo hayo. Ushauri huo ni mzuri sana, Kamati inaupokea na tunaishauri Serikali ilichukue

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA)]
pendekezo hili na ilifanyie kazi kwa umakini wa hali ya juu sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Kafullila.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji mwingine alikuwa Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, ambaye ni maarufu kama *senior citizen*. Yeye amezungumzia mambo mengi, lakini kwanza ameongelea mambo yafuatayo:-

Amezungumza kwa kirefu sana kuhusu Ofisi ya Rais (Ikulu). Amesema kwamba, Ofisi hii ndiyo kioo cha Utumishi hapa nchini na hivyo inapaswa kuteua Watumishi makini, walio hodari, wasiopenda rushwa na wachapa kazi. Pia amesitiza sana kwamba, wateuliwe kutokana na sifa na siyo kufuata ukabila, urafiki na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii hakuna ubishi kwamba, mtu yeyote ataiafiki, Kamati tumekubali ni ushauri mzuri sana, ingawa siamini kwamba, Ofisi ya Rais imekuwa ikiteua kwa urafiki au ukabila. Naishauri Serikali kama jambo hili linajitokeza, basi iwe makini na ichukue ushauri huu, izingatie Ofisi ya Rais kama alivyosema ni kioo cha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Mheshimiwa Ntukamazina aliingia ndani zaidi ni eneo la *TASAF*, *MKURABITA* na *MKUKUTA*, ambazo zipo chini ya Ofisi ya Rais na hizi zinafanya kazi nzuri sana. Amependekeza kwamba, zitengewe fedha za kutosha ili zisaidie kuondoa umaskini hapa nchini. Pendekezo hili tunalikubali sana kwa sababu sisi tumekuwa tukikagua *TASAF* na *MKURABITA*, tumekuta wana matatizo ya kifedha. Tunaishauri Serikali ijitahidi kutenga fedha za kutosha katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili limechangiwa pia na Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe na amekuwa akichangia sana katika Kamati yetu. Yeye ametaka *MKURABITA* kuharakisha upimaji wa ardhi. Kwamba, upimaji wa ardhi umekuwa ukisuasua na ameitaka Serikali ifanye haraka sana kuhakikisha viwanja na mashamba ya Wananchi yaliyoko vijijini yasipimwe kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA)
vipande vipande, yapimwe kwa Wananchi wote wa Tanzania ili waweze kutumia hati za mashamba yao kukopa fedha na kujiondoa katika wimbi la umaskini.

Nampongeza Mheshimiwa Mkosamali, kwa mchango mzuri sana wenye afya. Kamati inatoa ushauri kwamba, Serikali iufanyie kazi mpango huu na kupima mashamba ya Wananchi vijijini haraka sana na kuwapatia hati zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, ametoa ushauri mwingine mzuri sana. Yeye ameshauri kwamba, Watumishi wa Umma wawe na mtazamo chanya, wabadili fikra zao za Kiutumishi. Pia ameshauri Mpango wa *OPRAS* uwafikie Watumishi wa ngazi zote kuanzia chini hadi juu. Tunaposema chini, kuanzia huko Wilayani kuja Mkoani mpaka ngazi ya Taifa. Kwa maana ya Makatibu Wakuu, Mawaziri wote wapimwe tu utendaji wao wa Kazi.

Ameshauri pia Sekretarieti ya Umma iajiri kwa kufuata vigezo, sifa na uwezo. Mtu asiajiriwe kindugu, kikabila na kidini. Tuangalie sifa zake, ana sifa gani, ana uwezo kiasi gani, ndiyo mtu huyu aweze kupata ajira. Mheshimiwa Ntukamazina, anapendekeza sifa na uwezo viwe vigezo pekee vya ajira. Tunamshukuru sana, Kamati inakubaliana na pia Serikali tunaishauri iwe makini katika eneo hili ambalo ni nyeti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mchango mwingine wa Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, yeye amezungumza mambo mengi lakini nitagusia machache. Kwanza, amezungumza kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Ameitaka Serikali itoe kauli Bungeni kuhusu *Biometric Voter Register Tender* na ieleze hatua za kiuwajibikaji zilizochukuliwa dhidi ya Watendaji wa *NEC* waliotoa Zabuni hii bila kufuata utaratibu wa Kisheria na Kanuni. Kimsingi, hoja hii ni nzuri, lakini namshukuru sana Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi, amejitahidi kulieleza kwa mapana sana na wote tumeelimika, tunamshukuru

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA)
Mheshimiwa Lukuvi ametoa majibu mazuri na pia Kamati inashauri tusiishie hapo.

Kwa kuwa hii haikuwa hoja ambayo imeletwa na Kamati hapa Bungeni, Kamati yenyewe inataka kujiridhisha kwanza. Kwa hiyo, tunasema kwamba, Kamati itafuatilia kujua ukweli wa ushauri huu. Tukishajua ukweli tutakuwa katika nafasi ya kuishauri Serikali hatua za kuchukua katika mapendekezo ya Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha Mjini na Mheshimiwa Zitto Kabwe, walichangia kuhusiana na Mabilioni ya Uswisi, ambayo yameelezwa pia na Mheshimiwa Waziri. Kuhusu mabilioni haya wanaeleza kwamba, yalitoroshwa na Watanzania wasio waaminifu na kufichwa Nchini Uswisi na Visiwa vya Geze. Katika hili Kamati inamshauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwanza, tumpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa juhudi kubwa sana anazozifanya na Serikali yako, tumeridhishwa na maelezo yako mazuri sana, tunakupongeza. Tunasema isiishie hapo, endeleeni na mtakapopata matokeo mazuri, tungependa Bunge letu hili Tukufu iljulishwe kupitia hapa na Wananchi wote wajue ukweli ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zitto Kabwe pia alizungumzia kwa kirefu sana kuhusu uhuru mpana na habari. Katika hili alizungumzia Katiba ya Ghana kwamba, inatoa uhuru mpana wa habari na alitaka kujua ni kwa nini Kamati haikutaka kueleza jambo hili katika taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme yafuatayo kwamba, Kamati ilipokwenda Ghana ilikwenda kujifunza mambo mbalimbali, kwanza, haikwenda kukopi kunakili mambo yote ya Ghana kuyaleta hapa Tanzania. Tulienda kujifunza, mambo ambayo ni mazuri tunaweza kuyachukua na mengine tunaweza tukaboresha tuka-*modify*, mambo ambayo hayaendani na taratibu za nchi yetu tunaweka pembeni. Kwa hiyo, siyo sahihi mambo yote ambayo yako kwenye Katiba ya Ghana, yatachukuliwa na Kamati kuja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA) kulishauri Bunge. Katika hili, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, kwa mara ya kwanza namshukuru sana mdogo wangu, Mheshimiwa Tundu Lissu, ameweka vizuri sana kwamba, Kamati haikwenda kuchukua yote ya Ghana kuyaleta hapa. Nakubaliana na wewe Mheshimiwa Tindu Lissu. (Makofi)]

Kamati katika ziara yake ilijitahidi kupata nyaraka mbalimbali ikiwemo Katiba ya Ghana, Katiba ya Zimbabwe na Kenya kwa ajili ya kuja kuzipitia kwa umakini kwa sababu safari ilikuwa ya siku chache, kuchambua yale ya muhimu yanayofaa tuweze kuishauri Serikali yetu. Kwa hiyo, nilitaka nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Zitto Kabwe, sisi hatutaki kukopi yote ya wenzetu, isipokuwa tunataka kujifunza na kuboresha. Tunataka Katiba yetu iwe ya mfano isiwe inafanana na watu wengine kwa kila neno na nukta.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alikuwepo mchangiaji mwingine, Mheshimiwa Fakharia Shomar. Yeye amezungumzia kwa kirefu sana kuhusiana na jengo ambalo linajengwa na *Rita*. *Rita* wanajenga jengo la ghorofa thelathini ambalo linamilikiwa kwa ubia kati ya *NSSF* pamoja na Serikali yetu. Sasa Kamati ilipotembelea pale tulikagua jengo linakwenda vizuri na jengo ni zuri sana. Kamati ilisikitishwa na mchango wa Serikali kwa wakati ule tulipotembelea, sijui sasa hivi. Iilitakiwa iwe imechangia bilioni kumi na saba za Kitanzania, lakini tulipewa taarifa kuanzia muda ule Serikali haijachangia hata shilingi moja.

Kamati ilisikitishwa sana na taarifa hiyo. Kamati inashauri na Mheshimiwa Fakharia ameshauri kwamba, Serikali itoe mchango wake haraka sana ili kuzuia riba isijitokeze katika mchango wa Serikali na mwisho tukapata matatizo katika jengo letu hili.

Vilevile Mheshimiwa Fakharia ameipongeza sana *Rita* na akasema Taasisi zingine zijitahidi kuiga mfano huu. *Rita* wamejikomboza kwa sababu watakuwa na ofisi zao, lakini pia watakodisha watapata mapato. Tunashauri na Idara zingine za Serikali na Mashirika ya Umma, kuiga mfano

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA)
huu wa kujenga majengo yao, badala ya kukaa kwenye
majengo ya kupanga na kutumia fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Fakharia pia amegusia Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na hili limezungumziwa pia na Mheshimiwa Felix Mkosamali. Wamesema kwamba, Sekretarieti hii inapewa fedha za Serikali ili ikafanye kazi, lakini tungependa Bunge tupate mrejesho wa kazi zao, kwa sababu wanavyofanya kazi sisi hatujui fedha zao zimetumika namna gani.

Mheshimiwa Mkosamali katika hoja hii pia alijaribu kuonesha kwamba, Sekretarieti ipanue wigo mpana, wasikae Dar es Salaam peke yake, waende Muhambwe, Karagwe, Songea na Ruvuma. Maadili ya Umma yasihusishe Wabunge, Makatibu Wakuu na Mawaziri peke yao, iende mpaka chini kwa Watendaji hata wa Kata, Wahasibu, Wakurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya na wengineo. Kwa hiyo, ushauri huu ni mzuri, Kamati imeuchukua na tunaishauri Serikali iuchukue na iufanyie kazi kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Fakharia pia alizungumzia habari ya Muungano. Anasema kwamba, Muungano wamekuwa wakitoa elimu ya uelimishaji kuhusu Muungano, semina mbalimbali, sasa Kamati inayohusika na masuala ya Muungano ambayo ni Kamati ya Katiba na Sheria, ingestahili nayo ijue mambo ya Muungano kwa undani kwamba, elimu hii inapotolewa basi ni vizuri na Kamati ikaalikwa ikajifunza masuala yote yanayohusu Muungano. Hoja hii ni nzuri, ina afya, tunaiafiki na tunashauri wanaohusika wazingatie kwa makini.

Mheshimiwa Felex Mkosamali pia alikuwa na mchango wake mwingine kuhusiana na TAKUKURU. Wasiwasi wake ulikuwa kwamba, TAKUKURU wanachunguza, wanakamata, wanafanya kazi nzuri na kwa kweli tumekuwa tukizungumza nao, wanafanya kazi nzuri sana na kupeleka majalada mengi kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (*DPP*). Kwa maoni yake yeye anasema, majalada yanayokwenda kwa *DPP* ni machache

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA) yanayorudishwa TAKUKURU kwa ajili ya kuwapeleka watu Mahakamani. Kwa hiyo, amekuwa na wasiwasi kwamba pengine haki haitendeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba, Sheria na Utawala, amelitolea ufafanuzi suala hili. Kamati inashauri kwamba, elimu itolewe kwa Umma, Wananchi wajue nini kazi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, nini kazi ya Mkurugenzi wa TAKUKURU na Ofisi ya TAKUKURU, mipaka yao ikoje ili kuondoa mikanganyiko ya vyombo hivi viwili. Kwa hiyo, tunashauri Serikali itoe elimu kwa Umma, Wananchi waweze kufahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji mwingine alikuwa Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mbunge wa Tarime, yeye amechangia kwa maandishi, amesisitiza juu ya Mradi wa *TASAF*. Ametoa ushauri mzuri sana, amesisitiza juu ya mambo mbalimbali kama matatu hivi. Alisema kwanza, lazima tuwe na watu sahihi na watu wenye fikra sahihi. Akasema hao wenye fikra sahihi wanaotekeleza majukumu sahihi na kwa muda mwafaka. Akasema hayo yakizingatiwa nchi yetu lazima itaondokana na umaskini. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Nyambari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyambari ameendelea kushauri kwamba, Wataalam wa *TASAF* wapate mafunzo na hasa waende kwenye nchi ya China, hasa Jimbo la Gwangdong na wajifunze katika *Department ya The Poverty Alleviation* ili waone namna gani ya kuendeleza familia zetu ambazo *TASAF* inakusudia kuziendeleza. Kimsingi, hoja hii ni nzuri sana na Kamati imeikubali. Naamini Serikali itachukua ushauri wa Mheshimiwa Nyambari kwamba, Wataalam waende huko China wakajifunze. Elimu haina mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Nyambari amechangia kuhusu Tume ya Mipango. Anashauri kuwa, Tume ya Mipango iwe na wepesi wa kufikiri fikra sahihi, ambazo zitajenga nchi yetu ili *concept* ya *The Big Results*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA)
Now iweze kufikiwa. Vilevile anashauri wasio na uwezo wa kufikiri haraka na kuangalia njia ya halali ya kutatua tatizo waondolewe mara moja kwenye Tume ya Mipango. Kamati inakubaliana naye kwa asilimia kubwa. Tunaishauri Serikali hoja hii iende nayo, tunataka watu wanaofikiri haraka sana na kutoa ushauri, siyo watu ambao wanakalia maamuzi yanayochukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji wetu mwingine alikuwa Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido. Amezungumzia masuala mbalimbali na moja alilolizungumza ni uhaba wa Mahakimu na hasa katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya katika Jimbo lake la Longido. Amesisitiza kwamba, Mahakimu hata kama wapo, lakini fedha hazipo za kuweza kuwajengea majengo ya Mahakama, pamoja na nyenzo za kufanyia kazi, matokeo yake wanakimbia wanaenda kukaa mijini. Ameshauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya Majengo ya Mahakama, pamoja na posho nzuri ya Mahakimu na mishahara mizuri.

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ameshauri Wazee wa Mahakama waongezwe posho yao. Posho wanayolipwa sasa hivi haitoshi ni kidogo. Posho ikiendelea kuwa ndogo ni kwamba, utendaji utakuwa hafifu sana na utaendelea kuwalaumu. Kamati inaafiki sana mapendekezo ya Mheshimiwa Laizer na tunamshukuru. Tunapendekeza na tunaishauri Serikali, iyachukue haya na kuyafanyia kazi haraka. Mishahara ni jambo la muhimu na posho ni kitu cha muhimu sana. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Laizer hakuishia hapo, amezungumzia na kushauri kwamba, Watanzania tuenzi Muungano. Muungano una manufaa sana kuliko tunavyoufikiria na kuubeza. Amependekeza tena ufanyike ukaguzi wa Miradi ya *TASAF*. Kwamba, Miradi ya *TASAF* huko vijijini inakokwenda ukaguzi ufanyike mara kwa mara kwa sababu kuna harufu ya wizi. Pia amependekeza majengo na viwanja vya Serikali vipewe hati na viendelezwe.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA)]

Mheshimiwa Laizer, tunakushukuru sana kwa maoni mazuri na tunaishauri Serikali izingatie mapendekezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji mwingine alikuwa Mheshimiwa Tundu Lissu, ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati. Yeye kwa ufupi aliongelea kwa undani sana ziara za mafunzo ya Kamati, amejitahidi ku-*summarize* na amependekeza kwamba, yoliyo mazuri tuyachukue, lakini tusije tukachukua yote ambayo tumejifunza huko nje ya nchi, kwa sababu kila nchi inatofautiana na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa mchango wake mzuri ndani ya Bunge leo na hata ndani ya Kamati, amekuwa akitoa mchango mzuri sana. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Tundu Lissu, pia ameshauri kwamba, Waraka wa Katiba uwe Waraka wa Kitaifa siyo wa upande mmoja. Amesema Waraka wa Katiba ni Waraka wa Kiasia, tunakubaliana naye sana. Kamati inasisitiza kuwa, Katiba tunayoitaka Tanzania, iwe ni Katiba ya watu wote, kwa maana ya Wakulima, Wafugaji, Wasomi, Wafanyabiashara, Wanasiasa na mtu yeyote ambaye ni Mtanzania aweze kuchangia katika Katiba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa mingi sana na kwa kuzingatia kwamba ndiyo mara yangu kwanza ninasimama hapa kuhitimisha, ningeliomba niishie hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba Bunge lako Tukufu liridhie Taarifa hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na liagize Serikali itekeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Gosbert Blandes, kwa kuhitimisha Hotuba yako uliyoitoa leo asubuhi. Kwa kweli niseme, umefanya kazi nzuri sana, tunakupongeza sana. Japo ni mara ya kwanza kufanya kazi hiyo, lakini umeifanya kwa ufanisi mkubwa sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge, nawahoji kuhusiana na Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika Taarifa hiyo.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilikubaliwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Kwa muda huu sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa niaba ya Mwenyekiti, anakuja Mheshimiwa John Lwanji. Mheshimiwa Lwanji, tafadhali una nusu saa.

MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa makofi hayo ya kunitia nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninachukua nafasi hii, kuwashukuru Wabunge kwa michango yao mizuri waliyoitoa katika kuboresha Taarifa ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe ufafanuzi kidogo kabla sijaendelea; ni kwamba, Mwanasheria Mkuu, ametuasa tusitumie maneno kuagiza au haitasita au kuitaka Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno hayo yametumika katika Taarifa yetu kwa makusudi, kwa sababu mara nyingi tuliposhauri tuliona kana kwamba ushauri haukuzingatiwa na Serikali. Kwa hiyo, tunaposhauri mpaka tunachoka tufanye nini? Hii ni Mihimili miwili tofauti, kama Mhimili mmoja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI)]

hausikii ushauri, kwa vyovyote vile itabidi tutumie maneno mengine. Kwa hiyo, ndiyo maana tumetoa maelezo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa lililojiri katika Taarifa yetu, zaidi lilikuwa ni tatizo la fedha kutokwenda kwa wakati katika Halmashauri zetu. Katika majumuisho yetu, mapendekezo yetu yaliyotolewa takribani kumi hivi, yamejibiwa matano tu. Katika Taarifa ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hiyo, lakini kuna suala hili ambalo tunalizungumzia kwamba, tuliiomba Serikali ipeleke fedha kwenye Halmashauri zote nchini hususan fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili Miradi iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichoshuhudia kule ni kilio. Miradi imefikia mahali imesimama, viporo vingi na unapowauliza wao wanachokisema ni kwamba, bwana hatujapokea fedha na ni kweli walikuwa hawajapokea fedha sisi tulipofika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *issue* nyingine ni ambayo haikuzungumzwa ni Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini, kuhakikisha zinafuatilia utelekezaji wa Miradi ya Maendeleo katika maeneo yao ili kuhakikisha Miradi inatekelezwa kwa mujibu wa Mikatiba na kuhakikisha thamani halisi ya fedha inaonekana katika Miradi hiyo. Hili halikuzungumzwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo halikuguswa ni kwamba, Kamati ilitoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha thamani ya fedha inayotumika katika Miradi ya Maendeleo, inaonekana katika Miradi husika na kwamba, Kamati haitasita kuzichukulia hatua Halmashauri zilizokiuka misingi ya Utawala Bora katika utelekezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hili hatukuwa tumesikia. Kamati ushauri mwingine au mapendekezo mengine ambayo tuliyatoa ni kwamba, Serikali ifanye jitihada za makusudi kukaa meza moja ya mazungumzo na Walimu kutatua matatizo yanayowakabili Walimu na Sekta ya Elimu kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI)]

ujumla ikiwa ni sehemu ya kutatua tatizo la kuporomoka kwa kiwango cha elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la mwisho ambalo halikuguswa tuliliainisha hilo baada ya kuona malalamiko mengi ya Waheshimiwa Wabunge. Tulisema kwamba, Serikali iyafanyie kazi malalamiko ya kila mara ya Waheshimiwa Wabunge dhidi ya Watendaji wa Halmashauri mbalimbali, kwani inaonesha wazi kuwa kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha za mali ya umma. Watendaji hawa wamegeuka kuwa mchwa wa kutafuna fedha za walipa kodi. Hili halikuguswa. Tunaiomba au tunaitaka Sekerikali iyafanyie kazi maeneo hayo yaliyobaki ambayo hayakuguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea katika michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kwamba, tunawashukuru sana kwa maoni mbalimbali yaliyotolewa. Ninaomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na waliochangia kwa maandishi na kutoa maoni yao kama ifuatavyo:-

Tunatambua mchango wa Mheshimiwa Sylvester Mabumba, ambaye katika mchango wake aliipongeza Serikali kwa kubuni Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi, kwa kuwa utasaidia kupunguza tatizo la foleni katika Jiji la Dar es Salaam. Hata hivyo, alionesha wasiwasi wake kwamba, Mradi huu hautakuwa mwarobaini wa kuondoa tatizo la foleni za magari katika Jiji la Dar es Salaam, endapo Serikali haitachukua hatua za makusudi za kuwafanya Wafanyakazi wa Dar es Salaam kutumia usafiri wa umma. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mabumba kwa ushauri huo ambao umeboresha Taarifa yetu kwa kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo lingine ambalo alikuwa amelitoa Mheshimiwa Mabumba, aliomba Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), iangalie uwezekano wa kuanzisha ada kubwa za maegesho ya magari binafsi yanayoingia katikati ya Jiji ili kuwafanya wamiliki wa magari hayo kutumia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI)]

usafiri wa umma. Nadhani pendekezo hili linaendana na pendekezo la Mheshimiwa Pauline Gekul.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo lingine lililotolewa na Mheshimiwa Mabumba, aliishauri Serikali kuhakikisha fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwenye Halmashauri zetu, zinapelekwa kwa haraka na kwa wakati ili Miradi hiyo iweze kutekelezwa kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa. Vilevile aliongelea suala la Shirika la UDA na alitoa ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kupitia Mikataba yote iliyoingiwa kati ya Shirika na Kampuni ya *Simon Group* ili kujiridhisha kama ina manufaa mapana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyefuatia kutoa mchango wake ni Mheshimiwa Godbless Lema, ambaye aligusia mambo mawili ambayo ni migogoro ya Ardhi katika Jiji la Arusha na Mradi wa *Machinga Complex*. Kwa ujumla mchango na ushauri wa Mheshimiwa Lema, ulilenga kuboresha Taarifa ya Kamati. Niseme tu kwamba, ushauri wake tumeupokea kama Kamati na tunaiomba Serikali iyafanyie kazi mapendekezo yote yaliyotolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Cecilia Pareso naye alitoa mchango wake katika eneo la Sheria Ndogo, ambapo alipendekeza mamlaka ya kuidhinisha kutumika kwa Sheria Ndogo, yaondolewe kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI na wapewe Wakuu wa Mikoa, kupunguza urasimu na ucheweshaji wa kupitisha Sheria hizi muhimu katika kuendesha Halmashauri zetu. Pia katika mchango wake alizungumzia kuhusu tatizo la migogoro ya ardhi katika Halmashauri zetu. Mheshimiwa Mbunge amelichukulia tatizo hili kuwa ni tatizo sugu na migogoro mingi ni baina ya Halmashauri na Wananchi au Mamlaka ya Vijiji na Wananchi. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge ameshauri Wizara Mama ya Ardhi, ihakikishe inafuatilia kwa karibu ufumbuzi wa matatizo ya ardhi na isimamie kwa karibu ugawaji na umilikaji wa ardhi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naye Mheshimiwa Pauline

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI)]

Gekul alizungumzia kuhusu suala la utaratibu wa Halmashauri kupeleka fedha nyingi kwenye akaunti za Watendaji wa Kata. Aliuliza ni kiasi gani kinachoruhusiwa ili kupelekwa kwenye ngazi za Watendaji wa Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli tulishuhudia wakati tulipokuwa tumetembelea Wilaya ya Kinondoni, ambako tulikuta kwenye Kata wamepeleka fedha nyingi na huku Wilayani wanasema fedha hizo zimeanza kutumika wakati kule kwenye Kata tulipofika mhusika anasema bado ile fedha ipo *intact* haijatumika. Sasa mkanganyiko huo ukatupa shaka kwamba, bila shaka kuna jambo ambalo halikuwa sahihi.

Tatizo lingine alilolizungumzia Mheshimiwa Pauline Gekul ni kama nililolizungumza mwanzo, tatizo la msongamano wa magari barabarani katika Jiji la Dar es Salaam. Aliishauri Serikali kuanzisha utaratibu wa kuzuia magari binafsi kuingia katikati ya Jiji au Serikali ianzishe utaratibu wa kutoza ada kubwa za kuegesha magari katikati ya Jiji ili kupunguza idadi ya magari na hatimaye kupunguza tatizo la foleni katika Jiji la Dar es Salaam.

Alizungumzia pia migogoro ya kiutawala baina ya Mameya na Wakurugenzi. Katika mchango wake, alitaka Serikali kuliangalia suala hili kwa umakini mkubwa na kuchukua hatua ya makusudi na haraka kutatua migogoro iliyopo bila kujali wadhifa au cheo cha mtu.

Kuhusu fedha za Miradi kutokupelekwa kwa wakati kwenye Halmashauri, Mheshimiwa Mbunge alisisitiza kuwa, tatizo hili limekuwa sugu na Serikali haipeleki fedha zilizotengwa kwenye Miradi ya Maendeleo kwa wakati na mara nyingine haipeleki kabisa.

Mheshimiwa Pauline Gekul, alizungumzia pia tatizo la barabara katika Mikoa na Halmashauri nyingi hapa nchini. Katika mchango wake kuhusu tatizo la barabara, alipendekeza kuwa, badala ya kupeleka fedha za kutengeneza barabara kwenye Halmashauri na Mikoa ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI)]

bora Serikali ikaanzisha utaratibu wa kupeleka vifaa vya ujenzi wa barabara ili Halmashauri ziweze kutengeneza barabara zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge, kwa maoni waliyopendekeza. Kuna mapendekezo pia ya ziada ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Felix Mkosamali, aliyependekeza kwamba, Kamati yetu iwasilishe Taarifa za Utendaji za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sabreena Sungura, naye amekerwa sana na migogoro ya kiutawala na ushauri mbaya wa kitaalamu uliotolewa katika ujenzi wa *Machinga Complex*.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa maoni hayo na ushauri huo uliotolewa kwa Kamati yetu, nina uhakika hii itakwenda kuboresha Taarifa yetu na tunaiomba Serikali basi ihakikishe inatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Waheshimiwa Wabunge katika kutoa ushauri wao waligusia maeneo mbalimbali ambayo ni Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mradi wa Upanuzi wa Hospitali ya Tumbi Kibaha, tatizo la migogoro ya ardhi, Utawala Bora, Mfuko wa Barabara wa Serikali za Mitaa na Mradi wa *Business Park Machinga Complex*. Pia tatizo la Barabara za Mkoa na Halmashauri na utaratibu wa kupeleka fedha nyingi za Miradi ya Maendeleo kwenye ngazi na Kata. Fedha za Miradi ya Maendeleo kutokupelekwa kwa wakati kwenye Halmashauri zetu ndiyo kilio kikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika haya yaliyozungumzwa, ukienda Hospitali ya Tumbi kule Pwani utasikitika, tena ni afadhali Hospitali ya Mkoa wa Singida, Hospitali ya Tumbi ni hoi. Tunaiomba Serikali na iliahidi kwamba, ingelitoa takribani shilingi bilioni 2.5 kila mwaka. Ilifanya hivyo, ilitimiza ahadi yake mwaka mmoja tu toka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI)]
ilipotoa ahadi mwaka 2008, lakini miaka yote iliyofuata
prorata hakuna kilichotolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ungelikiwaona wale watu, sisi tuliofika pale ni kama vifaranga vimetelekezwa na kuku, hawana la kufanya, majengo yameanza kuwa *dilapidated*. Muda mwingine wanakuwa na vifaa lakini hawawezi kuvitumia, kwa sababu majengo yenyewe hayajakamilika. Tunaiomba Serikali iondoe donda hili la macho, hakuna asiyefahamu umuhimu mkubwa wa Hospitali ya Tumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine ninakushukuru sana na hasa Mheshimiwa Spika, kwa kuona umuhimu wa kuiunda Kamati hii. Kamati hii imefanya kazi kuanzia mwezi Machi mpaka Desemba, lakini *impact* yake imekuwa *felt*. *Impact* yake imeweka alama kubwa, *landmark* kubwa mahali ambapo imetembelea. Kila mahali tulipotembelea Viongozi na Watendaji walielewa umuhimu wa Kamati. Sasa watu wengine bado wanachanganya, hawaelewi kazi za hii Kamati na kazi za Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Naomba Serikali kwa upande huu hasa Wizara husika, ijaribu kuwaelimisha Wananchi, itoe elimu kwa Wananchi waelewe. Watu hawaelewi, tunapofika sisi wanakuwa na matumbo moto wanafikiri tunakwenda kukagua hesabu zao, hapana, sisi tunakwenda kuangalia pesa au bajeti tuliyopitisha kweli zimefanya kazi. *Is there value for money?* Ndiyo kazi ambayo tunakwenda kuifanya.

Mahali ambapo tumekuta wamefanya vizuri tumewapongeza. Moshi Mjini tumewapongeza, Siha kwa Mheshimiwa Mwanri, tumewapongeza na mahali ambapo hawakufanya vizuri wamepata pilipili. Yupo kijana Mwenyekiti wetu ni hatari katika kukandamiza wale ambao ni wazembe na ambao hawakutekeleza yale ambayo walipaswa kuyatekeleza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA TAMISEMI)]

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa kutuamini na Kamati ipo imara. Nadhani watu wengi pengine hawakupata nafasi ya kuchangia, waliona kama vile zina-*overlap* yale waliyochangia katika Kamati ya LAAC iliyohitimisha jana. Nafikiri kulikuwa na mkanganyiko huo, lakini kadiri siku zinavyokwenda, nina uhakika wataelewa umuhimu wa hii Kamati na wataipa nafasi kubwa ya kufanya kazi ili kuhimiza maendeleo yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Lwanji, kwa kuhitimisha hoja yako vizuri sana na tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Sasa naomba kulihoji Bunge kwamba lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mapendekezo na Maoni ambayo yamo katika Taarifa yao.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Taarifa ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali
ilikubaliwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Wote kabisa wameafiki, kwa hiyo, Taarifa hiyo imepita na kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge, nazipongeza sana Wizara zote, ambazo zimehusika na Taarifa ambazo Kamati zake zimewasilisha leo. Nami nakubaliana na michango mizuri sana ambayo imetolewa leo.

Michango ya akina Mheshimiwa Ntukamazina, kuhusu vigezo katika ajira mbalimbali Serikalini kuzingatiwa sana na siyo tu sifa na vigezo wakati wa ajira. Vilevile wakati wa *promotions* mbalimbali ndani ya Serikali ni vizuri sifa na vigezo vikaendelea kuzingatiwa sana na tukafika mahali tukajua ni nani anayempandisha nani na kwa nini.

Tatizo kubwa sana hasa kwenye Halmashauri zetu, tunaletewa Maafisa wengi sana hadi unajiuliza hivi aliyemteua huyu anamjua kweli huyu? Sasa hilo ni tatizo! Kama ni *application* ni hiyo katika nchi utapata matatizo tu Mheshimiwa Waziri kila wakati. Kwa hiyo, ipo haja kabisa ya kuwa na *panels* nzuri na zinazoeleweka maana sasa hivi bahati nzuri wasomi ni wengi siyo kama miaka ya 60 au 70, kada nyingi sana zina wasomi wengi sana, chache sana ndiyo bado za *Nuclear Physics* lakini nyingine hizi wapo wengi sana.

Kwa hiyo, ipo haja ya kuchuja vizuri ili anayefanya kazi kwa bidii kuwa mfano ndiyo wale wanaopata *promotions*, inatia moyo. Wanapopata *promotions* watu ambao hawana juhudi yoyote inavunja moyo kila mtu, matokeo yake tutakuwa tunagombana hapa kumbe hatujui tatizo lipo wapi hasa. Tukirekebisha hapo, ninaamini inaweza ikatusaidia sana.

Katika nchi yetu pia tutambue wanaofanya kazi kwa juhudi na maarifa, kuwatambua na kuwapa zawadi, mahali pengi sana hatuwatambui, mtu anajitahidi lakini hakuna anayemwona.

Niliwahi kutoa mfano mmoja siku moja hapa watu wengine wakanicheka, nikawaambia nimefanya mambo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

mengi sana katika Jimbo langu, hutakuta mahali pamoja pameandikwa Jiwe la Msingi limewekwa na Mheshimiwa Job Ndugai, hakuna hata mahali pamoja. Kwa hiyo, siku nitakayotoka mimi *memory* yote imekwisha, kwa sababu katika utaratibu wetu tulionao, hatu-*recognise efforts*. Sasa hili lazima tulibadilishe, Watumishi wetu wanaofanya kazi nzuri tuwatambue, inatia moyo sana na wale wasiofanya vizuri basi *retrenchment* na wapo wengi wa kufanyiwa *retrenchment*.

Syndrome hii ya kuilamu Serikali kila wakati, kwa kweli Serikali ina maeneo ya kulaumiwa sasa alaumiwe nani, ndiye Baba! *Syndrome* ya Watanzania wakati mwingine imepitiliza mno, kila kitu Serikali tu.

Tuliwahi kutembelea Uganda anakotoka Rais Museveni kule Mbarara, kuna mfugaji mmoja kijana tu ana mifugo yake ya kisasa anafuga vizuri. Tulipomtembelea mmoja wa wale tuliokuwa nao katika msafara ule akamwuliza swali, ana nyumba yake nzuri na anasomesha vizuri. Wakamwuliza, unadhani Serikali ya Uganda ikufanyie nini ili kuboresha mambo yako? Alichukua muda yule kijana kujibu lile swali, akauliza unasemaje? Unadhani Serikali ikufanyie nini katika ufugaji wako ili mambo yako yaweze kuwa mazuri zaidi? Akasema Serikali? Serikali ifanye nini? Mimi siihitaji Serikali!

Baadaye akasema nimekumbuka, amani na salama basi. Kukiwa na amani na salama mambo yangu ni safi! Watanzania wangapi wakiulizwa swali hilo watajibu hivyo? Sisi kila kitu ni Serikali tu, siyo kweli! Duniani huko watu wanataka *Yes Government*, pakishakuwa na amani na salama baadhi ya watu inatosha, kwingine kote anaogelea, mazingira safi anakwenda zake mbele, lakini sisi Serikali kila kitu! Wakati mwingine tunazidi kidogo. Yapo mazingira yakishawekwa vizuri Mwananchi unasonga mbele. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, ninachotaka kukisema ni kwamba, katika kutambua *efforts* za watu, kwa mfano, *TRA*,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

wanatoa zawadi kila mwaka kwa walipa kodi wakubwa kule Dar es Salaam Kitaifa. Hawafikirii hata siku moja kutoa zawadi kwa walipa kodi wa TRA wazuri kwa kila Wilaya au kwa kila Kata, wakawatambua kwenye Kata kwamba huyu ni mlipa kodi mkubwa, watu wakaitwa wakaona alah, kumbe hili jambo lina maana. Kwa hiyo, ninachokisemea ni hicho, kuibua na kuwatambua watu wanaofanya vizuri katika *levels* mbalimbali kule waliko kwa kile kidogo wanachokifanya kama mfano kwa jamii na kwa maana hiyo unaifanya jamii nzima kuchangamka kuona kumbe jambo hili ni zuri sana. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, nawapongeza tena Kamati na Wizara zote ambazo mmehusika na suala hili la leo na tunawatakiya kila la kheri kwa kazi zenu. Kwa ratiba ya leo kazi zetu zinaishia hapa, tutaendelea na Wizara ambazo zitashughulikiwa kesho.

Kwa hatua hii sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge.

Samahani kidogo, unajua unapokuwa na muda wa kutosha inaleta tabu kidogo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, naomba nikuite.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 153 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba nitoe kauli ya kutengua Kanuni hiyo kwa maelezo yafuatayo:-

Kwa kuwa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge wa kushughulikia Taarifa za mwaka za Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa umepangwa kumalizika tarehe 20 Desemba, 2013;

Na kwa kuwa ratiba ya shughuli za Mkutano huu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

inaonesha kuwa Kamati zisizopungua mbili zinawasilisha Taarifa zake kwa siku moja;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, muda wa kujadili hoja uliowasilishwa Bungeni ni dakika zisizozidi 15;

Na kwa kuwa kwa kutenga dakika 15 za kuchangia kutatoa nafasi Wabunge wachache tu kuchangia katika Taarifa za Kamati ambapo Wabunge watakaopata nafasi ya kuchangia kwa siku hawatazidi kumi;

Na kwa kuwa ili kuongeza idadi ya wachangiaji inabidi kupunguza muda wa uchangiaji kwa kutenga dakika kumi za kuchangia badala ya 15;

Na kwa kuwa ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake kikamilifu na wakati huohuo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi kupata fursa ya kujadili Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge inabidi kutengua Kauni ya 62(1)(a) inayotoa maelezo ya muda usiozidi dakika 15 za uchangiaji;

Hivyo basi, Bunge lako Tukufu linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Nne, Kanuni ya 62(1)(a) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 62(1)(a) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Mbunge anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15, itenguliwe na badala yake utumike muda usiozidi dakika kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na mapendekezo haya aliyotusomea Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, yaliafikiwa na Kamati ya Uongozi. Kwa hiyo, yanaletwa mbele yenu na sababu yake ni kwamba, Ripoti nyingi hizi tutazisoma kwa siku moja moja. Wabunge mnaotaka kusema mnajiandikisha, lakini kwa kutumia dakika 15 wachache sana wanapata nafasi. Tunadhani kwa kutumia dakika hizi ambazo zimependekezwa, tunaweza tukawapa fursa Wabunge wengi zaidi.

Kwa pendekezo hilo, naomba muamue hoja iliyotolewa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Hoja ya kutengua Kanuni iliafikiwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuanzia kesho uchangiaji wetu utakuwa ni dakika kumi kama mlivyoamua.

Sasa naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.31 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 13 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*